# NAFASI YA WAHUSIKA WAZEE KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI

**BETT KIPLIMO ANDREW**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SAYANSI ZA JAMII KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI, YA CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**NOVEMBER 2024**

Mount Kenya University

## UNGAMO NA IDHINI

### Ungamo la Mwanafunzi

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo chochote Kikuu kwingine.

Sahihi: ……………… ………………….. Tarehe: ...09/0112024.......................................

Bett Kiplimo A.

MAKI/2022/51273

Mount Kenya University

### Idhini ya Msimamizi

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

Dkt. Joseph Kariuki Gakuo

Chuo Kikuu Kishirikishi cha Bomet

Sahihi ………… ….. Tarehe:. 09/11/2024.........

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza nafasi ya wazee katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni *Mkamandume* (Said A. Mohammed 2013) na *Tumaini* (Clara Momanyi 2006). Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni; Kutambua sifa za wahusika wazee katika riwaya teule, Kuchunguza mchango wa wahusika wazee katika kuendeleza maudhui katika riwaya za *Mkamandume (2013) na Tumaini(2006)*, na kubainisha jinsi wahusika wazee wamefanikisha matumizi ya fani katika riwaya za *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006).* Utafiti huu uliongozwa na nadharia mseto ambayo ni: uhalisia na umuundo katika kukusanya na kuhakiki data. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka kwenye riwaya mbili zilizoteuliwa. Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo ikiwa na maana kuwa ulichunguza sifa zinazobainika za jambo linalotafitiwa. Utafiti huu ulifanyika kwenye maktaba. Mtafiti alisoma vitabu viwili pamoja na makala mengine yaliyomsaidia kukidhi dhamira ya utafiti. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia njia ya uchambuzi wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Adam (2014) hii ni mbinu ambayo humpa mtafiti idhini ya kusoma au kuisikiliza kazi ya fasihi, kutambua maudhui, mtazamo na falsafa ya kazi hii pamoja na mambo mengine muhimu. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kupitia maelezo baada ya kuchanganuliwa. Maelezo haya yalijikita katika ufafanuzi wa nafasi ya wahusika wazee katika riwaya zilizoteuliwa. Utafiti huu ulibaini kuwa wahusika wazee wametumika katika kukuza na kuendeleza maudhui mbalimbali, kuonyesha hulka za wahusika wazee na hatimaye kufanikisha matumizi ya fani mbalimbali katika riwaya zilizotafitiwa. Utafiti huu ni wa manufaa kwa wachanganuzi wa masuala ya kijamii yanayohusu wazee katika jamii, mashirika yasiyo ya kiserikali na ya kiserikali yanayoshughulikia wazee kupata uelewa zaidi kuhusu hali za wazee na nafasi yao katika jamii. Watafiti, wasomi na wahakiki wa fasihi watafaidika na utafiti huu kwa kuwa unachangia kujaza mapengo katika utafiti hasa kuhusu wahusika wazee.


Mount Kenya University

## ABSTRACT

This study intended to examine the role of the elderly characters in two Kiswahili novels, Mkamandume (Said A. Mohammed 2013) and Tumaini (Clara Momanyi 2006). The objectives of this research were; Identifying the characteristics of the elderly characters Investigating the contribution of elderly characters in developing the themes in the novels of Mkamandume (2013) and Tumaini (2006), and identifying how the elderly characters have enabled the authors to use various stylistic devices in the novels of Mkamandume (2013) and Tumaini(2006). This research was guided by a hybrid theory that is realism and structuralism in collecting and reviewing data. Research data was collected from the two selected novels. This research was descriptive in the sense that it examined the specific characteristics of the subject being researched. This research was done in the library. The researcher read two books as well as other articles that helped him meet the set objectives. The research data was analyzed using descriptive analysis method. According to Adam (2014) this is a method of analysis that allows the researcher to read or listen to the literary work, understand the content, perspective and philosophy of this work among other important things. The study results were presented in a descriptive manner after analysis. This study contentrated on defining the role of elderly characters in the nominated novels. The study findings show that, the elderly characters play a role in thematic development, showing of character traits of the elderly and lastly enables the author to use various stylistic devices. This study is useful to analysts of social issues concerning the elderly in society, non-governmental and governmental organizations dealing with the elderly to be well conversant with the conditions of the elderly and their position in society. Scholars, researchers and reviewers of literary works will be among the beneficiaris of this research as it provides more insight in this area.


Mount Kenya University

## YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ... ii
IKISIRI ... iii
ABSTRACT ... iv
MAELEZO YA ISTILAHI ... x
SURA YA KWANZA ... 1
MSINGI WA UTAFITI ... 1
1.2 Suala la utafiti ... 3
1.3 Malengo ya utafiti ... 3
1.4 Maswali ya utafiti ... 3
1.5 Sababu za Kuchagua mada ... 4
1.6 Upeo na mipaka ... 5
1.7 Umuhimu wa Utafiti ... 5
1.8 Hitimisho ... 5
SURA YA PILI ... 6
MWAUO WA MAANDISHI ... 6
2.1 Utangulizi ... 6
2.2 Wahusika na Uhusika ... 6
2.2.1 Wazee Katika Jamii za Kiafrika ... 9
2.3 Maudhui ... 11
2.4 Fani ... 11
2. 5 Misingi ya Kinadharia ... 12
2.5.1 Nadharia ya Uhalisia ... 12
2.5.2 Nadharia ya Umitindo ... 14
2.6 Hitimisho ... 16
SURA YA TATU ... 17
MBINU ZA UTAFITI ... 17
3.1 Utangulizi ... 17
3.2 Muundo wa utafiti ... 17
3.3 Mahali pa utafiti ... 17
3.5 Ukusanyaji wa data ... 18
3.6 Uchanganuzi wa data ... 18
3.7 Uwasilishaji wa matokeo ... 18

Mount Kenya University

3.8 Maadili katika utafiti 18
3.9 Hitimisho 19
SURA YA NNE 20
UCHANGANUZI WA DATA, UFASIRI NA MATOKEO YA UTAFITI 20
4.1 Utangulizi 20
4.2 Wasifu wa Clara Momanyi 20
4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Tumaini (2006)* 21
4.4 Wasifu wa Said A. Mohammed 22
4.5 Muhtasari wa *Mkamandume (2013)*) 24
4.6 Sifa za wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)* 25
4.6.1 Wazee ni wenye bidii 25
4.6.2 Wazee ni wahafidhina 26
4.6.3 Wazee ni wapyoro 28
4.6.4 Wahusika wazee ni wafisadi 28
4.6.5 Wahusika wazee ni wasiri 29
4.6.6 Wenye hasira 29
4.6.7 Wahusika wazee pia ni watambuzi 30
4.6.8 Wazee ni wapatanishi na wapenda amani 31
4.6.9 Wahusika wazee ni katili 31
4.6.10 Wazee ni waoga 32
4.6.11Wahusila wazee ni wacheshi 33
4.6.12 Wenye chuki 33
4.7 Sifa za wahusika wazee katika *Mkamandume (2013)*) 33
4.7.1 Wazee ni wenye hekima 35
4.7.2 Wazee ni wenye bidii 36
4.7.3 Wazee ni wasamehevu 37
4.7.4 Wazee ni wanaharakati/watetezi wa haki 38
4.7.5 Wazee ni wenye mapenzi ya dhati 40

4.7.6 Wazee ni washauri ........................................................................................ 41
4.7.7 Wazee ni wenye dharau .................................................................................. 42
4.7.8 Wahusika wazee ni wahafidhina ..................................................................... 43
4.7.9 Wahusika wazee ni katili ................................................................................. 44
4.7.10 Wahusika wazee ni wapelelezi ..................................................................... 45
4.7.11 Wazee ni walevi na wapyoro ........................................................................ 45
4.7.12 Wazee ni wacheshi ........................................................................................ 46
4.7.13 Wazee wametamauka .................................................................................... 47
4.8 Maudhui yanayoibuliwa na kuendelezwa kupitia kwa wahusika wazee ........................ 48
4.8.0 Maudhui katika Riwaya ya *Tumaini (2006)* ........................................................ 48
4.8.1 Maudhui ya ukeketaji ...................................................................................... 48
4.8.2 Ndoa za mapema .............................................................................................. 50
4.8.3 Maudhui ya Elimu ............................................................................................ 52
4.8.4 Maudhui ya ukatili ............................................................................................ 53
4.8.5 Uongozi mbaya ................................................................................................. 54
4.8.6 Maudhui ya Bidii ............................................................................................... 55
4.8.7 Maudhui ya urafiki ............................................................................................ 56
4.8.8 Maudhui ya mila, desturi na tamaduni .............................................................. 57
4.8.9 Maudhui ya migogoro ........................................................................................ 59
4.9 Maudhui katika *Mkamandume (2013)*) ................................................................... 60
4.9.1 Maudhui ya utamaushi ....................................................................................... 60
4.9.2 Maudhui ya ukatili .............................................................................................. 61
4.9.3 Maudhui ya Uongozi mbaya ............................................................................... 62
4.9.4 Maudhui ya majuto ............................................................................................. 64
4.9.5 Maudhui ya mila na utamaduni ........................................................................... 67
4.9.6 Changamoto za uzee ........................................................................................... 69
4.9.7 Maudhui ya ukulima na changamoto zake .......................................................... 72

4.10 Fani katika Riwaya ya *Tumaini (2006)* ........ 73
4.10.1 Matumizi ya methali ........ 73
4.10.2 Matumizi ya misemo ........ 74
4.10.3 Matumizi ya Tashbihi ........ 75
4.10.4 Matumizi ya Lafudhi ........ 76
4.10.5 Mbinu ya dayalojia ........ 76
4.10.6 Matumizi ya balagha ........ 77
4.10.7 Mbinu ya majazi ........ 78
4.10.8 Matumizi ya Kinaya ........ 80
4.10.9 Mbinu ya taswira ........ 81
4.10.10 Matumizi ya Wimbo ........ 83
4.11 Fani katika *Mkamandume (2013)*) ........ 83
4.11.1 Matumizi ya jazanda ........ 83
4.11.2 Matumizi ya taswira ........ 85
4.11.3 Matumizi ya kisengere nyuma ........ 86
4.11.4 Uzungumzi nafsia ........ 87
4.11.5 Matumizi ya takriri ........ 88
4.11.6 Mbinu ya dayalojia ........ 89
4.11.7 Mbinu ya majazi ........ 90
4.11.8 Matumizi ya nyimbo ........ 91
4.12 Hitimisho ........ 93
SURA YA TANO ........ 94
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 94
5.0 Utangulizi ........ 94
5.1 Muhtasari wa utafiti ........ 94
5.2 Hitimisho la utafiti ........ 95

Mount Kenya University

5.4 Mapendekezo ... 96

5.5 Mapendekezo ya Utafiti zaidi ... 97

5.6 Hitimisho la sura ... 97

MAREJELEO ... 98

VIAMBATISHO ... 101

KIAMBATISHO 1: IDHINI YA CHUO ... 101

KIAMBATISHO II: BARUA YA CHUO ... 102

KIAMBATISHO III: IDHINI YA NACOSTI ... 103

Mount Kenya University

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Dhamira** - Lengo la mwandishi au jambo linalomsukuma mwanafasihi kutunga kazi husika. Dhamira huweza kuchukuliwa kuwa ni ujumbe ambao mwandishi amekusudia kupitisha.

**Fani** – Ufundi wa kisanaa unaotumiwa na msanii katika kazi yake ya fasihi. Fani huweza kuhusisha dhana kama vile, wahusika, lugha, mtindo, umbo na mandhari.

**Mandhari** – Hurejelea mazingira yanayotawala, eneo ambapo matukio katika kazi ya fasihi hutokea, au wakati wa hadithi ya kazi ya kifasihi inayohusika.

**Mtindo -** mtindo ni matumizi ya lugha kupitia uteuzi unaotumiwa na mwandishi mmoja katika uandishi wa matini ya aina fulani.

**Mzee** – Mtu ambaye ameishi miaka mingi na huchukuliwa kuwa mwenye hekima: aghalabu zaidi ya miaka hamsini.

**Nyenzo** – Kifaa cha kufanyia au kuwezesha shughuli fulani. Nyenzo katika utafiti huu utakuwa ukirejelea lugha kwa kuwa ndicho kinatumiwa kupitisha ujumbe.

**Uhalisia** – Nadharia inayoangazia na kueleza hali na matukio katika jamii kwa kuzingatia uthabiti wa maisha.

**Umitindo -** Nadharia inayosisitiza kwamba dunia ni umoja usiogawanyika. Dunia haikuundwa kutokana na vipande vinavyoweza kutenganishwa na kujitegemea, bali imeundwa na mahusiano ya kimfumo. Nadharia hii huchukulia fasihi kama dunia yenye viungo ambavyo hutegemeana na kujalizana.

**Umuundo** – Nadharia inayoangazia jinsi kazi fulani imeundwa au kufumwa, hujikita katika matumizi ya lugha ili kuwasilisha ujumbe ifaavyo.

**Wahusika** – Hurejelea washiriki ama viumbe waliotajwa au wanaotumika kupitisha ujumbe katika kazi yoyote ya fasihi.

**Wanarika** – Kikundi cha watu wanaotoshana kiumri na hupitia hali sawa katika maisha kama vile changamoto.

## SURA YA KWANZA

## MSINGI WA UTAFITI

### 1.0 Utangulizi

Sura hii inaweka msingi wa utafiti huu kwa kushughulikia *usuli* wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, upeo na mipakati, sababu za mada kuchaguliwa pamoja na umuhimu wa utafiti huu.

### 1.1 Usuli wa mada

Wahusika ni wale washiriki ama viumbe waliotajwa katika kazi yoyote ya fasihi (Hawthorn 2010, Wamitila 2002, Senkoro 1983). Wanaweza kuwa watu, wanyama, ndege, majini na hata viumbe wengine wa kidhahania (Kimaro 2014). Mtunzi wa kazi ya fasihi huwa na uhuru wa kuchagua wahusika ambao kwa mtazamo wake watamwezesha kuafikia malengo ya kazi yake.

Nafasi ya wahusika inarejelea wajibu ambao wahusika wametunukiwa katika kazi za kifasihi au watunzi mbalimbali. Kazi ya fasihi huwa na lengo la kupitisha ujumbe, mwandishi huwajibika kuwapa wahusika majukumu maalum ambayo mara nyingi huwiana na hulka zao. Wahusika hutumika na waandishi kwa nia mbalimbali kama vile kukuza na kuendeleza maudhui, kuendeleza fani na vilevile kufanikisha dhamira. Wahusika huwa ni wa umri tofautitofauti katika kazi ya kifasihi kama walivyo watu katika jamii. Kuna watoto, vijana, watu wazima na vilevile wazee. Wahusika hawa hutumika aghalabu kuwasilisha hali, masuala pamoja na changamoto za wanajamii wenye umri sawa na wao katika jamii. Ni dhahiri kuwa kila kikundi cha wanarika hupitia changamoto zinazotofautiana, kila kikundi vilevile huwa na majukumu tofauti katika jamii. Jukumu la wazee hutofautiana na lile la vijana.

Mzee amefasiriwa kwa namna mbalimbali na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (1990), mathalan; Ni mtu ambaye ameishi miaka mingi, aghalabu zaidi ya hamsini; pili ni mtu anayeheshimiwa kwa ajili ya cheo chake kazini au mali aliyo nayo; Tatu ni jina la heshima kwa wanaume; Na nne ni mzazi, hasa baba. Umoja wa Kimataifa hufasiri wazee kama watu waliohitimu umri wa miaka sitini na zaidi (UNHCR 2020). Hata hivyo kulingana na makala haya, mzee ni yule mtu ambaye amehitimu umri wa miaka hamsini na zaidi.

Kumetokea mabadiliko mengi katika maendeleo na mitazamo ya kijamii kuhusu wazee kutoka kipindi cha kabla ya wakoloni, kipindi cha wakoloni na nyakati za usasa ambapo utandawazi umechangia na kuathiri jamii kwa njia mbalimbali. Mabadiliko haya yameathiri nafasi ya

Mount Kenya University

wazee katika jamii. Licha ya mabadiliko haya, wazee wamebakia kuwa kiungo muhimu. Baadhi ya wazee wameishi muda mrefu na kushuhudia haya mabadiliko na hivyo kuwa vyombo vya kufafanua hayo mabadiliko na kuendeleza utamaduni wao katika nyakati hizo.

Wasomi wengi wametafiti kuhusu wahusika katika fasihi ya Kiswahili. Tafiti hizi nyingi zimeshughulikia masuala ya wahusika wa kike na chache zimeangazia wahusika wa kiume pamoja na wahusika wa aina nyingine. Baadhi yazo ni kama vile; Karimi (2022) aliyeshughulikia Nafasi ya Wahusika Wendawazimu Katika Riwaya Teule, M'ngaruthi (2019), alitafiti kuhusu Usawiri wa Wahusika Katika Mashairi Teule. Osoro (2003), aliangazia Usawiri Wa Wahusika wa Kike Katika Fasihi ya Kiswahili, Fakih (2017) naye alichunguza Mabadiliko ya Usawiri wa Wahusika Katika Riwaya Teule naye Kanwa (2022), alitathmini usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoandikwa na wanawake.

Kuna tafiti zinazowahusu wazee katika jamii za Kiafrika ambazo zimefanywa kama vile utafiti wa Chilala (2015) aliyetafiti kuhusu taswira ya wazee katika jamii za Kiafrika, Malaza ~~A~~ na Addison (2013), walitafiti kuhusu picha za wanawake wazee katika fasihi ya Kiafrika. Tafiti hizi zimeangazia wahusika wa aina nyingine ila katika fasihi ya Kiswahili, nafasi ya wazee haijashughulikiwa sana. Hivyo tafiti hizi zilimchochea mtafiti kuwa na ari ya kutaka kutafiti kuhusu nafasi ya wahusika wazee katika riwaya teule kwa kuwa kulikuwa na nafasi na haja ya kuitafiti.

Said A Mohammed ni mzawa wa Tanzania na ni mwandishi maarufu wa riwaya, hadithi fupi na mashairi ya Kiswahili. Naye Clara Momanyi ni mzawa wa Kenya. Ni msomi na mwandishi maarufu wa fasihi hasa riwaya. Waandishi hawa wamebobea katika uandishi wa kazi za kubuni na kuibua masuala mengi yanayoathiri jamii. Waandishi wa jinsia mbalimbali huweza kuwasawiri wahusika wao kwa namna tofauti. Kuna dhana kuwa waandishi wa kiume wamekuwa wakiwasawiri wanawake kwa namna hasi au kama wanyonge na pia kuwa waandisshi wa kike wamewasawiri wanaume kwa mtazamo hasi. Licha ya hayo, madai haya kulingana na utafiti wa Kanwa (2022), ni kuwa usawiri wa wahusika huathiriwa pakubwa na utamaduni uliomlea mwandishi. Kuwa katika riwaya zilizoandikwa na wanawake, wahusika wamesawiriwa kwa njia zote hasi na chanya.

Jamii mbalimbali huwa na tamaduni na mitazamo zinazofanana na pia kutofautiana kuwahusu wazee. Ili kuipata taswira kamili na mtazamo pana kuhusu suala hili mtafiti aliazimia

Mount Kenya University

kutathmini kazi kutoka jamii mbalimbalimbali na hivyo kuchagua riwaya moja iliyoandikwa na Mkenya na nyingine Mtanzania.

Mtafiti alichochewa na masuala yaliyozungumziwa hapa kutaka kuchunguza nafasi ya wahusika wazee katika riwaya teule ili kupata uelewa zaidi, mathalan; ukosefu wa utafiti kuhusu nafasi ya wahusika wazee katika riwaya, mabadiliko katika jamii kuhusu nafasi ya wazee, nafasi aali inayochukuliwa na wazee katika jamii, tajriba na mitazamo ya waandishi kutoka jamii tofauti na jinsia tofauti.

### 1.2 Suala la utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini nafasi ya wazee katika riwaya ya *Mkamandume (2013)* ya Said A. Mohammed na*Tumaini (2006)* yake Clara Momanyi. Utafiti huu ulibainisha wazee katika riwaya hizi mbili kisha kueleza na kubainisha nafasi zao. Ulichunguza jinsi wazee wanachangia katika kuendeleza maudhui kama vile uendelezaji wa mila na desturi, uhifadhi wa historia ya jamii miongoni mwa mengine. Vilevile, jinsi fani imeendelezwa kwa kutumia wazee hasa matumizi ya methali, misemo na nahau. Aidha utafiti huu ulichunguza sifa ambazo wazee wamepewa na waandishi. Tafiti nyingi zimeshughulikia aina mbalimbali za wahusika kama vile; wanawake, vijana, watoto, wendawazimu na wahusika wa kiume. Hata hivyo, kutokana na mapitio, ni wazi kuwa wahusika wazee hawajashughulikiwa na tafiti za hapo awali na hivyo utafiti huu uliweza kuziba pengo hili katika utafiti.

### 1.3 Malengo ya utafiti

i) Kuchunguza sifa za wahusika wazee katika riwaya za *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006)*.

ii) Kuchunguza mchango wa wahusika wazee katika kuendeleza maudhui katika riwaya za *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006).*

iii) Kubainisha jinsi wahusika wazee wamefanikisha fani katika riwaya za *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006).*

### 1.4 Maswali ya utafiti

i) Je, wahusika wazee wana hulka zipi katika Riwaya ya *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006)?*

ii) Je, wahusika wazee wanaendeleza maudhui yepi katika riwaya ya *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006)?*

iii) Wahusika wazee wamefanikisha vipi fani katika riwaya ya Mkamandume (2013) *na Tumaini (2006)?*

### 1.5 Sababu za Kuchagua mada

Mada hii ilichaguliwa kwa sababu kadha. Mwanzo ilitokana na umuhimu walio nao wazee katika jamii. Licha ya kuwa wazee wana nafasi adhimu katika jamii, hakuna utafiti ambao umefanywa unaoangazia nafasi ya wazee katika fasihi ya Kiswahili. Wazee ni nguzo kuu katika jamii yoyote. Wao ndio hutarajiwa kuiongoza jamii kuweza kuepukana na majanga na vilevile changamoto mbalimbali zinazowakumba wanajamii. Nafasi ya wazee katika jamii imetambuliwa tangu enzi za kale ndiposa kukafumwa methali; palipo wazee hapaharibiki jambo. Kauli hii hubeba ukweli ulio na uzito wa aina yake.

Wazee huwa na hekima kutokana na tajriba yao ya kuishi miaka mingi humu duniani. Wengi wameshuhudia mabadiliko katika jamii na pia baadhi yao wakachangia katika kuleta mabadiliko hayo. Kushuhudia huku ndiko kunawafanya kuwa johari yenye dhamana katika jamii. Wazee hawa huwa hifadhi ya hekima pamoja na matukio ya historia ya jamii yao. Wazee wamepewa nafasi na hadhi kubwa katika masuala yanayohusiana na ndoa. Wao ndio hufanya maamuzi kuhusu ndoa za wanao na vilevile katika kupeleka na kupokea posa. Mzozo unapotokea baina ya wanandoa, ni wazee ndio huitwa ili kuweza kusuluhisha.

Lugha, desturi na tamaduni za jamii huhifadhiwa na kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na wazee. Wao ndio hujua jinsi mila fulani hutekelezwa na ndio huamua ni nani ambaye anastahili kupokezwa nini na wakati upi. Halikadhalika wao ndio hutazamiwa kutoa mwongozo wakati wa majanga yanayohusishwa na kuvunjwa kwa mila itikadi za jamii. Na muhimu zaidi ni kuwa, wao ndio hutegemewa kutoa mwongozo wakati wa kuchagua viongozi katika jamii.

Licha ya wajibu mkuu walio nao wazee, baadhi yao katika miaka ya hivi karibuni, wametuhumiwa kuendeleza matendo yanayoenda kinyume na matarajio. Baadhi yao wamekuwa wakiendeleza mila ambazo zimepitwa na wakati. Kwa mfano, ukeketaji, ndoa za mapema na hata chuki miongoni mwa wanajamii. Jambo lingine lilitokana na mabadiliko ambayo yametokea katika jamii kwa miaka ya hivi karibuni. Nia kuu ni kudadisi jinsi wazee wamekumbatia na kupinga mabadiliko haya katika jamii na pia kutaka kudadisi athari ya mabadiliko haya kwa wazee. Jamii pia imeathirika kwa jumla, na mtazamo wake kuhusu wazee, hasa katika karne hii, imebadilika kwa kiasi fulani.

Utafiti huu unalenga kuweka wazi jinsi wahusika wazee wametumika katika riwaya kwa nia ya kupitisha ujumbe na kuendeleza fani. Kwa njia hii itaweza pia kudhihirisha umuhimu wa wazee katika jamii na kuonyesha baadhi ya changamoto zinazowakumba ili kuwezesha wanaohusika na masuala ya wazee kuchukua hatua mwafaka. Kwa njia hii, utafiti huu utafaidi jamii nzima.

## 1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza nafasi ya wazee katika tamthilia mbili zilizoteuliwa ambazo ni *Mkamandume* (Said A. Mohammed 2013) na *Tumaini* (Clara Momanyi 2006). Uchunguzi huu utajikita kwenye wahusika wazee wa jinsia zote. Katika kutalii nafasi ya wahusika wazee, uchunguzi huu uliangazia maudhui yanayojengwa na kupitishwa kupitia wazee; fani inavyoendelezwa na jinsi sifa za wahusika wazee. Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kuwa wazee wametengewa nafasi muhimu na kutokana tajriba ya waandishi husika.

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni wa manufaa kwa wachanganuzi wa masuala ya kijamii yanayohusu wazee katika jamii, mashirika yasiyo ya kiserikali na ya kiserikali yanayoshughulikia wazee kupata uelewa zaidi kuhusu hali za wazee na nafasi yao katika jamii. Watafiti, wasomi na wahakiki wa kazi za kifasihi watafaidika na utafiti huu kwa kuwa umechangia katika kujaza mapengo katika utafiti hasa kuhusu wahusika wazee. Utafiti huu umechangia pia katika kuhamasisha jamii kuhusu wazee na umuhimu wao, changamoto ambazo wazee hupitia katika maisha yao na pia kuibua mjadala kuhusu wahusika wazee katika vitengo tofauti tofauti kama vile vya kiusomi, kisiasa na kijamii.

## 1.8 Hitimisho

Sehemu hii ndio utangulizi na ndio msingi mkuu wa utafiti. Masuala yaliyoshughulikiwa katika sehemu hii ni usuli wa mada, suala la utafiti, malengo, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada pamoja na kuiwekea mipaka utafiti wenyewe na umuhimu wa utafiti.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia matini yaliyopo kuhusiana na mada kwa nia ya kujenga msingi bora wa utafiti utakaofanywa. Sehemu hii itaangazia yaliyoandikwa kuhusu wahusika na uhusika, wazee katika jamii za Kiafrika, maudhui, sifa za wahusika pamoja na fani.

## 2.2 Wahusika na Uhusika

Dhana ya wahusika imefasiliwa kwa njia mbalimbali kama vile; Kamusi ya TUKI (1998:169), imefasili wahusika kama watu, miti au viumbe wanaotumika kusimamia binadamu katika kazi za kifasihi. Wamitila (2002), ameandika kuhusu wahusika katika fasihi ambapo amewafafanua kuwa wahusika ni washiriki ama viumbe waliozungumziwa au kutajwa katika kazi za kifasihi; wahusika hawa ni pamoja na binadamu, wanyama, ndege, mazimwi au viumbe wengine wa kufikirika. Kazi hii ilisaidia katika kutambua wahusika katika kazi zinazotafitiwa.

Kazi ya fasihi huwa ni kazi ya kisanaa iliyo na nia ya kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu. Ujumbe huo huwasilishwa kwa kupitia lugha. Ni dhahiri kuwa binadamu pekee ndio viumbe waliotunukiwa kipawa cha kutumia lugha kuwasiliana. Ili kuwasilisha ujumbe, wahusika huumbwa na hupewa uwezo wa kutumia lugha. Wanyama, ndege, viumbe wa majini na wa kidhahania huweza kupewa huo uwezo wa kutumia lugha licha ya kuwa kwa uyakinifu hawana uwezo huo.

Fasihi kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili toleo la nne, ni uwanja unalohusisha tungo za sanaa kama vile mashairi, riwaya, tamthilia, tenzi, misemo, vitendawili, hadithi na ngano. Sanaa kwa upande mwingine unafasiliwa kama ufundi wa kupitisha hisia na fikra za binadamu kupitia matini, michoro, vinyago au uchongaji (Kamusi ya Kiswahili Sanifu 1990). Kwa kudai kuwa sanaa ni ufundi, inamaanisha kuwa, inajumuisha uvumaji na utumiaji wa vifaa au zana mbalimbali ili kupitisha ujumbe. Katika fasihi, vifaa hivi hujumuisha mbinu zinazotumiwa kufanya lugha iwe na mnato. Lugha yenyewe huwasilishwa kupitia wahusika ambao ni viumbe wa mtunzi ya kazi ya fasihi. Maelezo haya yalifaidi kazi hii kwa kumwezesha mtafiti kuchunguza jinsi lugha inavyotumiwa na wahusika katika kazi zilizoshughulikiwa.

Hill (1977), kwenye *The Romantic Imagination* anasema kuwa ubunifu wa hali ya juu ni jambo lisiloweza kuepukika katika kuhakikisha kuwa mtunzi wa fasihi amefanikiwa kusawiri wahusika kwa njia bora na kuwezesha wahusika hao kulandana na wahusika wanaopatikana katika mazingira ya kawaida. Maoni haya yanawiana na yale ya Ruo (1989) ambapo anasema kuwa maisha ya mwandishi wa fasihi na mazingira yake ya kihistoria, kisiasa, kijamii pamoja na hali za kiuchumi zinaathiriana kwa kiwango kikubwa. Hivi ina maana kuwa mwandishi huathiriwa na uzoefu wake wa maisha. Mwandishi hivyo basi huwatumia wahusika wanaopatikana katika mazingira yake halisi ili kuakisi hali yake ya maisha. Waandishi wengine waliozungumzia hili suala ni Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa wahusika ni viumbe wanaoumbwa kutoka kwa mazingira ya mtunzi ambayo yanawezakuwa ya kimaeneo, kihistoria, kijamii, kiutamaduni au ya kisiasa. Kazi hizi zitamfaa mtafiti katika kutalii uhusiano uliopo au athari ya masuala ya kijamii na kisiasa katika wahusika wa kazi zinazotafitiwa.

Msokile (1992), katika *Misingi ya Hadithi Fupi* amesema kuwa wahusika huchorwa kwa ufundi na ustadi mkubwa na mtunzi ili waweze kuakisi hali tofautitofauti za maisha ya kijamii. Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa, mtunzi huwachorea wahusika hadhira yake kwa kutumia hulka bainifu, jinsi walivyo, vitu ambavyo wanavipenda na vile hawavipendi katika maisha yao. Maandishi haya yatamsaidia mtafiti katika kudadisi sifa za wahusika.

Wahusika wa kifasihi huwa na ukuruba sana na wahusika katika jamii au watu wanaoishi katika jamii. Wahusika wa umri mbalimbali pia hutumika ili kuakisi jamii kwa ukamilifu wake. Wahusika hawa hutekeleza majukumu yanayolingana na matarajio ya jamii katika umri wao. Kazi nyingi za fasihi huwa na wahusika wanaowakilisha jamii kwa ukamilifu wake yaani, kuanzia kwa watoto, vijana, watu wazima na pia wazee, vilevile wahusika wa jinsia zote hutumika katika kazi hizi pia ingawa waandishi wachache wamewahusisha jinsia huntha katika kazi zao. Hata hivyo usawiri wa wahusika hawa huathiriwa na jinsia ya mwandishi kwa njia moja au nyingine.

Wahusika katika fasihi ni viungo muhimu sana. Viungo hivi ndivyo vinavyowezesha ujumbe kuwasilishwa. Wao huweza kutazamwa kama vipaza sauti vya mwandishi kwa kuwa hutumika kueleza aliyo nayo mwandishi moyoni mwake au akilini mwake. Senkoro (2011), amewainisha wahusika kwa njia tatu; wahusika wakuu, wadogo na bapa. Wahusika wakuu kulingana naye ni wahusika wanaotokea mara nyingi katika kazi fasihi kuanzia mwanzo hadi tamati. Wahusika hawa ndio hutumika katika kujenga maudhui ya kazi ya fasihi husika. Hawa huweza kuangaliwa kama 'midomo' ya wasanii au vipaza sauti vya watungaji. Anaendelea kusema

kuwa inawezekana kuwepo kwa wahusika wakuu zaidi ya mmoja katika kazi ya kifasihi; wakati mwingine huweza wakawa wahusika wawili au hata zaidi. Wahusika wadogo ni wale hujitokeza mara moja moja katika kazi za kifasihi ili kufanikisha na kukamilisha ulimwengu wa kazi husika. Hawa huwa nguzo muhimu katika ujenzi wa dhamira hasa zile dhamira ndogondogo. Hata hivyo wahusika hawa huweza kusaidia kuikuza lengo kuu la kazi husika, ila kwa kuwa nafasi waliyopewa ni finyu wakaitwa wahusika wadogo. Wahusika bapa ni wale ambao hawabadiliki katika kazi ya kifahisi kuanzia mwanzoni hadi tamati. Wahusika hawa huweza kuchorwa kama wa kingano ambao huwafanya wazuri kuwa wazuri kuanzia mwanzo hadi tamati na wabaya wabaki wabaya katika kisa kizima. Kazi hii itasaidia katika kutambua aina ya wahusika na majukumu waliyopewa na waandishi. Hivyo ilisaidia pia kutambua maudhui yaliyolimbikizwa wahusika wazee katika riwaya teule.

Kulingana na utafiti wa Mutua (2017), ambao uliangazia mitazamo ya waandishi wa kike na wa kiume kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia, aliweza kugundua kuwa waandishi wanawake wamewachora wahusika wa kike kwa mtazamao hasi na unaowatweza katika jamii. Kulingana naye, hali hiyo imechangiwa na athari za kitamaduni kutoka jamii ambapo mwandishi amekulia, mtazamo unaoshikiliwa pia na Kanwa (2022) katika utafiti wake. Aidha, mtafiti huyu aligundua kuwa waandishi wa kiume wamemsawiri mwanamke kwa njia tofauti. Wamemsawiri kwa njia chanya ingawa wamemnyima nafasi ya kuibuka mshindi dhidi ya mwanaume. Utafiti huu ni muhimu katika kuangazia jinsi wahusika wa kike wamesawiriwa katika riwaya ambazo mtafiti atashughulikia. Tofauti iiliyopo baina ya utafiti huu wa Mutua na huu hapa ni kuwa hapa mtafiti alijikita katika kuangazia tamthilia na vilevile alizingatia mitazamo ya waandishi.

Karimi (2022), alitafiti kuhusu nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya za Kiswahili. Alipata kuwa wahusika wendawazimu waliweza kutumika kuendeleza maudhui hasa yale ambayo yanachukuliwa kuwa miiko katika jamii miongoni mwa maudhui mengine. Vilevile utafiti wake ulidhihirisha kuwa wahusika hao waliweza kutumika katika kuendeleza mbinu za uandishi. Wahusika waliotafitiwa hapa ni wale ambao ni wendawazimu ilhali utafiti huu utajikita kwa wahusika wazee. Utafiti huu uliweza kufaidi kazi hii kwa kumwezesha mtafiti kutambua baadhi ya wajibu wa wahusika katika riwaya anayotafiti.

Kanwa (2022), alitafiti kuhusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoandikwa na wanawake. Aliweza kutambua kuwa wahusika wa kiume wamechorwa kwa njia zote mbili ambazo ni hasi na chanya. Kulingana naye waandishi huathiriwa na tamaduni zilizomlea

mwandishi na dini. Jamii nyingi zimefuata mfumo dume au kuumeni. Tofauti kuu baina ya utafiti wake na huu ni kuwa wake ulijikita kwenye mtazamo wa waandishi wa kike na kiume na vilevile hakukuwa na mipaka ya kiumri katika kazi yake. Matokeo haya yalifaidi utafiti huu kwa kuwa kitabu mojawapo kilichochunguzwa kiliandikwa na mwanamke na hivyo kuchangia mtazamo wa wahusika kutegemea jinsia ya mwandishi.

### 2.2.1 Wazee Katika Jamii za Kiafrika

Suala la uzee katika jamii za Kiafrika hasa katika fasihi halijatafitiwa sana. Madai haya yanaungwa mkono na watafiti kama vile (Chilala 2015). Hata hivyo kuna baadhi ya watafiti ambao wameangazia suala hili la uzee katika fasihi. Madai haya yanaungwa mkono na Chiangong (2018); Anasema kuwa kuwa utafiti mwingi ambao umefanywa ni katika uwanja wa sosholojia, anthropolojia na gerontolojia. Utafiti uliopo katika uwanja wa fasihi unahusiana wa mila na desturi za jamii za Kiafrika (Chiangong 2018), athari ya uzee katika mwili na uzee na utata uliopo katika kuzeeka (Pretorius 2015, Lutwama-Rukundo, Kabonesa and Nsibirano 2018, Fondo 2018).

Kuna utata katika suala la uzee na umri. Utata huu unatokana na kigezo ambacho hutumiwa kuamua kuwa mtu fulani ni mzee. Kuna wanaodai kuwa hekima alionao mtu ndio humfanya kuwa mzee kama vile Hampate Ba (1969), na wengine wanashikilia kigezo cha umri. Kuwa mtu akishafikia umri fulani huweza kuchukuliwa kuwa mzee. Umri huu kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu ni miaka hamsini. Jamii ya Kiafrika kulingana na Hampate Ba (1969), ni kuwa uzee haupimwi kwa miaka ambayo mtu ameishi bali kwa kuangazia ujuzi na hekima alionao mtu. Anaendelea kusema kuwa sio ajabu kuwa na mzee wa miaka ishirini na mtoto wa miaka sabini na mbili, kwa sababu kigezo cha msingi ni ujuzi na hekima. Hata hivyo anaendendelea kusema kuwa, walio na umri mkubwa ndio mara nyingi huwa na ujuzi na hekima ikilinganishwa na wenye umri mdogo kwa sababu ya tajiriba yao kubwa kutokana na kuishi kwingi.

Tafiti zilizofanywa kuhusu wahusika wazee ni pamoja na ile ya Danowski (2011), ambaye alitafiti kuhusu usawiri wa wahusika wazee katika fasihi ya watoto. Utafiti wake ulibaini kuwa wahusika wazee kwa kiwango kikubwa wamechorwa kwa mtazamo hasi. Hii inatokana na michoro ambayo inatumika kwenye vitabu hivi. Hata hivyo alibaini kuwa mtazamo huu hasi hautoki tu vitabuni bali pia kwenye vyombo vya habari.

Malaza na Addison (2013), katika utafiti wao kuhusu taswira ya wanawake wazee katika fasihi ya Kiafrika. wanasema kuwa mwanamke mzee katika jamii ya Kiafrika mara nyingi amechorwa kwa njia hasi. Wanawake hawa huchorwa kama watu walio wabinfasi na wasiowajali wengine hasa wadogo wao. Hata hivyo utafiti wao ulibaini kuwa wanawake wazee katika jamii ya Kiafrika wanapata fursa ya kudhihirishwa kwa njia chanya wanaume wanapodidimizwa na hali wasiyoweza kuepuka.

Hungwe na wenzake (2013), walichunguza usawiri wa uzee nchini Zimbabwe. Katika utafiti wao walibaini kuwa uzee umemithishwa na uongozi mbaya unaowagandamiza kizazi kinachojaribu kuleta mabadiliko na pia kuangamiza baadhi yao. Kutokana na uongozi mbaya, walibaini kuwa baadhi ya wazee wanakimbilia nchi Jirani ambako wanakumbwa na changamoto chungu nzima kama vile kukosa huduma muhimu, kukosa kutambuliwa na kupewa stakabadhi muhimu, magonja, kukosa matumaini na hata kuaga ugenini. Walidhihirisha pia kuwa wazee ni wahafidhina. Waliangazia pia mabadiliko yanayotokea katika jamii ambapo wazee hupelekwa kwenye vituo maalum vya kuwashughulikia jambo ambalo wanadai kuwa si desturi ya Kiafrika bali inadhihirisha athari ya mila za kigeni.

Chilala (2015), aliyeshughulikia usawiri wa wahusika wazee katika fasihi za Kiafrika. Katika utafiti wake alibaini kuwa wahusika wazee wamesawiriwa kwa njia mbalimbali. Wahusika hawa wamechorwa kwa njia Chanya na hasi. Wahusika wazee kulingana naye wamechorwa kama wenye hekima bila kuzingatia mipaka ya kijinsia, wazee wanastahili kuheshimiwa kwa kuwa wanao uwezo wa kuwalaani wadogo wao iwapo watakosa kuwaheshimu. Wahusika wengine hata hivyo wamechorwa kama waasi kwa kukosa maadili licha ya kuwa wazee na hatimaye kuwa wahusika wazee wanaheshimiwa zaidi kijijini kuliko mijini.

Tafiti hizi nyingi zimefanywa katika sehemu zingine za Kiafrika na katika nyanja tofauti. Utafiti kuhusu wahusika wazee katika riwaya au fasihi ya Kiswahili bado ni finyu sana. Utafiti mwingi wa Kiswahili umejiegemeza katika wahusika wanawake, vijana na watoto. Wazee wanaonekana kama waliosahaulika licha ya nafasi yao muhimu katika jamii. Utafti huu ulilenga kufungua na kupanua ukurasa huu katika fasihi ya Kiswahili.

Mount Kenya University

## 2.3 Maudhui

Senkoro (2011), anasema kuwa jambo linaloshughulikiwa katika fasihi pamoja na mtazamo wa msanii ni baadhi ya mambo yanayounda maudhui. Anaendelea kusema kuwa maudhui ya katika kazi ya kifasihi hujumliisha fikra na pengine maadili mbalimbali yaliyomo ndio humfanya msanii wa fasihi kubuni kazi hiyo. Haya mawazo hayazuki tu hivi hivi bali huwa na uhusiano na hali yakinifu za kiasiasa, kiuchumi na kitamaduni zinazopatikana kuathiri mfumo wa jamii husika. Msanii wa kazi ya fasihi huzungumzia hali inayomzunguka na hivyo mambo anayozungumzia yanafaa kuchambuliwa kwa kuzingatia hali ambazo zilimlea na kumkuza msanii huyo (Senkoro 2011). Msanii ni zao la jamii na hivyo utunzi wake huangazia matukio yanayoathiri jamii. Maelezo haya ni muhimu kwa kuwa utafiti huu utajikita katika kudadisi maudhui katika kazi husika. Hivyo kazi hii itamwezesha mtafiti kuweza kuzamia suala la maudhui kwa undani na pia kuweza kutambua mchango wa mazingira kwa uwasilishaji wa maudhui katika kazi hizi

Ruo (1989), anaaeleza maudhui kama dhana, fikra na habari inayopatikana katika kazi ya sanaa. Maudhui hivyo basi ni nguzo kuu katika kazi yoyote ya sanaa. Msanii huwa na msukumo wa kuwasilisha mawazo yake kwa hadhira kwa kupitia wahusika. Wahusika wanaotumiwa katika kazi ya fasihi huteuliwa kimakusudi ili kuhakikisha kuwa hakuna mkinzano baina ya kile kinachowasilishwa na yule anayewasilisha. Kazi hizi zitamfaa mtafiti katika kutambua maudhui yanayowasilisha kupitia kwa wahusika maalum hasa wazee kwa kutilia maanani wazo kuwa wahusika hawatumiwi tu kuwasilisha maudhui bali wahusika maalum hutumia kuwasilisha maudhui maalum.

## 2.4 Fani

Senkoro (2011), anafafanua fani kuwa ni ule ujuzi wa kisanaa unaoutumiwa na mtunzi katika utunzi wake. Wamitila (2008), anafafanua fani kuwa ni jumla ya mbinu, mitindo na vifaa anavyotumia mtunzi kuiwasilisha maudhui na lengo yake. Fani huweza kuhusisha vipengele kama vile, wahusika, lugha, mtindo, muundo na mandhari. Fani ndicho kiungo kikuu kinachotumiwa na mwanidishi kuwasilisha dhamira na maudhui yake. wahusika katika kazi hii ya fasihi huangaliwa kama vipaza sauti. Lugha nayo ndio nyenzo kuu ya kupisha ujumbe huo.

Muundo kulingana na Wamitila (2008), hutumiwa kufafanua jinsi kazi ya fasihi imepangwa. Mpangilio huu hujitokeza kwenye maumbo ya kazi za fasihi. Hurejelea jinsi mwandishi amepanga na kugawa kazi yake katika sura, maonyesho au vitendo. Huangazia pia mfuatano

wa matukio yake, msuko n.k. msuko unaweza ukawa sahili au changamano. Msuko sahili ni ule ambao matukio husimuliwa mojamoja kuanzia mwanzo hadi mwisho ilhali msuko changamano ni ule unaohusisha usimulizi wa kwenda mbele na kurudi nyuma.

Wamitila (2008), anafafanua mtindo kuwa idadi jumla ya mbinu na njia zinazofanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi. Mtindo hudhihirisha jinsi mtunzi wa fasihi anavyoiunda kazi yake. Huweza kujumuisha maswala kama vile kuteua na kutumia msamiati maalum, kuteua tamathali za usemi, taswira, uakifishi, sentensi na kadhalika. Mandhari nayo hurejelea mazingira ya tukio, eneo la tukio, sehemu au kipindi cha hadithi ya kazi husika ya fasihi. Anaendelea kufafanua kwamba hadithi tofauti tofauti husimuliwa kwenye muktadha fulani wa kimazingira, kiwakati, kimaeneo, na kimahali. Kazi hizi zimemwezesha mtafiti kufafanua dhana ya fani, muundo, mtindo na mandhari. Ufafanuzi huu ni muhimu kwani utamwesha mtafiti kuelewa kile anachotafiti.

Lugha nayo inaangaliwa kama nyenzo muhimu ya kazi za kifasihi kulingana na Wamitila (2008). Bila lugha, maudhui pamoja na lengo la mtunzi wa kazi ya fasihi hayawezi kuwasilishwa ili kuwafikia walenga wa kazi husika ambao ni wasomaji wake. Lugha huhusisha uteuzi wa tamathali mwafaka za usemi, uteuzi na mpangilio mzuri wa maneno, sajili za lugha, uteuzi wa nahau na misemo mbalimbali ili kufanya kazi ivutie msomaji.

**2. 5 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mseto ya Uhalisia na Umitindo.

**2.5.1 Nadharia ya Uhalisia**

Nadharia hii, hurejelea uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi (Ntarangwi 2004). Anafafanua kuwa, mwandishi anayeshikilia nadharia hii huwa na imani kuwa matokeo ya vitu halisi na ukweli anaoshikilia ni ule unaoonekana na ulio na uwezekano wa kuthibitika kwa njia mbalimbali.

Nadharia hii kulingana na Njogu na Wafula (2007), ilizuka mnamo karne ya kumi na kenda na kushika kasi sana. Ilizuka baada ya kutokea kwa mabadiliko ya viwanda yaliyotokea kule bara Ulaya. Mapinduzi haya yalisababishwa na kuwepo kwa changamoto mpya zilizoletwa na mabadiliko yaliyozushwa na mtindo mpya wa maisha. Mabadiliko haya yalikuwa pamoja na kuzuka kwa tabaka la makabwela, kuzuka na kupanuliwa kwa miji na kubadilika kwa mifumo ya uzalishaji mali.



Mount Kenya University

Nadharia iliyokuwa ikitumika katika kipindi hicho ilikuwa ni ulimbwende. Hata hivyo ulimbwende ulikosa kukidhi mahitaji ya jamii ya wakati huo. Ulimbwende haukuweza kuibua wala kushughulikia matatizo ya wanajamii katika kipindi hicho na hivyo basi kupelekea kuzuka kwa uhalisia ambao ulionekana kuzungumzia mambo bayana na kujaribu kutolea suluhu. Udhaifu mkubwa wa walimbwende ulikuwa kujikita katika mambo ya kindoto au kinjozi na kupuuza matatizo au masuala yanayoathiri jamii.

Waasisi wa nadharia hii huko ulaya ni pamoja na Rene Wellek, (1961), Hegel G. (1971). George Lukacs (1972), na Gustav Flaubert, (1990), Uhalisia umefasiriwa kwa njia mbalimbali kama vile, Holemann, (1972), anayeeleza uhalisia kama ukweli uliopo mazingirani mwake na hivyo utunzi unapaswa kuiga mazingira au hali ya dunia kwa karibu zaidi (Drabble, 1993).

Mbatiah (2001), anaeleza uhalisia kuwa ni istillahi inayorejelea njia ya kuandika inayojishughulisha na kuchora picha kamili ya maisha ya kila siku katika jamii maalum. Wamitila (2003), anadai kuwa historia ya uhalisia ni ndefu sana na ulizuka ukiwa vuguvugu la kupinga mtazamo wa ulimbwende. Anaendelea kufafanua kwamba, uhalisia ni neno lililotumiwa kifasihi kufafanua hali halisi katika jamii kwa kuangazia uchumi, siasa, jamii na tamaduni. Mawazo yake yanawiana na ya Mbatiah aliyedai kuwa uhalisia unatilia maanani kuwa uhalisia, inaweza kuangaliwa kama mkondo wa kuandika unaosisitiza usawiri wa vitushi kifasihi jinsi yalivyo katika maisha ya kijamii.

Lukacs (1963), anadai kwamba mtunzi husukumwa na ari ya kuonyesha uhalisia kikamilifu na kwa kipindi chake maalumu. Matukio, wahusika na mandhari husawiriwa kama vya kiihalisia yaani hufananisha na taswira maalum ya aushi. Wamitila (2003), akimrejelea Hegel anasema kuwa, neno uhalisia hutumika kuashiria kazi ya kifasihi ambazo zinawakilisha ulimwengu au jamii ambamo wahusika wanatekeleza na kutenda shughuli mbalimbali kutegemea wanavyochochewa na hali ya mambo wakati huo. Msokile (1993), naye anatazama uhalisia kuwa ni mtindo ambao msanii huonyesha aushi kama ulivyo.

Ntarangwi (2004), anasema kuwa, mhalisia huwa na imani kuwa kazi ya kifasihi inastahili kuwaangazia wanajamii wakiwa katika imwengu wao wa kawaida wenye matukio halisi na yanayoaminika. Hivyo taswira ambazo zinaundwa na kutumiwa na mtunzi zinafaa kuakisi hali hiyo.

Lukacs (1972), anaangazia uhalisia kama lengo kuu la msanii. Hivyo basi, mwandishi husukumwa na ari ya kuchora uhalisia kwa kikamilifu katika kipindi na mazingira maalum.

Mwandishi anapaswa kusawiri ulimwengu kama changamani na wenye ukamilifu fulani unaobadilika na wenye sheria. Katika kusawiri huku anafaa kuhakikisha kuwa wahusika wake wanashabihiana na watu wanaoishi katika jamii husika.

Mihimili ifuatayo ya uhalisia ilitumika;

i) Maisha na matukio yote katika jamii hutambuliwa na kuelezwa kupitia uhalisi wake unavyodhihirika na wala sio unavyodhaniwa. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti katika kuangazia hali za maisha zilizosawiriwa katika riwaya husika jinsi yalivyo na sio jinsi anavyofikiria, na hivyo kumwongoza katika kukusanya data na vilevile katika kuchanganua data.

ii) Kazi ya mwandishi inafaa kudhihirisha ukweli jinsi ulivyo katika mazingira halisi. Mtafiti ataongozwa na mhimili huu kuangazia masuala yanayoibuliwa katika kazi ya fasihi katika uhalisia wake. Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa ilichukuliwa kuwa na ukuruba dhahiri au wa karibu na hali halisi katika jamii.

iii) Msanii huzingatia matatizo yanayokumba jamii wakati fulani kubaini vyanzo vyake. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti katika kutambua matatizo yanayowakumba wahusika wazee katika jamii zinazoshughulikiwa katika riwaya teule. Matatizo haya yanaweza kujitokeza kupitia kwa maudhui ya kazi teule.

iv) Msanii anatarajiwa kuwasawiri wahusika wake, matukio na mandhari yanayoakisi uhalisi wa mambo katika kipindi chake. Mtafiti wa kazi hii anashughulikia wahusika wazee. Kulingana na mhimili huu, wahusika wanaosawiriwa na msanii wanafaa kuwa wale wanaokubalika na kuaminika katika jamii. Mtafiti ataongozwa na mhimili kutambua wahusika wazee kulingana na imani pamoja na mtazamo wa wanajamii na vilevile kutambua sifa zao.

Hata hivyo nadharia ya uhalisia ina upungufu katika uchunguzi wa jinsi lugha inavyotumika katika kazi ya kifasihi, hivyo, nadharia ya umitindo ulitumika kukidhi upungufu huo.

### 2.5.2 Nadharia ya Umitindo

Nadharia hii iliasisiwa na Leech (1969). Wengine walioshikilia na kuchangia maendeleo ya nadharia hii ni pamoja na Ferdinand de Saussure (1974), Buffon (1930) na Fowler (1975). Bufon (1930) anadai kuwa mtindo ni jinsi mwandishi anatumia lugha kupitisha ujumbe. Anaendelea kusema kuwa mtindo ndio humtambalisha mwandishi. Leech (1981), kwa upande wake anadai kuwa ni njia ambayo lugha hutumiwa kama mali ya mtu binafsi. Vilevile, mtindo

ni matumizi ya lugha kupitia uteuzi unaotumiwa na mwandishi mmoja katika uandishi wa matini ya aina fulani.

Nadharia hii ilipinga mtazamo wa kijadi ambao ulidai kuwa fasihi ni zao la mchango wa maswala mawili ambayo ni maudhui na fani. Mtazamo mpya unadai kuwa fasihi si mchango wa vitu viwili bali ni umbo linaloundwa kwa viungo hivyo viwili ambavyo ni maudhui na fani na kwamba kuna uwezekano wa kutenganishwa. (Njogu na Wafula 2007). Muundo na mtindo hapo awali ulichukuliwa kuwa ni visawe vilivyomaanisha lugha ambayo inatumika katika matini au mazungumzo ya kazi ya fasihi.

Nadharia ya umuundo inasisitiza kwamba dunia ni umoja usiogawanyika. Dunia haikuundwa kutokana na vipande vyenye uwezo wa kutenganishwa na kujitegemea, bali imeundwa kutokana na mahusiano ya kimfumo. Miundo hii inapaswa kufikiriwa kwa ujumla wake (Njogu na Wafula 2007). Saussure alifanyia majaribio mengi nadharia hii na kufanikiwa. Alidai kuwa lugha imeundwa kwa sehemu mbili zinazojitokeza kupitia mazungumzo: lugha dhahiri na lugha dhahania. Lugha dhahania ni lugha ambayo mara nyingi haionekani wazi, ingawa baadhi ya kanuni zake huonekana katika mazungumzo ya kila siku. Lugha dhahiri hujidhihirisha kupitia uwezo wa mtu wa kuunda sentensi nyingi kadri anavyotaka. Kwa ufupi, hii ndio lugha inayotumika.

Nadharia hii inaangalia fasihi kama muundo au umbo lililokamilika. Umbo hili huundwa kwa vipengele ambavyo haviwezi kutenganishwa. Fasihi huundwa na vipengele mbalimbali ambavyo ni pamoja na maudhui, wahusika, ploti, muktadha na lugha. Vipengele hivi hutegemeana kiasi kwamba huwezi kueleza kipengele kimoja bila kutegemea kipengele kingine. Mihimili ya nadharia hii ambayo ilitumika katika utafiti huu ni ifuatayo;

a. Muundo wa kazi ya kifasihi ndio humwezesha mtunzi kufikisha ujumbe anaokusudia. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti katika kuchunguza jinsi waandishi wa riwaya teule wametumia miundo mbalimbali katika kupitisha ujumbe wao. Kwa kuangazia kazi ya kifasihi kimuundo, mtafiti aliweza kuzingatia uhusiano uliopo baina ya matini na ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa.
b. Lugha ndiyo humwezesha mtunzi kuelewa na kueleza ujuzi wake wa utendaji na mtazamo wa jamii kuhusu maisha. Mhimili huu ulimwezesha mtafiti kuhakiki jinsi waandishi wa riwaya teule walitumia lugha na pia kumpa uwezo wa kuelewa mtazamo

wa jamii kwa kutambua mbinu mbalimbali za lugha zilizotumika na wahusika wazee. Mhimili huu pia ulimuongoza mtafiti katika uchanganuzi wa data.

Nguzo za nadharia hizi mbili zilimwongoza mtafiti katika kukusanya na kuchanganua data kwa kuzingatia jinsi waandishi wa riwaya teule walikuwa wametumia lugha kwa njia mbalimbali kuvuma na kuunda kazi zao.

### 2.6 Hitimisho

Sura hii iliangazia masuala yanayojenga msingi wa huu utafiti. Yaliyoangaziwa hapa ni pamoja na suala la wahusika na uhusika, wazee katika jamii ya Kiafrika, maudhui, fani pamoja na misingi ya kinadharia itakayoongoza huu utafiti.

Mount Kenya University

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mbinu zilizotumiwa katika utafiti. Katika sehemu hii mtafiti alishughulikia muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, jinsi alivyoteua sampuli, jinsi ya kukusanya data, njia ya kuchanganua data, namna ya kuwasilisha matokeo pamoja na maadili aliyoyazingatia.

### 3.2 Muundo wa utafiti

Utafiti uliofanywa ulikuwa wa kitaamuli na kisoroveya. Utafiti wa kitaamuli ni mtazamo unaochunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa (Kothari, 2004). Kusudi lake ni kuchunguza jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani. Utafiti wa kisoroveya unalenga kuchunguza masuala yanayofanana bila kuyalinganisha. Lengo kuu katika muundo huu ni kukusanya data na kueleza uhusiano wa vipengele mbalimbali vya data hiyo. Muundo huu ulilenga kufanikisha utafiti huu kuhusu nafasi ya wahusika wazee katika riwaya zilizoteuliwa, kwa kujikita kwenye malengo ya utafiti na mihimili ya kinadharia.

### 3.3 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanyika kwenye maktaba. Mtafiti alihitajika kusoma na kuchanganua kwa kina matini yaliyohusiana na mada. Njia hii iliwezesha kukukusanywa kwa data iliyolingana na malengo ya kazi hii pamoja na kuzingatia mihimili ya kinadharia. Mtafiti atalenga kukusanya data za aina mbili ambazo ni data ya kimsingi na ya upili. Data ya msingi ilipatikana kutoka kwenye riwaya teule ilhali data ya upili ilipatikana kwenye nakala na machapisho pamoja na tasnifu ambazo zimefanywa tayari. Data ya kimsingi ilipatikana kwa kusoma *Mkamandume (2013)*) pamoja na *Tumaini (2006).* Data hii ilijumuisha maneno, sentensi pamoja aya zilizomwezesha mtafiti kutambua na kuthibitisha au kutetea hoja alizonazo.

### 3.4 Uteuzi wa sampuli

Mtafiti alitumia uteuzi wa kusudio ili kupata riwaya mbili alizoziteua kuzishughulikia ambazo ni *Mkamandume* (2013) na *Tumaini (2006)*. Mtafiti alikuwa na nia ya kuchunguza wahusika wazee katika riwaya za Kiswahili. Hivyo hatua ya kwanza ilikuwa ni kutambua riwaya zinazoshughulikia masuala ya wazee. Pili mtafiti alikuwa na lengo la kuangazia jinsi wazee wamesawiriwa na waandishi wa jinsia tofauti ili kupata taswira kamili ya mambo na hivyo akafikia uamuzi wa kuteua mwandishi mmoja wa kiume na mwingine wa kike. Vilevile, mtafiti

alikusudia kupata maoni kutoka jamii mbalimbali, hivyo aliteua riwaya moja iliyoandikwa na Mkenya na nyingine ya Mtanzania. Mtafiti hatimaye, alikusudia kuchunguza vitabu ambavyo vimeandikwa na waandishi hawa kwa miaka ya hivi karibuni na ambayo masuala ya wazee yameshughulikiwa kwa mapana.

### 3.5 Ukusanyaji wa data

Data ilikusanywa kupitia usomaji wa riwaya teule za *Mkamandume (2013) na Tumaini (2006).* Mtafiti alisoma riwaya hizi mbili, kisha atakusanya data ambayo ilihusisha vifungu vya maneno na kauli ambazo zilimwezesha kutambua wahusika wazee katika riwaya hizi mbili, kutambua na kuthibitisha sifa za wahusika hawa na kisha kutambua maudhui yanayokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa wahusika wazee, na hatimaye mbinu za lugha na tamathali za kiusemi zilizotumiwa na wahusika wazee. Data ya upili itakusanywa kupitia usomaji wa makala na machapisho yaliyo na habari kuhusu wahusika wazee, nadharia ya uhalisia pamoja na ndharia ya umitindo.

### 3.6 Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa ilikuwa inahusisha vifungu vya maneno na kauli za wahusika mbalimbali. Mtafiti alichanganua data hii kwa kupanga data aliyokusanya katika makundi manne ambayo ni; data iliyo na habari kuhusu au inayotambulisha wahusika wazee, data inayodhihirisha maudhui, data inayoonyesha fani, na hatimaye data inayotambulisha sifa za wahusika wazee. Baada ya kugawa data hii, mtafiti alifafanua data hii kwa kujikita kwenye malengo na mihimili ya kinadharia ambapo, atatambua maudhui yaliyowasilishwa kupitia wahusika wazee, pili alitambua na kufafanua sifa za kimtindo zilizotumika na sifa za wahusika wazee katika riwaya teule.

### 3.7 Uwasilishaji wa matokeo

Baada ya data kuchanganuliwa, matokeo yaliwasilishwa kupitia maelezo. Maelezo haya yalijikita kwenye ufafanuzi wa nafasi ya wahusika wazee katika riwaya ya *Mkamandume* (2013) *na Tumaini (2006)*. Uwasilishaji huu ulifanywa kwa kujikita kwenye maswali ya utafiti, malengo na mihimili ya nadharia ya uhalisia pamoja na umitindo.

### 3.8 Maadili katika utafiti

Katika kazi hii, mtafiti alihakikisha kuwa amepata vibali mbalimbali kama vilivyohitajika katika viwango mbalimbali vya utafiti kutoka kwa idara husika kama vile kutoka Chuo Kikuu cha Mount Kenya pamoja na taasisi inayoshughulikia masuala ya utafiti (NACOSTI) ili kuanza

kukusanya data na kuendelea na utafiti. Katika uchanganuzi wa data, mtafiti alihakikisha kuwa data iliyochanganuliwa ni ile iliyokusanywa kutoka kwenye riwaya teule pekee bila kuongeza au kutoa kwingine ili kuhakikisha kuwa matokeo yake yalikuwa ya kweli na ya kutegemewa. Mtafiti pia alikikisha kuwa ametambua mawazo ya watu wengine kama vile maneno na mafungu ya maneno kwa kutaja majina yao na kuhakikisha kuwa kazi zote zilizorejelewa zimeonyeshwa kikamilifu katika marejeleo ili kuepuka wizi wa kitaaluma. Mtafiti pia alihakikisha kuwa habari iliyokusanywa ilitumika kwa njia nzuri pasi na kudhulumu au kuathiri yeyote kwa njia mbaya hasa walengwa wa utafiti huu.

### 3.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia masuala muhimu yaliyoongoza utekelezaji wa utafiti. Mambo ambayo yamejadiliwa katika sura hii ni muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, njia ya kuteua sampuli, mbinu za kukusanya na kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo, pamoja na maadili yaliyozingatiwa na mtafiti.

Mount Kenya University

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA, UFASIRI NA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Sura hii iliangazia wasifu wa waandishi wa riwaya teule, muhtasari wa riwaya teule, sifa za wahusika, maudhui yaliyowasilishwa kupitia wahusika wazee na mbinu za lugha zilizofanikishwa kwa kutumia wahusika wazee.

## 4.2 Wasifu wa Clara Momanyi

Clara Momanyi ni Profesa Kiswahili na Isimu na hufunza katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki (CUEA). Aliwahi kuhudumu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta katika Shule ya Sanaa na Sayansi za Kijamii, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, na akawa mwenyekiti wa idara ya ukuzaji mtaala wa Kiswahili katika chuo hicho. Ana shahada ya Ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, shahada ya uzamili, katika somo la Kiswahili, na Uzamifu katika somo la Fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta. Pia aliwahi kuhudumu kama mweka hazina wa Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki, katibu mkuu wa Chama cha Kitaifa cha Kiswahili cha Kenya, mkaguzi mwandamizi wa Kiswahili, mwandishi wa fasihi ya Kiswahili na ametafsiri zaidi ya machapisho ishirini, na mwanachama mwandamizi wa tawi la Kenya la Chama cha Wanawake wa Kiafrika kwa Utafiti na Maendeleo.

Amechapisha na kuhariri makala mbalimbali ambazo ni pamoja na: mhariri mwenza wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili, mwaka 2006 na Njogu K. na M. Mathooko, "The Effects of Persians on the Kiswahili Language" katika The Guide, Journal of East Africa (vol.11 no. 11, Dec/Jan. 2004), "Swala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili" katika Utafiti wa Kiswahili, Eldoret Chama cha Kiswahili cha Taifa, 2002, "The History of the Wataveta: The Hidden Reality" katika Fabula, Journal of Folklore Studies (Berlin, 2002), Ronald Ngala: Teacher with a Mission, 2001, Tamathali katika Vitendawili  2001).

Baadhi ya hadithi na riwaya alizoandika ni pamoja na; *Mchezo wa Kobole* (1990), *Nakuruto* (1995), *Siku ya Wajinga mwaka* (2005), "*Ngome ya Nafsi*" katika *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Nyuso za Shetani* (2011), *Wingu Jeusi* (2014), *Maisha ni Hamu* (2015), *Mwisho wa Tamaa* (2016) na riwaya ya *Tumaini* 2006 miongoni mwa kazi nyingine nyingi za kitaaluma na kibunifu.

### 4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Tumaini (2006)*

Riwaya ya Tumaini iliandikwa na Clara Momanyi kuchapishwa mwaka 2006. Riwaya hii inazungumzia utamaduni unaoendelezwa na wazee na jinsi unavyoathiri malezi ya watoto. Mhusika mkuu ni Tumaini, bintiye Mzee Masumbuko na Bi. Amina. Mzee Masumbuko anaamini sana katika utamaduni na yuko tayari kufanya lolote kulinda utamaduni huo. Katika jamii yao, msichana anatakiwa kupashwa tohara na kuolewa. Mzee Masumbuko anaamua kumpasha Tumaini tohara anapoelekea darasa la nane. Tumaini hafurahia uamuzi huo kwani alijua angekatizwa masomo yake na badala yake kuolewa.

Hadithi inapoanza, tunampata Tumaini akitoroka usiku kutoka nyumbani kwa sababu babake hakuelewa azma yake ya kuendelea na masomo. Mamake alikuwa hawezi kumsaidia kwa kuwa alimuogopa Mzee Masumbuko na hivyo aliridhia chochote alichosema. Tumaini alihiari kukimbilia kwa shangazi yake, Bi. Halima, aliyeishi mtaa wa Miembeni na ndiye aliyedhamini masomo hivyo Tumaini alijua kuwa huyu ndiye angemsaidia.

Mzee Masumbuko alipogundua kuwa Tumaini ametoroka, alimfukuza mkewe Bi. Amina, akimtaka amtafute Tumaini. Bi. Amina alienda kwa kakake Yusufu kumtafuta Tumaini. Idi, kaka yake Tumaini, alitumwa kwa Bi. Halima kumtafuta Tumaini na alipomkuta, alimwongelesha kwa dharau kwa kukwepa tohara. Baada ya Bi. Amina kumkosa Tumaini kwa Yusufu, aliamua kwenda kwa dadake Bi. Halima ambapo alimpata. Bi. Amina na Bi. Halima walipanga jinsi ya kumsaidia Tumaini kuendelea na masomo bila kumfahamisha Mzee Masumbuko.

Mzee Masumbuko aliendelea na mipango yake ya kutaka kumwoza bintiye baada ya kukosa kumpasha tohara na hivyo aliamua kumtafutia Tumaini mume mbali na kwao ili kuepuka vitisho vya ndugu zake. Alitembelea rafiki yake wa zamani, Sulemani bin Mabruk, na kupanga kumpa Tumaini mume. Baada ya juma moja, Mzee Masumbuko alirejea nyumbani na kumjulisha mkewe kuwa baada ya siku tatu wageni wangefika, bila kueleza nia yao.

Siku ya wageni kufika, wazee walikusanyika nyumbani kwa Mzee Masumbuko. Wageni walipoeleza nia yao ya kuleta posa ya Mabruk kwa Tumaini, Yusufu alikasirika na kumhoji Mzee Masumbuko kwa nini anamposa mtoto wao mchanga ambaye bado anasoma.

Tumaini aliendelea na masomo yake kwa bidii. Baada ya kumaliza mtihani wa darasa la nane, alienda kuomba kazi kama kijakazi kwa Chifu Andrea. Bi. Selina, mke wa Chifu, alimpenda

sana. Hata hivyo, Chifu Andrea na mwanawe Majuto walijaribu kumdhulumu, jambo lililomsikitisha sana Tumaini na kumfanya arudi kwa Bi. Halima. Majibu ya mtihani wa darasa la nane yalipotoka, Tumaini alifuzu na alikuwa miongoni mwa wanafunzi watano waliochaguliwa kujiunga na shule ya upili na kupokea ufadhili. Babake aliungana na Chifu Andrea kupanga njama ya kumtoa Tumaini kwenye orodha ya wanaopata ufadhili, lakini Tumaini aligundua njama hiyo na akaazimia kutibua mpango huo na hatimaye akafaulu kupata ufadhili.

Tumaini alijiunga na Milimani Mission School na alitia bidii sana, hasa katika masomo ya Sayansi kwani alitaka kuwa daktari. Binamu yake Riziki alijiunga na chuo cha ualimu baada ya kidato cha nne. Waliweza kusoma bila shida kutokana na hazina aliyokuwa ameipata Shabani.Dada zake Tumaini hawakupata elimu kutokana na tamaa ya babake. Mashaka alifanya vizuri katika mtihani wa darasa la nane lakini hakuwahi kuendelea na masomo baada ya kuolewa na Mzee Lusimbo kwa lazima kama mke wa tatu. Rehema naye hakumaliza darasa la nane kwani aliolewa baada ya kupokea posa. Majuto, mwana wa Chifu Andrea, alikuwa mtukutu na aliacha shule na kuanza wizi, mwishowe akafungwa.

Tumaini alifanya vyema katika mtihani wa kidato cha nne na alichaguliwa kujiunga na chuo kikuu kusomea udaktari wa tiba. Sifa, rafiki yake, alichaguliwa kusomea udaktari wa meno. Tumaini na Sifa walibaki marafiki na walikubaliana kuendeleza mapenzi yao baada ya kumaliza masomo. Riwaya hii inaonyesha jinsi utamaduni unaoshikiliwa na kuendelezwa na wazee katika jamii inavyoathiri malezi ya watoto na athari za malezi hayo.

### 4.4 Wasifu wa Said A. Mohammed

Alizaliwa Pemba, Zanzibar mnamo Desemba 12, 1947. Hakupata malezi ya baba na mama kwani wazazi wake walitengana akiwa na umri mdogo sana na kumfanye alelewe na mama zake "wakubwa", Bi Jokha na Bi Rukia. Alisomea Shule ya maghulamu ya Wete, Pemba kabla ya kuhamia Kiembe Samaki kisha Darajani, Unguja alikohitimu elimu ya shule ya msingi na kujiunga na shule ya upili ya Gulioni ambayo awali iliitwa King George The VI, na hatimaye kujiunga na Chuo cha Ualimu cha Nkurumah, Zanzibar mnamo 1966. Alipata fursa ya kufunza baada ya kuhitimu Ualimu mnamo 1966 katika shule ya msingi ya Kizimbani kwa muda mfupi kisha akahitajika kwenda kufundisha Biolojia, Hisabati, Kemia na Kiswahili katika shule ya upili ya Utaani hadi 1974. Alijiunga na shule ya International Correspondence alikosomea masomo ya Sanaa katika kiwango cha Kidato cha Tano na Sita.

Alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka wa 1976, kusomea Shahada ya kwanza katika Elimu. Alijikita katika Isimu na Fasihi ya Kiswahili. Alisomea shahada ya uzamili katika Isimu Tekelezi katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Said alisomea shahada ya Uzamifu (PhD) Ujerumani katika Chuo Kikuu cha Karl Marx Leipzig, kuanzia mwaka wa 1981 hadi 1985.

Amewahi kuhudumu kama Rais wa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI) Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA). Amefunza vyuo mbalimbali kama mhadhiri kama vile Chuo Kikuu cha Moi Eldoret mwaka wa 1987 na baadaye kufundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi hadi 1990. Baadaye alienda Ujapani katika Chuo Kikuu cha Osaka akiwa Mkuu wa Idara ya Lugha za Kigeni. Baada ya kupata Uprofesa alihamia Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani alikofundisha Kiswahili kati ya 1997 na 2012.

Said alipenda kusoma, kutunga mashairi na hadithi fupi tangu alipokuwa mwanafunzi wa darasa la tano. Alitunga shairi moja lililopata umaarufu sana lililopewa mada *'Nimfuge Ndege Gani Ili Nipate Salama'* 1960. Alishajiishwa na walimu wake, Mohamed Abdallah na Kindi Abubakary kutunga mashairi na hadithi. Kipawa chake cha uandishi anadai kuw aalirithi kutoka kwa mama yake "mkubwa" aliyekuwa nyakanga na alikuwa bingwa wa kuimba nyimbo za unyago. Elimu ya Dini ya Kiislamu ambayo alipata kutoka kwenye madrassa ulichangia pakubwa katika uandishi wake.

Ametunga mashairi ambayo yamechapishwa katika diwani mbalimbali zikiwa ni pamoja na *Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) *na Jicho la Ndani* (2002), kazi zinazozungumzia masuala ya kisiasa, kiuchumi, mapenzi na utamaduni. Ametunga riwaya na tamthilia zaidi ya 60 ambazo ni pamoja na; *Utengano* (1980) *Kiza Katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990), *Kivuli Kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Babu Alipofufuka* (2001) na *Sadiki Ukipenda* (2002), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2004), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Dunia Yao* (2006), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012), *Gharama ya Amani* (2014*), Mashetani Wamerudi* (2016) na *Mkamadume* (2013). *Mkamandume (2013)* ni riwaya inayoangazia vipindi tatu tofauti vya kisiasa na wenye wahusika wa kihalisia.

Mount Kenya University

### 4.5 Muhtasari wa *Mkamandume (2013))*

*Mkamandume (2013))* inachunguza vipindi vitatu vya utawala tofauti: kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, na baada ya ukoloni. Hadithi inaanza kwa kuelezea asili ya Mkamandume, mhusika mkuu, na historia ya nchi ya Malelejimema. Inasemekana kuwa watu wa kwanza walitoa jina hilo kwa nchi hiyo. Kizazi cha kwanza kilitokana na viwiliwili viwili vilivyopuliziwa roho, ambavyo baadaye vilibadilika kuwa mwanamume na mwanamke. Malelejimema ilijengwa juu ya misingi ya wema ambayo iliwavutia wageni kutoka sehemu mbalimbali.

Mkamandume alikuwa na familia iliyojumuisha mkewe Tufaa, watoto wake Time, Fikirini, Mtumwa, Msimu, Viwe, Katija, na mamake Bi. Fuu. Mkamandume alibadilika ghafla katika ndoa yake, jambo lililomshangaza mkewe. Hali hii ilionekana alipomwadhibu binti yake Viwe kikatili baada ya kugundua alikuwa mjamzito, hali iliyopelekea kutengana na Viwe.

Kazini, Mkamandume alidhulumiwa na bosi wake. Alifanya kazi ya kusafisha vyoo bila vifaa vya kutosha, hali iliyomfanya kazi hiyo kuwa ngumu zaidi. Tuzo ya mfanyakazi bora ilitolewa kwa upendeleo na licha ya bidii yake, Mkamandume hakutuzwa hata mara moja. Tuzo hiyo ilimwendea Zuhura Saleh Mcheshi kinyume na matarajio ya wengi.

Hatimaye, Mkamandume alipewa likizo ya miezi mitatu bila malipo, jambo lililomkasirisha sana na kumfanya awe na uhasama dhidi ya bosi wake. Alianza kulipiza kisasi dhidi ya maadui zake wa zamani akiwemo baba yake Soud, ambaye alimkataa alipomposa binti yake, Time. Licha ya uhasama huo, Soud alijitolea kumsaidia Mkamandume kwa hali yoyote ngumu aliyokutana nayo ikiwemo kumlipia gharama ya chakula.

Mzee Mkasi na Bw. Sleyyum wanamsimulia Soud masaibu yaliyowakumba wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Mzee Mkasi hakutaka kukumbuka vita vya pili vya dunia vilivyokuwa vya kikatili. Aliwapoteza mkewe Biti Sahera na mwanawe Masudi katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Alieleza jinsi alivyodhulumiwa wakati wa vita vya ukombozi nchini Malelejimema na kuteswa kizuizini bila hatia.

Mkamandume alisafiri kwenda makao makuu kumtafuta binti yake Viwe. Njiani alipoteza fahamu na kuokolewa na wavuvi. Alishangazwa na mabadiliko ya makao makuu kwani yalikuwa bora kuliko Malelejimema. Alikutana na Soud hotelini baada ya kushindwa kulipia gharama ya chakula. Soud alimlipia na kumjulisha maendeleo yake na Nadia. Pia, alikutana na

mwanawe Viwe ambaye alikuwa amebadilika na kuwa msomi na mwanabiashara. Alishirikiana na Soud kuanzisha michezo ya tamthilia ya kuwazindua wanajamii.

Mwishowe, Mkamandume alirudi Msera kukabiliana na adui yake Bw. Shombo. Baada ya kumkata shingo, alimwendea bosi wake na kumwangamiza kisha akaungana na waandamanaji ambao waliongozwa na Soud, Time, Mzee Mponda, Mtumwa, Msimu, Viwe, Mzee Mkasi na Bwan' Sleyyum. Polisi waliwavamia waandamanaji hao na kuwafyatulia risasi, Mkamandume anajirusha mbele kumkinga Soud na anapoteza uhai wake ambaye aliangamia alipomkinga Soud. Soud, Viwe na Time wanatoroshwa na kufichwa ili wasikamatwe na polisi wanaowatafuta tokea siku ya maandamano.

### 4.6 Sifa za wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)*

Wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)* wamechorwa kwa namna mbalimbali. Kuna wale waliochorwa kama waasi na wengine wamechorwa kwa njia Chanya. Wahusika wanaodhirika kuwa wazee katika riwaya hii ni pamoja na Mzee Masumbuko, Mzee Sulemani, Mzee Sudi, Mzee Okwemba, Mzee Chumo, Mzee Lusimbo, Mzee Seyai na Mzee Majungu. Majina na majukumu yanayotekelezwa na wahusika hawa pamoja na jinsi mwandishi amewarejelea hudhirisha wazi kuwa ni wazee katika hii jamii. Sifa za wazee hawa ni kama zifuatazo;

#### 4.6.1 Wazee ni wenye bidii

Wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)* wamechorwa kama watu walio na bidii maishani. Wao ndio hutekeleza majukumu mengi yanayohusiana na uteagaji Uchumi ili familia zao zipate angalau chakula na pia karo za shule. Wazee katika riwaya hii wanatia bidii na kujihusisha na ukulima wa aina mbalimbali na vilevile kujihusisha na biashara ya ndizi. Kwa mfano Mzee Masumbuko anajishughulisha na ukulima wa mimea mbalimbali kama vile migomba, miboga, mamumunye, matiki, mihindi na mimea ya pamba.

> Kutokana na umbo lililoshitadi siha na nguvu, mzee huyu alipoingia shambani alilima mithili ya trekta. Alikata miti, akafyeka magugu na kupiga matuta utadhani kapagawa. Jasho lilipapa juu ya kipaji chake na upara kung'aa zaidi. Kutokana na ukakamavu wake katika kilimo, shamba lake liliguna kwa wingi wa mavuno. Aidha aliatika aina mbalimbnali za migomba kama vile mkono wa tembo, mkojozi, kigurue, mzungu mwekundu hata kisukari.
>
> Upande mwingine wa shamba mzee huyu aliatika miboga. Mamumunye, na matiki yalinawiri kutokana na huduma zake pevu. Baada ya kukamilisha kazi kondeni mwake, Mzee Masumbuko aliindea konde nyingine mlimokuwa na mihindi na mimea ya pamba. Uk 12 – 13.

Mount Kenya University

Mzee Sulemani pia anadhihirisha kama mtu aliye na bidii kwa kujihusisha na biashara. Mzee huyu alipata kujuana na Mzee Masumbuko kupitia biashara.

> Sulemani alikuwa mchuuzi huko Maungujan a harakati zake biashara Mombasa zilimkutanisha na Mzee Masumbuko, ambaye aghalabu alimtembelea. Urafiki shadidi uliimarika kati ya wazee hao, wakawa hawana siri kati yao.
>
> Uk 51

Mzee mwingine aliyepewa sifa hii ni Mzee Okwemba. Licha ya umri wake kwenda sana hali inayodhihirika kutokana na ulegevu mwilini anapopinda na uchache wa meno anapocheka, mzee huyu anajishughulisha na biashara ya kuchuuza Samaki. Samaki hao anawatoa mbali kunako mabwawa ya maji;

> Mzee Okwemba aliyasitiri maisha yake kwa kuchuuza Samaki. Shaibu huyu alikuwa akitembea mwendo mrefu kwenye mabwawa ya maji ambako shughuli za uvuvi ziliendelea. Huko alijinunulia Samaki na kuwachuuza mtaani humo. Uk 3

Ni dhahiri kuwa wazee katika riwaya hii wameonyeshwa kama watu walio bidii. Wanajihusisha na shughuli mbalimbali ili kujipatia kipato na pia ili kuendesha maisha yao na pia ya familia zao.

### 4.6.2 Wazee ni wahafidhina

Wazee katika riwaya hii wamepewa sifa ya uhafidhina. Mhafidhina kulingana na Kamusi Teule ya Kiswahili (2014), ni mtu ambaye hushikilia mila, tamaduni na kaida za zamani na akakataa kubadilika. Baadhi ya wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)*, wamedhihirsha sifa hii. Wahusika hawa ni pamoja na Mzee Masumbuko anayeshikilia mila kuwa mtoto msichana anapaswa kupashwa tohara na kuoleka. Imani hii yake ndiyo inayoleta mgogoro mkubwa baina yake na mwanawe Tumaini ambaye anahiari kutoroka kwao. Kutoroka huko hakukumzuia babake kuendelea na mipango ya kumpasha tohara hadi inapombainikia kuwa Tumaini kahiari kuhama kwake. Anabadili mkondo na kuanza kupokea pos ahata hivyo hili linagonga mwamba na anaamua kufunga safari kwendda kumtafutia mume kutoka kwa rafikiye Sulemani ingawa siku ya siku, vurugu zinatokea na mipango yake kutibuliwa.

Inagwa Mzee Masumbuko hakufaulu kumpasha tohara Tumaini, dada zake wawili (Rehema na Mashaka), walimridhia mzee huyu matakwa yake na kilichofuatwa ni kuozwa kwao wakiwa na umri mdogo kama alivyojulishwa Tumaini kwenye barua aliyoandikiwa na Idi;

> Mwishoni mwa muhula alipata barua kutoka nyumbani iliyoandika na Idi. Katika barua hiyo, Tumaini alijulishwa kwamba Rehema hakujiunga na darasa la nane kwani babake aliletewa posa, na kisha Rehema akaolewa. Aliolewa na fundi wa

> baiskeli aliyeitwa Shauri. Mashaka aliamua kusoma, lakini lililomkera Tumaini ni kwamba tayari huyu alikwisha tafutiwa mchumba. Hivyo, baada ya elimu ya msingi yeye pia angeolewa.
>
> Uk 110-111.

Mashaka aliolewa kwa Mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Kuolewa kwao kulitangulizwa na kupashwa tohara kwao. Idi alitumwa na ujumbe siku moja Kwenda kuwaalika Bi. Halima na mumewe kwenye sherehe ya kupashwa tohara kwao;

> "Nimetumwa niwaambie wewe na Ba Mdogo mffike nyumbani Jumamosi- mimi na akina Mashaka tunapashwa tohara", Idi alisema huku haya zimemchachia.
>
> Uk 78

Hali hii ya kushikilia mila ya kuoza mabinti mapema si jambo lililoshikiliwa na Mzee Masumbuko pekee kwani pia Mzee Lusimbo anamuoa Mashaka kama mke wa tatu huku Mzee Chumo anasemekana kumuoa Zena kwa lazima akiwa na umri mdogo. Msichana huyu alijaribu kukataa ila alibebwa hobelahobela na vijana waliotumwa na kumpeleka akaolewe kama mke wa nne.

> Tumaini alikumbuka vyema jinsi vijana hao makatili walivyombeba Zena juu juu na kumpeleka kwa Mzee Chumo ili akawe mke wa nne. Juhudu za Zena kujiopoa ziliambulia patupu kwani vijana hao mabarubaru walimshinda nguvu.
>
> Uk 49

Mzee Sulemani pamoja na wazee walioandamana naye mathalani Mzee Sudi, wanaonekana kuwa pia na sifa hii ya uhafidhina. Mzee Masumbuko alipomwendea Mzee Sulemani na kumtaka urafiki wao ukolee zaidi kwa kumposa bintiye, Mzee Sulemani alikubali licha ya kuwa Tumaini alikuwa msichana mwenye umri mdogo. Vilevile, ndoa za kupangwa ni mila iliyopitwa na wakati ila wazee hawa bado wanathamini na kuendeleza.

Wazee pia wanashikilia imani kuwa wanawake hawafai kuingilia mazungumzo baina ya wanaume au wazee. Hali hii natokea wakati Tumaini alijitoma ndani ya mkutano uliokuwa ukijadili majina ya wanafunzi wanaostahili kufadhiliwa. Mzee mmoja anaonekana kukerwa na tabia ya tumaini;

> Mzee mmoja mwenye nywele zilizokinai mvi aliudhika na alimaka, "Eh! Haya nayo ni makubwa. Msichana huyu kapata wapi ujasiri kama huu wa kuwavunjia wazee kikao. Mamaye humfunza nini huyu?"
>
> Uk 101

### 4.6.3 Wazee ni wapyoro

Wazee pia wameonyeshwa kama wapyoro. Mpyoro ni mtu anayeweza kutumia lugha ya matusi bbila kujali anaozungumza nao. Mzee aliyedhihirisha sifa hii katika riwaya hii ni Mzee Masumbuko. Anapolewa huonekana kutumia lugha yenye matusi na pia anapokasirika anajipata akitumia matusi. Hali hii ilitokea wakati wa kikao cha kumposa Tumaini kwa Mabruk pale ambapo Yusufu aliingilia kati na kukataa kuwa mwanao hawezi akaozwa kisha kukashamiri vurugu. Mzee Masumbuko anamfanyia Yusufu ishara ya matusi licha ya kuwa miongoni mwa wazee na wanawake. Mzee Masumbuko pia anamrushia matusi Shabani matusi licha ya Shabani kumfungulia mlango;

> Shabani aliufungua mlango ili mzee huyo aweze kutoka, lakini kinyume na hayo alimiminiwa matusi mfululizo. Matusi hayo yalimkera mno Shabanii na kumhakikishia kuwa hakika ulimi unauna kuliko meno. Shabani hangeweza kustahimili maudhi hayo, na bila kumjibu lolote, alimchukua mkewe wakaenda zao huku Bi. Halima akimkumbusha mzee huyo kuwa njma zake zitagonga mwamba.
>
> Uk 64.

### 4.6.4 Wahusika wazee ni wafisadi

Ufisadi kulingana na Kamusi Teule ya Kiswahili (2014), ni tendo la kukosa uadilifu kama vile ulaji rushwa. Baadhi ya wahusika wazee kama vile Mzee Masumbuko anashiriki vitendo vya kifisadi ili kuweza kubadili mkondo wa sheria. Mzee Masumbuko alikuwa amepania kukatisha masomo ya bintiye kwa kila njia ili kufanikisha mpango wake wa kumuoza mapema. Alishirikiana na Chifu Andrea ambaye bila shaka ni mlaji rushwa na asiyejali haki za wanyonge. Mzee Masumbuko kabla ya kuja kwa wageni waliokuja kumpoza Tumaini anaonekan akimtembelea chifu jioni moja akiwa amemkokota mbuzi, lengo likiwa ni kulainisha mikono ya chifu ili asiingilie mpango wake;

> Siku moja jioni kabla ya wageni wa Mzee Masumbuko kuwasili, Bi. Halima alimwona mzee huyu akimkokota mbuzi kuelekea uani mwa Chifu Andrrea. Haya yalimshtia Bi. Halima kwani hakuelewa kwa nini Mzee Masumbuko ampelekee chifu mbuzi. Alisimama ghafla huku ameduwaa kama mtu aliyepokonywa ulimi. Bi. Halima mara kicheko kilimpasuka "Haheee, he, he, heee!" halafu akajisikia akisema, "Mngalegeza demani; chombo ki juu ya mwamba. Maajabu ya Firauni haya! Aliwaza iwapo Mzee Masumbuko alikuwa akienda kumhonga chifu ili kuufunika uovu aliotenda au aliotarajia kutenda.
>
> Uk 55

Vilevile Mzee Masumbuko anaonekana akitoka kwa Chifu huyo siku moja masaa ya magharibi. Baadaye Tumaini anabaini kuwa ziara ile ilikuwa ya kupanga njama ya kumnyima ufadhili wa kimasomo.

> Baada ya Tumaini kumtajia yale yaliyomleta pale, Bi. Selina alimdokezea kuwa wazee wale walikuwa wanaongea juu ya ufadhili wa masomo kwa wale waliofauli mtihani.
>
> "Lakini haya yanamhusu baba kwa njia gani ikiwa hakuwa na mtoto aliyefuzu isipokuwa mimi ambaye tayari alikwisha nitupa kama nguo mbovu?" aliuliza Tumaini.
>
> Bi. Selina alitulia kwa muda kisha akatamka, "Babako alikuja kumshawishi chifu ahakikishe wewe huko katika orodha ya hao watakaofadhiliwa."
>
> Uk 97

### 4.6.5 Wahusika wazee ni wasiri

Wahusika wazee pia wamechorwa kama watu wanaoweza kuhifadhi siri. Mzee Masumbuko ni mhusika anayedhihirisha sifa hii. Mpango wake wa kumpasha tohara Tumaini unapogonga mwamba na kupewa vitisho, anapanga njama ya kumuonza bintiye kwa mwana wa rafikiye aishiye Maunguja. Alifunga safari bila kumueleza yeyote nia ya safari yake, anaporudi baada ya juma moja, anamuarifu mkewe kuwa kutakuwa wageni baada siku tatu ila hakumweleza haja ya wageni hao. Nia ya kuja kwa wageni hao inabakia siri hata siku yenyewe inapofika, wale majirani na wazee waliolikwa hawaambiwi sababu ya kufika pale.

> Asubuhi siku iliyofuata, nyumbani kwa Mzee Masumbuko kulikuwa na pitapita nyingi. Wanawake walipika mseto wa mapochopocho ya vyakula, huku wazee wakipiga gumzo barazani wakisubiri wageni. Mpaka dakika hiyo, Mzee Masumbuko alikuwa hajawafahamisha wazee wenziwe dhamira ya kuja kwa wageni hao.
>
> Uk 56

Hali inabakia kuwa hiyo ya usiri hadi wakati wa mazungumzo, Mzee Sudi anapowapasulia mbarika kuhusu ujumbe wa wageni hao kuwa ni kuleta posa. Hali inakuwa tete na vurugu kushamiri.

### 4.6.6 Wenye hasira

Wahusika wazee wameumbwa kama watu wenye hasira. Katika riwaya ya *Tumaini (2006)*, Mzee Masumbuko amechorwa kama mzee aliye na wingi wa ghadhabu. Hali hii inadhihirika na jinsi ambavyo anahusiana na wahusika wengine na pia wanawe. Tumaini anapotorak nyumbani, Mzee Masumbuko anasemekana kuwa midomo ambayo alipokasirika ilichezacheza kama mtu anayetaka kupasua kicheko. Vilevile alipoingia nyumbani akiwa amelewa huuliza chakula kwa hasira;

> Aidha alipoingia nyumbani, nyumba nzima iliingia tfrani kwani alipasuka kama radi huku akiulizia chakula kwa hasira utadhani alishikiwa shokoa katika ulimaji wake ulioishia ulevini. Uk 13

Mzee Masumbuko alikuwa mwepesi wa hasira na jambo dogo lingemghadhabisha na hivyo kuwaadhibu wanawe kwa kosa lolote dogo. Tumaini anapotoroka, Idi anamtaarifu kuwa babake amekasirika na ametayarishiwa gunia huku akielekea shambani kutafuta jani la upupu;

> "Baba amekasirka Tuma! Alimwambia Mashaka amtayarishie gunia tupu kisha akachukua panga na kuelekea shambani," Idi alisema.
>
> "Jani la upupu!" alitamka Tumaini. "Upupu?"
>
> Aliuliza Riziki kwa mshangao, akimtazama mama yeke.
>
> "Naam, baba ana mazoea ya kutuadibu kwa kututia ndani ya gunia pamoja na majani ya upupu. Natumaini mnajua jinsi yanavyowasha. Baada ya kulifunga gunia ndi kwa Kamba, ndipo anapomchapa anayeadhibiwa hadi fimbo ivunjike vipandevipande."
>
> Uk 28.

Mkewe Bi. Amina anaporudi nyumbani bila Tumaini, anamkuta mumewe akimngojea akiwa amehamaki;

> Alipofika nyumbani kwake, alimkuta mumwe ameketi nje ya nyumba, ufito mkonono. Bi. Amina hakumtarajia mumewe kuwa nyumbani wakati ule isipokuwa shambani mwao. Lakini alipomtupia jicho usone, alielewa mara moja kuwa Masumbuko kajipachika pale kitini kwa shari. Macho yalikuwa yamepiga wekunda kwa ghadhabu huku midomo ikimchezamcheza. Mkewe alimsalimia lakini bdala ya kuitikia salamu hizo, Masumbuko alisimama ghafla na kumnyooshea ule ufito huku akitamkwa kwa hamaki, "Yuko wapi? Yu wapi huyo mwanao Mchuro uliyeenda kumtafuta enh? Nijibu haraka ama…" kabla mkewe hajajibu, Masumbuko alimrushia ule ufito kwa nguvu zake zote.
>
> Uk 36

Maelezo haya yanamsawiri Mzee Masumbuko kama mtu mwenye hamaki tele na asiyeweza kutuliza hasira zake.

Baada ya kutibuka kwa mpango wake wa kumuoza Tumaini kwa Mabruk, anakasirika na kuishia kuanza vurugu.

> Mzee Masumbuko hasira zilimpanda baada ya kujua nasaha zake hazikufua kitu.
>
> Uk 62

**4.6.7 Wahusika wazee pia ni watambuzi**

Mzee Okwemba ni mhusika ambaye ametunukiwa sifa hii. Mzee huyu anapomwona Tumaini akisoma barua ya Sifa aliyoletewa na Idi anabaini kuwa imetoka kwa mvulana;

> "Heee! He! He! Misichana, kijana nafurahisa we sana enh?" Mzee Okwemba alicheka na kufunua kinywa chote. Tumaini alimtazama na kucheka kutokana na

Mount Kenya University

vile mzee huyo alivyocheka. Uchache wa meno kinywani ndio uliomchekesha zaidi Tumaini kuliko hata yale yaliyokuwemo katika barua hiyo.

“Mzee umejuaje barua yatoka kwa kijana?” Tumaini alimwuliza.

Uk 130.

### 4.6.8 Wazee ni wapatanishi na wapenda amani

Wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)* pia wamechorwa kama wapatanishi na wasiopenda vurugu. Mgogoro unapozuka wakati Mzee Sulemani na wenzake walipoleta posa za Tumaini, ni wazee ndio walichukua hatua ya kujaribu kurejesha utulivu chumbani na kuwapanisha Mzee Masumbuko na shemejiye Yusufu. Wazee hawa ni pamoja na Mzee Sudi, Mzee Seyai, na Mzee Majungu;

> Alipokwisha kusema haya, kulitokea vurugu na tafrani kubwa. Vimako viliwatoka wote waliokuwa mle, isipokuwa Bi. Amina ambaye alizielewa hasira za mumewe. Yusufu bila kusema lolote aliinuka na kuishika bakora ya Mzee Masumbuko iliyokuwa karibu naye na kuigongesha kwa nguvu mezani. Kikao kile kilivurugika, watu wakaanza kutawanyika ovyo. Vilio vya mshangao vilisika miongoni mwa wale wanawake, huku wazee wakijaribu kumpokonya Yusufu ile bakora. Alitaka kuivunjia juu ya kichwa cha shemejiye akisema bakora hiyo ndiyo aliyoitumia Mzee Masumbuko ‘kumwadhibu’ dadake kwa kisingizio kuwa alimlipia mahari.
>
> “Leo utaonja utamu wa bakora hii unayompigia dadangu,” Alifoka Yusufu.
>
> “Msalie Mtume!” Mzee Sudi alisihi.
>
> Uk 63

Licha ya juhudi zao hizo kutofaulu kuwapatanisha mahasimu hawa wawili, iliweza kusaidia kuwatenganisha na kuwazuia kupigana. Kikao kile kilivunjika bila kuzaa matunda yoyote.

### 4.6.9 Wahusika wazee ni katili

Wahusika wazee wamepewa sifa ya kuwa katili. Mtu katili ni yule asiye na utu au huruma na anaweza kutenda mambo fulani ili kuathiri wengine bila kujali. Baadhi ya wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)* waliopewa sifa hii ni pamoja na Mzee Masumbuko. Mzee huyu anaonekana kukosa huruma. Anajulikana kuwa wanawe wanapokosa, yeye huwaadhibu kwa kuwatia ndani ya gunia lenye jani la upupu kisha kuwatandika hadi fimbo inapovunjika au mpita njia anapotokea na kumwombea huruma. Mzee huyu anadhihirisha sifa hii pale Tumaini alipotoroka kwao, wakati mkewe anaporudi kutoka kwa kakake, anamkuta ameketi akiwa amejawa na hasira akimngojea. Punde tu anaanza kumuuliza maswali na kisha kumrushia ufito aliyokuwa nayo mkononi nusura impate mkewe Bi. Amina. Ufito huo unatua kwenye mpaipai na kuuvunja.

> Mkewe alimsalimia lakini badala ya kuitikia salamu hizo, Masumbuko alisimama ghafla na kumnyooshea ule ufito huku akitamkwa kwa hamaki, "Yuko wapi? Yu wapi huyo mwanao Mchuro uliyeenda kumtafuta enh? Nijibu haraka ama…" kabla mkewe hajajibu, Masumbuko alimrushia ule ufito kwa nguvu zake zote. Ufito ulifyatuka kama mshale, ukayoyomea kwa Bi. Amina ambaye alichutama ghafla na kuupisha. Ufito uliupiga Dhoruba kali mpapai uliokuwa umepndwa hapi uani ukakatika vipande viwili.
>
> Uk 36

Ufito huo ungempata Bi. Amina huenda bila shaka ungemwangamiza kama sio kumjeruhi vibaya. Hata hivyo huo haukuwa mwisho wa mgogoro huo kwani Mzee Masumbuko alipoona ufito ulimkosa aliendea upanga uliokuwa karibu na mlango. Jambo hili lilimfanya kukimbilia kwa Mzee Okwemba ambapo ananusurika baada ya mzee huyo kumwelekeza Mzee Masumbuko upande mwingine hali Bi. Amina alikuwa amejificha chumbani mwake. Kando na haya inasemekana kuwa Mzee Masumbuko humpiga mkewe mara kwa mara kwa kusingizia kuwa alimlipia mahari.

### 4.6.10 Wazee ni waoga

Wazee pia wamechorwa kama watu wenye sifa ya uoga. Mzee Okwemba ni mojawapo wa wazee walioipewa sifa hii riwayani. Wakati Bi..Amina akifukuzwa na mumewe na kukimbilia kwa Mzee Okwemba, Mzee alibumburushwa usingizini na vishindo vya Bi. Amina kuingia kwake na hivyo kuanza kupiga kelele ili kuwaita majirani ghafla Mzee Masumbuko anamjia na upanga anashtuka na kupiga magoti kuomba msamaha. Hata hivyo, baada ya Mzee Masumbuko kutoka pale na Mzee Okwemba kufahamikiwa kuwa ni nani aliyekuwa mle ndani, bado anatetemeka kuashiria uoga aliokuwa nao mzee huyu.

> Mlango ulifunguliwa taratibu na Bi. Amina akachungulia nje.
>
> "Mama Toma… ni wewe! Toka mama, yeye kwisa Kwenda. Misee ile mbaya. Ye nachapa we tena," Mzee Okwemba alitamka huku akitetemeka mwili mzima kwa hofu.
>
> Uk 37.

Mount Kenya University

### 4.6.11Wahusila wazee ni wacheshi

Baadhi ya wahusika wazee wana uwezo wa kuwafanya wasomaji pamoja na wahusika wengine katika riwaya kucheka. Mhusika aliyepewa sifa hii riwayani ni Mzee Okwemba. Matamshi ya mzee huyu yameathirika kutokana na uchache wa meno kinywani mwake licha ya kuwa pia na athari ya lugha yake ya kwanza. Wanapozungumza na Tumaini, Tumaini anabaki akicheka kutokana na maneno yake na pia uchache wa meno kinywani mwake.

> "Haa! He he hee!" Mzee Okwemba alicheka huku kinywa akikiwacha wazi na kutazama anga lile la asubuhi. Tumaini naye aliitikia kicheko kwa kucheka zaidi. Sio kutokana na udamisi wa shaibu huyu bali kutokana na uchache wa meno yake.
>
> Uk 81

### 4.6.12 Wenye chuki

Wazee wamechorwa kama watu wenye chuki. Hali hii inadhihirika kutoka kwa Mzee Masumbuko ambaye anahifadhi hasira zake kwa muda mrefu licha ya aliyemwathiri kuomba msamaha. Mzee Masumbuko alimchukia Tumaini kutokea ule wakati ambapo alitoroka kwao na kukwepa tohara. Wanapokutana na Tumaini na Bi. Halima akitoka sokoni, anajibu salamu za Bi. Halima ila za Tumaini hakuzijibu. Chuki hii yake inaendelea hadi Tumaini alipopita mtihani wa kidato cha nne. Mkewe anapomtaka waende anmwambia hana mtoto kama huyo.

> "Baba Tuma, fahamu kwamba chuki humchoma anayehifadhi. Lingekuwa jambo bora zaidi iwapo ungesahau yote yaliyopita na kumtaka mwanao akuombe msamaha ikiwa kweli alikukosea. Yule nim toto wako, na siku moja atakuhitaji wewe kama mzazi wake." Bi Amina alimsihi.
>
> Tuma alinikana siku ile aliyonyanyia mguu kuhama hapa. Kwa hivyo yeye si mwanangu, unasikia? Masumbuko alisema kwa hasira.
>
> Uk 151.

## 4.7 Sifa za wahusika wazee katika *Mkamandume (2013)*)

Katika riwaya hii wazee wameweza kupewa sifa za aina mbalimbali ambazo zitatambuliwa katika sehemu hii na pia kuthibitisha kuwa wahusika wanaorejelewa ni wazee iwapo mwandishi hajawatambua kuwa ni wazee. Wahusika hawa ni pamoja na Mkamandume, Mzee Mkasi, Mzee Mponda, Bi. Reja, Bi. Mwana, Bi. Bw. Sleyyum, Babu Yakobo pamoja na wazee wa Kijiji. Wahusika hawa wanatambuliwa kuwa ni wazee kwa kigezo cha umri wao na pia kwa mwandishi kuwatambua kuwa ni wazee.

Mkamandume ambaye ni mhusika mkuu katika kisa hiki ana umri wa zaidi ya miaka hamsini. Hii inadhihirika kutokana na maelezo ya mwandishi anayesema;

> Miaka arobaini iliyopita anakumbuka alikuwa kasimama chini ya msufi pembeni mwa konde yake alipokuwa kafuatana na babake kuja kondeni hapo. Analikumbuka kama leo, lile sauti gonda la babake lilivyokuwa likimimika.
>
> Uk 23

Ni wazi kuwa umri wa Mkamandume ulizidi miaka hamsini, kwa kuwa wakati anapoenda na babake mle kondeni, bila shaka alikuwa amehitimu zaidi ya miaka kumi ndipo anao uwezo ya kuyakumbuka yale yaliyotokea mle wakati ule.

Bi. Reja naye tunaelezwa kuwa alikuwa na umri ambao bila shaka umezidi miaka hamsini. Mwandishi anasema;

> Bi. Reja mtu mzima mara kwake Tufaa, alikuwa msiri na mtatuzi wa matatizo yake- tangu ndani mpaka nje. Na hiyo si ajabu, yeye Bi. Reja ndiye aliyemfunga ubinda Bi Tufaa alipovunja ungo nay eye ndiye aliyeshuhudia baka jekundu juu ya kisero siku ya kuingia ndani kwake.
>
> Uk 99-100.

Wakunga katika jamii za kiafrika pamoja na wale wanawake wanaotekeleza majukumu ya unyumba na unyago, walitarajiwa kuwa ni watu walio na umri mkubwa au uliokomaa. Maelezo ya mwandishi pia kusema kuwa Bi. Reja alikuwa anamzidi Tufaa mara mbili au tatu, inadhihirisha kuwa Bi. Reja amezidi miaka hamsini. Mwanawe Tufaa Viwe amefikia umri wa kubaleghe hali inayomweka Tufaa baina ya miaka thelatini na arobaini. Vilevile tunaarifiwa kuwa nywele zake zilikuwa zimanza kubadili rangi;

> Alipokwisha kufikiri kidogo, aliinuka, akakaza kanga yake kifuani na ile aliyokuwa kajitanda akajipiga nayo kilemba kama vile alikuwa akificha nywele zake zilizokwisha changanya jivu.
>
> Mohammed 2013; uk 101.

Bw. Sleyyum pia amedhihirishwa kama mzee katika riwaya hii. Maneno yafuatayo yametumika kumrejelea mhusika huyu;

> Pamoja na uzito wa uzee na ubaba alioachiwa juu yake na marehemu rafiki yake. Akawa anamtazam akwa kushawishi Soud na kumwambia kwa mpasuko wa bomu la ghafla, "Lini unafikiria kuoa wewe?".
>
> Mohammed 2013; uk 66.

Wahusika wengine wametambulishwa kwa kutumia au kutaja jina mzee kabla ya kutaja jina lake, na wengine mwandishi ametaja umri wao kama Mzee Mkasi aliye na umri wa miaka sabini na tatu.

### 4.7.1 Wazee ni wenye hekima

Wahusika wazee wamechorwa kama wenye hekima katika riwaya hii. Wazee wanaodhihirsha sifa hii ni pmaoja na Mzee Mkasi na Bi. Reja. Hekima kulingana na kamusi teule ya Kiswahili (2014), kuwa ni akili ya ndani au busara. Akili hii huweza kujidhihirisha kupitia kwa ung'amuzi wa mambo, kufanya maamuzi ya busara na kwa kupitia jinsi watu wanajibu maswali fulani au kuelekeza mazungumzo kwa njia ambayo haiwezi ikamdhuru au kumwathiri anayezungumziwa.

Mzee Mkasi anadhihirisha sifa hii katika mtagusano wake na Time. Licha ya kuwa Time alikuwa mwana wa adui yake, Mzee Mkasi anamkaribisha kwake na kuwa na mazungumzo naye na kushirikiana katika shughuli mbalimbali kama vile upishi, ukulima na gumzo. Kupitia kwa mazungumzo yao, Mzee Mkasi anadhirika kuwa mwenye hekima, kwa mfano anaweza kubaini kuwa kuna jambo lililomleta Time kwake ila anaamua kutomuuliza, anamwacha mwenyewe afunguke wakati ukifika. Vilevile anapoulizwa maswali hayatoi majibu yote kwa uwazi bali anamwachia anayeuliza kuweza kutambua mwenyewe. Kwa mfano wanapozungumzia kwa nini Mzee Mkasi hapendi kuchinja, Mzee Mkasi hampi jibu la wazi na tunapata kuelezwa yafuatayo;

> Haikujulikana kwamba Time alimfahamu mzee huyu. Haikutambulikana kama hata alikuwa na haja ya kumfahamu. Kwa kawaida maneno yake ni ya kupindupindua na mkabala wake utata mtupu. Katika maneno yake katu hakupi uwazi wa ukweli moja kwa moja – ukweli uutafute wewe mwenyewe tu!
>
> Uk 167.

Mzee Mkasi vilevile anarejelewa kama Bahari ya maarifa na elimu ya mdomo, hali ambayo inawiana uwepo wa hekima;

> Alikuwa Bahari Mzee Mkasi – Bahari ya marifa na elimu ya mdomo.
>
> Mohammed 2013, 189.

Bi. Reja ni mwanamke mzee katika riwaya hii anayedhihirisha hekima kwa kiwango fulani. Mwanamke huyu anawezakung'amua changamoto anazopitia mwenzake. Kutokana na hali ambayo mwenzake anaweza kumtembelea ili kupata suluhu la jambo zito ni dhahiri kuwa huyu mwanamke ana hekima au maarifa nyingi. Tunaelezwa yafuatayo kumhusu;

> Mara pale katika Kwenda na kurudi, alikuja kusita kwa ghafla, akamtumbulia macho Tufaa aliyekuwa sasa akijifuta machozi kwani kwa kiasi fulani keshafarijika, kumpata mti aliyeweza kumwaia dukuduku lake; na tena mtu aliyemwamini na kumwona ana hazina ya mizungu na mwingi wa maarifa ya

> kidunia. Tufaa hakufunga safari kuja hapo kulia kilio cha bure. Alijua kwamba kichwa chake kilichojaa mvi kimebeba siri nyingi za maisha.
>
> Uk 102.

Malezo haya yanadhihirisha kuwa, Bi. Reja hakuwa tu na umri mkubwa bali alikuwa mwenye hekima.

**4.7.2 Wazee ni wenye bidii**

Sifa inayodhirika kwa wazee wengi katika riwaya hii ni kuwa ni watu wenye bidii. Wazee wengi wanajihusihsa na shughuli za ukulima ili kuweza kukimu familia zao au kujikimu wenyewe. Wahusika wenye sifa hii ni pamoja na Mkamandume, Mzee Mkasi naBabu Yakobo.

Babu yakobo ambaye alikuwa wa asili ya Kikamba ambaye alikuwa akiishi mkabala na kina Soud ingawa alishaiaga dunia alikuwa mzee mwenye bidii.

> Mbali kule juu, zamani kulikuwa na kibanda cha Babu Yakobo mzee wa ki-kamba aliyeimarisha konde za mihogo, migomba na miwa na vitango pepeta.
>
> Uk 53.

Mzee Mkasi naye ameonyeshwa kama mzee mwenye bidii katika ukulima. Mzee huyu anaonekana kuwa ni mtu apendaye kufanya kazi yake. Time alipokuwa akienda kwa mzee huyu tunaambiwa kuwa;

> Time alipita kwenye ujia mwembamba Katikati ya migomba iliyoiva kijani na mikungu yake ndixi iliyokuwa ikininginia na kugaragara chini udongoni. Baadhi ya ndizi zilikuwa zinaivia juu na kuliwa na komba. Hatua nyingine mbele, mhogo ulioshiba rutuba ya ardhi unachezesha majani yake yaliyoshiba siha ili kuthibitisha jasho na juhudi za mzee mkasi. Mayugwa yaliyoota kwa shime na inda, yakimwagaa majani yake ya makawa makubwa. Mbele zaidi matuta ya viazi vitamu. Tena michungwa, michenxa kangaja, michenza ajemi, milimau, mibirimbi ya kushitukia, midimu, mibalungi, mistaafeli, mitufaa na minazi kitamli ya kutupia hapa na pale. Kitalu kidogo lakini tossha, kilizunguka masikani ya mzee huyu. Mohammed 2013; uk 161.

Vilevile mara kwa mara tunampata mzee huyu akiwa kondeni mwake. Kila wakati Soud anapokuja kumtembelea huwa anampata akiwa shambani mwake. Walipomaliza kula na Time walielekea kondeni mwake kuangalia mimea yake na kule anapata nanasi lilioiva ambao analichukua na kulikata ili wale na Time. Ni dhahiri kuwa mzee huyu ni mtu aliye na bidii licha ya umri wake uliosonga. Vilevile Mkamandume anapomtembelea Mzee huyu, anagundua jinsi ardhi yake ilivyojaa mazao ya aina mbalimbali dhihirisho tosha la bidii ya mzee huyu.

Mzee mwingine aliyechorwa kama mwenye bidii ni Mkamandume ambaye licha ya kutotambuliwa kazini kwa bidii yake anaendelea kufanya kazi kwa sababu ndivyo maumbile

yake. Wafanyakazi wenzake wanaishia kumhusudu kwa kile wanachokiita kimbelembele kwa sababu ya kujituma kazini;

> Lakini Mkamadume hakumenyeka kwa kazi kwa ajili ya pesa, bali kwa sababu yu ya kuwa yeye ni Mkamandume. Ndivyo alivyo kimaumbile. Akiamini kitu, hana mipaka katika kukitekeleza. Kinyume na walivyodhani wengine, alikuwa akiitikia wito wa ndani wa mapenzi ya nchi yake.
>
> Mohammed 2013; uk 28.

Vilevile Mkamandume ni mkulima hodari, alikuwa akiatika mimea ya aina mbalimbali kama vile mihogo na migomba, hata hivyo mambo yanapoanza kumwendea kinyume anaishia kufyeka yote;

> …alikupuka, akatimka mpaka katikati ya kiini cha konde yake bila kujua anafanya nini, aliuingilia mhogo na migomba na kuanza kufyeka.
>
> Uk 23.

**4.7.3 Wazee ni wasamehevu**

Katika riwaya hii, baadhi ya wazee wamechorwa kama watu ambao ni wasamehevu. Wanaweza kuwasamehe maadui wao wa jadi na kuweza kushirikiana nao. Pia wazee hawa wanawasaidia hali inapokuwa ngumu. Mfano wa wazee waliopewa sifa hii ni pamoja na Mzee Mkasi, Bw. Sleyyum pamoja na wazee wa Kijiji ambao walimsamehe Mkamandume licha ya madhila aliyowatendea hapo awali.

Mzee Mkasi kwa mfano aliweza kufungwa korokoroni mara kadha licha ya kutokuwa na hatia. Alifungwa kwa visingizio kuwa anapinga uongozi uliopo, na mwenye kumlimbikizia visingizio hivi si mwingine bali ilikuwa Mkamandume.

> "…na bila ya shaka, babangu, hasimu yako mkubwa alitumiwa kujenga shutuma au tuhuma zote hizo…"
>
> "Aaaa, simlaumu sana babako. Alikuwa masikini hajui anafanya nini. Yeye alitumiliwa tu. Na sasa mtazame yuko wapi. Mtazame sasa wamemfanya nini."
>
> Mkamandume 2013, uk 187.

Kutokana na mazungumzo haya, ni wazi kuwa Mzee Mkasi hana kinyongo na Mkamandume licha ya uovu wote aliotendewa kwa sababu yake. Vilevile Mzee Mkasi siku zote humkaribisha Time na wakawa ni mijadala, kushiriki kazi na pia kula pamoja Jambo ambalo ni muhali kupata ikitokea baina ya maadui au mtu kumfanyia wana wa adui yake.

Wakati wa mapambano na maandamano, tunawapata wazee wote wakija pamoja na kushirikiana licha ya kuwa kulikuwa na tofauti baina yao hapo awali hasa na Mkamandume.

Mkamandume, Viwe na Soud wanapofika kijijini, wanapokelewa vyema na wanakijiji ambao wako tayari kwa mapambano;

> …baadhi walikuja kuwaarifu mabadiliko ya Malelejimema nzima kwamba watu walikuwa wamechoka! Hata miongoni mwa wale waliokuwa na inda na inadi zamani. Wazee wa Kijiji, akiwemo Mzee Mponda, aliyekuwa adui na mgomvi wa kudumu wa Mkamandume walikuja kuwaambia kwamba wamesikia habari njema walizoanzisha na kwamba wao wako tayari.
>
> Uk 478.

Wazee hawa wanadhihirisha hali ya kusameheana licha ya kuwa hawajapata fursa ya kuombana msamaha waziwazi. Hii inaonyesha kuwa wazee ni watu ambao hawana haja ya kuweka chuki bali wako tayari kusameheana na kuungana. Hii vilevile huenda ikawa ni dhihirisho la hekima walio nao wazee hawa.

**4.7.4 Wazee ni wanaharakati/watetezi wa haki**

Wazee wamesawiriwa katika riwaya hii kama watetezi wa haki. Wanaungana na kuongoza mapambano dhidi ya uongozi mbaya na maovu yanayoendelezwa na uongozi uliopo mamlakani. Tunapata viongozi hawa wakitafuta habari na ushauri kuhusu maswala ya kisheria kutoka kwa Soud na hatimaye kuungana wote katika maandamano ya kutetea haki zao. Kulikuwa na njama ya kunyakua ardhi yao bila wao kuhusishwa katika maamuzi hayo.

> …ulizuka uvumi pale kijijinia kwamba ardhi kubwa karibu na ufukwe wa Bahari imeshapangwa kuuziwa wageni kwa madhumuni ya kujenga hoteli.
>
> "Hii ni ardhi nzuri kabisa kwa kilimo na mifugo ya wananchi. Hatuna pahala pengine pa kutosha pa kulima chakula chetu na kufugia ng'ombe wetu. Na huu ni mwanzo tu, kesho tutakuja ambiwa tuvunje nyumba zetu tuwapishe wageni wengine wajenge kambi yao ya kijeshi!" Walisema wazee wa Kijiji, "Ikiuzwa ardhi hii kujengwa hoteli sisi tutaishi wapi na vipi? Haiwezekani, hatukubali…." Walisema wazee huku wakimtaka shauri Soud.
>
> Uk 479.

Kutokana na mazungumzo haya, inadhihirika wazi kuwa wazee hawa hawako tayari kuwapa nafasi viongozi wao kuwanyanyasa na ndio maana wanatafuta ushauri kwa Soud. Ushauri wanaopata ni kuwa wanafaa kupanga na kushiriki maandamano ili kutetea haki zao. Nao kwa pamoja wanakubali ina kushirikiana katika harakati hizi

Bwana Sleyyum ni mmoja wa wazee waliojitolea kufadhili maandamano hayo;

> Magari yalikuwa yakienda na kurudi kwa wingi. Magari yaliyojitolea Kwenda kusomba watu mashmba na vijijini kuja kuwamimina mjini kwenye maandamano. Bwana Sleyyum ambaye siku hizi ameondosha woga kabisakabisa (na kweli Hapana anayeogopa tena) alitayarisha matangi kwa matangi ya sharubati na

> kuyaweka njiani huru kwa watu waliokuwa na kiu kunywa walivyopenda kwani siku hii jua lilikuwa likiwaka si mchezo. Pia, Bwana Sleyyum, alitoa mabasi yake Matano Kwenda kuwachukua watu wa ngoma kadha wa kadha za ki-Malelejimema kuja kuhamasisha watu na kutia shamrashamra maandamanoni. Uk 484.

Bwana Sleyyum kando na kujitolea kufadhili huo, mwenyewe alijiunga na wazee wengine katika kushiriki maandamano;

> …yalipofika maandamano alijitia kundini (Mkamandume), akaungana na jamaa mstari wa mbele kabisa. Pale alikuwapo Soud, Time, Mzee Mponda, Mtumwa, Msimu, Viwe, Mzee Mkasi, Bwana Sleyyum na wakuu wa Kijiji cha Msera. Wote walikuwa wamekamatana mikono wakimwaga hamasa zao kwa furaha na bila ya woga wowote.
>
> Mohammed 2013; uk 485.

Mkamandume kando na kujiunga na wazee wenzake katika maandamano, alikuwa na juhudi zake mwenyewe ambazo zilikuwa na lengo la kupigana na madhila licha ya kuwa baadhi ya mbinu alizotumia hazikuwa za kisheria. Kwa mfano alijiunga na kina Soud na Viwe katika maonyesho ya tamthilia na hatimaye aliporudi kijijini alijiunga nao kuhamasisha wanakijiji ambao tayari walikuwa wameanza kuchoka na mkondo wa mambo na wimbi la mabadiliko kuanza kuvuma. Mkamandume alichukua sheria mikononi mwake kwa kuwaangamiza mahasimu wake ambao ni Bwana Shombo pamoja na Mtemi.

> …alichomoza kidogo yule mti alipokuwa akikaribia kuhakikisha kuwa ndiye adui yake na alipohakikisha hivyo alingojea. Sasa Bwana Shombo alikuwa karibu na pale aliposimama Mkamandume. Kama fumba macho na kufumbua, Mkamandume aliruka kwa nguvu za ajabu na kwa Dhoruba moja la panga alimkata kichwa Bwana shombo. Bwana shombo hakuwahi hata kutoa ukwenzi wa maumivu au kutetea roho yake.
>
> Uk 482.

Mkamandume vilevile alimvizia Bosi wake alipokuwa akiingia kazini na kumwangamiza kwa kumkata shingo kama alivyomfania Bw. Shombo;

> Bosi alipokwisha fika hapo, alizima moto gari na kufungua mlango na kutoka garini na brief-case yake mkononi. Alitia loki gari na kugeuka kuelekea jengo la ofisini. Wakati huo ndipo Mkamandume alipochopoka. Alitimka mbio kutoka mle nyuma shina, akaruka na kumfyeka Mtemi shingoni. Hakukuwa na ghasia zozote. Alilitupa panga lake hapohapo na taratibu, akaelekea upande unaokuja maandamano. Hakuna yeyote aliyeona tukio lile.
>
> Mohammed 2013; uk 485-486.

Mkamandume aliwaangamiza watu hawa wawili akiwa na imani kuwa anatetea haki. Na ndio maana baada ya kuwaangamiza wote wawili anaenda kujiunga na maandamano na kujitia

mstari wa mbele licha ya kuambiwa arudi nyuma ndio asionekane kwa kuwa alikuwa akisakwa na polisi. Ni wazi kuwa mzee huyu amejitolea mhanga kupigania taifa lake kwa vyovyote vile.

### 4.7.5 Wazee ni wenye mapenzi ya dhati

Wazee katika riwaya hii vilevile wamechorwa kama watu walio na mapenzi tele hasa kwa wajukuu wao na pia wanao walio wachanga. Mkamandume anadhihirisha sifa hii katika sehemu mbalimbali. Ni wazi kuwa kuwa Mkamandume anampenda mwanawe mdogo aitwaye Katija. Anapoondoka usiku, Katija anamwona na kumuuliza aendako. Mkamandume anamjibu na kisha kumsogelea na kumvuta na kumkumbatia na kumbusu kipajini. Vilevile Matendo haya yanadhihirisha upendo alio nao kwa mwanawe. Mkamandume anampenda Time sana licha ya kuwa hataki kumuonyesha wazi. Tunaelezwa kuwa;

> …kwa dhahiri mpaka hivi karibuni Mkamandume amemwonyesha Time kwamba hampendi kwa kile yeye Mkamandume alichokiita "vituko vyake", lakini moyoni mwa Mkamandume Time alikuwa kajaa tele kwa pumzi za mapenzi.
>
> Uk 41.

Anapofika jijini na kukutana na Soud na Viwe pamoja na mwanawe Viwe, Mkamandume, Mkamandume mzee anaonekana kumpenda sana Mkamandume mdogo. Hii inadhihirika na mahusiano yao ya karibu na anapokaa naye kutizama tamthilia ya kina Soud.

> …kundini mwa hadhira Mkamandume kila siku aliketi pamoja na kijukuu chake, somo yake Mkamandume. Sasa kimevuta umri, zaidi ya miaka mitano tokea kuzaliwa. Katika kukaa nacho, hakukiachia kitazame mawengemawenge tu tamthilia zile, bali alikiongoza na kukielimisha jinsi tamthilia zinavyokwenda kwa maana na taathira zake mbele yao.
>
> Uk 474.

Mkamandume anadhihirisha mapenzi yake kwa kijukuu huyu licha ya kuwa mwanzoni hakufurahia mimba ya mwanawe Viwe na akaishia kumuadhibu jambo lililopekea Viwe kutoroka nyumbani.

Mzee mwingine anayedhihirisha mapenzi ya dhati ni Mzee Mkasi. Mzee huyu anawapenda watoto sana. Hii inadhihirika kutokana na uhusiano baina yake na Soud na Time. Time na Soud wamekuwa wakija kwa Mzee Mkasi tangu wakiwa wadogo na kufurahia kuwa naye nyakati zote. Hii inadhihirisha kuwa Mzee Mkasi alikuwa anawapenda watoto hawa licha ya kuwa babake Time alikuwa hasidi wake.

> …hakukuwa na mtu mzima aliyewahamu Time na Soud wakati ule na hata sasa. Hata baba na mama zao walishindwa kuwapa wao mapenzi, uhuru, amanii ina utulivu kama walioupata kwake (Mzee Mkasi).

Mount Kenya University

Mohammed 2013, 188.

### 4.7.6 Wazee ni washauri

Wazee katika *Mkamandume (2013)*Mkamandume (2013) wamechorwa kama washauri. Kutokana na hekima na heshima ambayo wazee wametunukiwa na jamii, mara nyingi tunawapata wakitoa ushauri kwa wale wenye umri mdogo na walio katika hali ngumu au hali mbalimbali. Baadhi ya wahusika wazee wanaotoa ushauri ni pamoja na Mzee Mkasi, Bwana Sleyyum pamoja na Bi. Reja.

Bi. Reja ni mwanamke ambaye amechorwa kama mshauri hasa kwa masuala ya uzazi na kifamilia ndio maana mkewe Mkamandume, Bi. Tufaa anapokuwa na tatizo kmhusu bintiye Viwe anamkimbilia akiwa na tumaini la kupata jawabu au angalau kupata usaidizi japo kidogo. Bi. Reja anampa ushauri kuhusu kile ambacho watafanya. Jambo hili si nzuri, ila Tufaa anaona ni afadhali kuliko madhila ambayo atapata kutoka kwa mumewe. Na hivyo wanaridhia kufanya njama ya kuavya mimba ile ya Viwe kwa kisingizio cha Viwe kufanyiwa unyago. Hata hivyo anamshauri asisherehekee mapema dhihirisho tosha la mtu anayeelewa mambo mengi.

> "….sijui nikwambie nini Bi. Somo." Alitoa shukrani.
>
> "Huna haja ya kunambia kitu, ngoja kwanza tuvuke huu mkondo ndipo tuseme *alhamdhulalah Rabi l-alamin."*
>
> Uk 103.

Bwana Sleyyum kwa upande wake anatoa ushauri kwa Soud kuhusu suala la ndoa. Mzee huyu aliwachiwa jukumu hilo na wazee wake Soud kabla ya kuaga dunia. Hivyo, anapoona muda umesomga na anamuona Soud hajaridhia kuoa, anamwalika kwake ili akamsaili kuhusu jambo hili. Hata hivyo Soud anamweleza kuwa hajataka kuoa kwa kuchelea gharama ya ndoa na hivyo alihiari kungoja kupata ajira. Hata hivyo baada ya mazungumzo, Bw. Sleyyum anamweleza Soud haya;

> "Soud Mwanangu," Bwan Sleyyum alikuja kwa matao ya chini ili kumbembeleza, "dunia yetu mbaya hii. Na akina sisi tunakamiwa. Watu wanataka kulipa visasa pasi na kikomo. Wanataka kulipa visasi kwa mambo ambayo sisi hatuyajui. Tunayasikia kama wanavyosikia wao - kama yalikuwepo kwa namna yanavyoelezewa. Likiisha hili linakuja hili. Kila siku nakama mpya. Wenye kani, moyo, nguvu na uwezo wanakimbia na sisi tuliobakii lazima tutafute njia ya kuhifadhiana."
>
> Uk 267.

Mount Kenya University

Ushauri huu alipewa Soud kwa kuwa Bwan Sleyyum bila shaka alijua huenda Soud ana uhusiano mwingine kando na ile aliyomtakia ambayo ni kumuoa bintiye Rafiqa. Jambo hili walikuwa wameshapanga na wazazi wake Soud kabla ya wao kuaga dunia.

Mzee mkasi anadhihirika kuwa mshauri katika miktadha mbalimbali. Kama ilivyo ada, mtu anapokuwa na tatizo zito, hukimbilia yule anayeamini kuwa anaweza kumtatulia shida yake. Time anapokuwa na tatizo na Mawazo kuhusu hali yake hasa uhusiano baina yake na Soud ambayo yaonekana haitaishia kwenye ndoa, Time anajawa na Mawazo tele. Anapojaribu kuangalia dunia yake hamwoni yeyote ambaye anaweza kumkimbilia hadi pale anapomkumbuka Mzee Mkasi kuwa ndiye mtu ambaye amebakia pekee katika dunia yake.

> Katika kutapatapa lakini, katika kutia na kutoa, alimkumbuka Mzee Mkasi. Alikuwa mtu pekee aliyebaki katika dunia ya Time ya kuhiniwa. Mzee Mkasi ndiyo punje ya tamaa iliyobaki, kwa hivyo lazima aipatilize. Watu husema: mtu, mtumie mtu, kwani kila mtu na mtuwe. Mzee Mkasi mtuwe ni Soud. Watu wanaokubaliana kwa vile Soud huchota maarifa kwa mzee huyo na mzee huyo aligida elimu ya kisasa kwa kijana wake.
>
> Uk 160.

Ni dhahiri kuwa Time anaenda kwa Mzee Mkasi akitafuta ushauri kwa kile ambacho atafanya kuhusiana na hali yake ile. Anaamini kuwa huenda Mzee Mkasi akamsaidia kufanya maamuzi mazuri na vilevile anaweza akamsaidia kumshawishi Soud.

**4.7.7 Wazee ni wenye dharau**

Dharau kulingana na Kamusi Teule ya Kiswahili (2013), ni tabia ya kutoheshimu ama kukosa kudhamini mtu au kitu. Mkamandume ni mzee mmoja ambaye anaonyehsa tabia hii. Anamdharau Mzee Mkasi kiasi cha kumwekelea makosa ambayo hajafanya ila ni kwa sababu hamthamini tu.

> Mbali na uhasama uliopo baina yao, kati ya watu Mkamandume aliowadharau, Mzee Mkasi alikuwa mwanzo kabisa.
>
> Uk 375.

Mkamandume alimdharau Mzee Mkasi kiasi cha kumpachika majina ya kumdhalilisha kama kumwita mlamakombo, mramba-nyayo-za-mwabwana zake.

> Asili ya yote hayo, ni kile alichokiita yeye Mkamandume, ubaradhuli wa Mzee Mkasi wa kukataa kushirikiana na Waafrika wenzake kutetea nchi yao na kuungana na wale aliowaita wageni wakati ule. Wakati ule alimwita Mzee Mkasi mlamakombo, mramba-nyayo-za-mwabwana-zake! Mzee Mkasi aliposalimika kwa miujiza katika vita vya mageuzo, Mkamandume aliona kwamba anastahili adhabu kubwa inayofanana na kifo. Ndiyo akamtilisha ndani kwa njama tu.



Mount Kenya University

Uk 375.

Ni kwa sababu ya kutomthamini Mzee Mkasi ndipo Mkamandume anamfanyia maovu haya yote na kumpangia njama hizi. Anamwona kama mtu asiyestahili kupewa nafasi katika maisha au kupata vitu vya dhamani katika maisha yake. hata hivyo Mzee Mkasi hakulipiza kisasi bali alimpokea mwanawe Mkamandume na kukaa naye.

**4.7.8 Wahusika wazee ni wahafidhina**

Wazee wamechorwa kama watu wanaoshikilia mila, tamaduni na desturi katika jamii mbalimbali. Hawa ndio kiungo muhimu cha kurithisha utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Katika *Mkamandume (2013)*Mkamandume (2013) wazee ambao wamepewa sifa hii kama vile Bi. Reja. Tufaa anapomwendea akitaka usaidizi, Bi. Reja anamweleza kuwa suluhu ni kuavya ile mimba ila njia watakayotumia kumtorosha Viwe inawapa changamoto. Utamaduni wa kale wa wasichana kufanyiwa unyago unakuwa njia au kisingizio kizuri cha kumtorosha Viwe. Anayedokeza jambo hili bila shaka anaonyesha kuwa ni mtu anayethamini mila hii ingawa imepitwa na wakati, ambaye ni Bi. Reja katika kisa hiki. Anasema;

> "…lazima tutayarishe unyago wa kuvinwa mwari- si bado hajavinwa Viwe?"
>
> Mohammed 2013; uk 103.

Kando na kuamini unyago, Bi. Reja anadhihirisha imani yake pia katika matumizi ya dawa za kienyeji licha ya kuwepo kwa maendeleo ya kisayansi ambayo yamefaulisha uwepo wa dawa za kisasa. Bi. Reja anamwambia Tufaa;

> "…Basi Viwe tutamchukua kwa kisingizio cha kumchezea unyago, lakini lengo letu ni kumtoa mimba kwa madawa ya kienyeji, na fundi wa hayo n'naye hapa mkononi." Bi. Reja alionyesha kidole chake shada kiganjani pake.
>
> Uk 103.

Bwan. Sleyyum anaonekana kushikilia pia utamaduni wa kale hasa ule wa wazazi kuwachagulia wanao wachumba. Mzee huyu alikuwa ashakubaliana na wazazi wake Soud kuwa atamuoa Rafiqa bintiye Bwan Sleyyum. Soud anapofikisha umri wa kuoa na Bwan Sleyyum kuona kuwa hajamposa msichana, anaamua kumwita kumkumbusha ahadi waliyokeana wazazi hao na kutaka yeye kumposa Rafiqa ila Soud anakataa rai hiyo.

> "Tulieka ahadi mimi na marehemu baba'ako ba Bi. Mwana na mama'ako, kwamba kwa madhumuni ya kuimarisha urafiki na undugu wetu, bora tungechanganyisha damu kabisa. Njia ya kuchanganya damu ilikuwa wewe kumwoa Rafiwa. Kwetu sisi hakukuwa na Fahari kubwa kuliko hiyo na wazee wako wasingetaka jambo jingine kubwa kuliko hili. Tumeishi siku tulizoishi na

kulitaja jambo hili waziwazi ili mlitambue. Na nadhani mmelitambua na kwa hiyo rai hii si ngeni kwa wewe na Rafiqa.

Uk 268.

### 4.7.9 Wahusika wazee ni katili

Wahusika wazee katika *Mkamandume (2013)*) (Mohammed 2013), wamepewa sifa hii ya kutokauwa na utu wala huruma. Baadhi ya wazee katika riwaya wanaodhihirisha sifa hii ni Mkamandume. Mhusika huyu anapogundua mwanawe ni mjamzito, anamtandika vibaya sana na kumshika shingo tayari kumwangamiza. Na sio Viwe pekee anayepokea kichapo hicho bali pia Time na Tufaa wanapojaribu kumwokoa Viwe kutoka kwa mikono ya Mkamandume;

> …alimvuta Time akamzaba kibao kikalo. Huyo Time akaanguka chini. Kisha akamkamata Viwe na kumtupa chini. Akamwinamia kumkaba shingo. Tufaa alipoona hivyo ubozi ulimtoka. Ukelele ulamtoka Tufaa. "Mtumee…unaua Bwana Mkamandume…unauaaa…."
>
> Mkamandume hakusema kitu. Sasa aliwahujumu maadui zake kama vile walikuwa si watu tena kwake. Kila alipovutwa na Time na Tufaa aliwapiga vibaya sana na kisha kurejea kumkaba roho Viwe.
>
> Mohammed 2013; uk 112

Ilibidi Tufaa na Time kupiga kelele kwa pamoja kuwaita majirani ili waje wawasaidie. Na hata walipofika, ilikuwa vigumu kumpapatua Mkamandume na bintiye tayari alikuwa ashaanza kutokwa na kipovu, ilibidi wanaume sita wenye nguvu waweze kusaidiana ndipo walipofaulu. Hii inadhihirisha kuwa Mkamandume alikuwa tayari kumuangamiza bintiye kwa kosa la kupata mimba na pia kuwahasiri jamaa zake bila huruma.

Mkamandume pia anadhihirisha ukatili wake anapomwangamiza Bwana Shombo kwa kumkata shingo akitoka msikitini kusali;

> Sasa Bwana Shombo alikuwa karibu na pale aliposimama Mkamandume. Kama fumba macho na kufumbua, Mkamandume aliruka kwa nguvu za ajabu na kwa Dhoruba moja la panga alimkata kichwa Bwana shombo.
>
> Mohammed 2013 uk 482.

Vilevile Mkamandume anamwangamiza Bosi wake kwa njia ileile ya kumkata shingo wakati wa maandamano;

> Bosi alipokwisha fika hapo, alizima moto gari na kufungua mlango na kutoka garini na brief-case yake mkononi. Alitia loki gari na kugeuka kuelekea jengo la ofisini. Wakati huo ndipo Mkamandume alipochopoka. Alitimka mbio kutoka mle nyuma shina, akaruka na kumfyeka Mtemi shingoni. Hakukuwa na ghasia zozote.

Uk 485-486.

### 4.7.10 Wahusika wazee ni wapelelezi

Wahusika wazee katika riwaya hii wamechorwa kuwa ni wapelelezi au wajasusi. Mpelelezi ni mtu anayeweza kuchunguza jambo fulani na kupata habari zote kuhusu tukio au tabia na mienendo ya mtu fulani bila kujulikana. Katika riwaya hii, Mkamandume amepewa sifa hii. Anawachunguza Bwana Shombo na Bosi na kupata kujua tabia na mienendo yao ndipo anappopanga njama ya kuwashambulia bila yeyote kujua au kushuku lolote;

> Hatimaye alifika pahala alipotaka kufika. Palikuwa pahala panapo kichaka kilichokusanya giza. Hapo alisimama chini ya Mlangimlangi na kusubiri. Alijua atapita hapo hasimu yake atakapokuwa akirudi msikitini kusali sala ya isha.
>
> Mohammed 2013 uk 482.

Vilevile Mkamandume alikuwa amemchunguza Mtemi hadi akajua wakati anapofika na jinsi anavyofika pale, akajua kuwa anakuja pekee bila dereva wala mlinzi wake;

> …. Mkamandume bila wasiwasi wa aliyoyafanya usiku jana alisimama mbali kidogo na pale *boss* anapoegesha gari lake. Lakini alipoliona gari lenyewe linakuja, mbio alifika pale chini panapo egesho la magari. Palikuwa na mti mkubwa uliotanda matawi yake mpaka chini na wenye shina nene. Nyuma ya shina hili nene lililofunikwa na matawi ndipo alipokwenda kujificha Mkamandume. Alijua kwamba dereva wa gari ni mwenyewe *boss,* kwani gari hulala nayo nyumbani na kuja nayo kazini asubuhi ambapo ndiyo tena dereva wake huichukua na kumwendesha kutwa nzima. Alikwisha peleleza hayo yote, hasa kwa vile *boss* amekuwa mtu mkubwa zaidi. Kanuni zake za itifaki zimebadilika kulingana na zile alizozijua Mkamandume alipokuwa akifanya naye ofisi moja.
>
> Uk 485.

Mkamandume bila shaka alijua uzito na ugumu wa kutekeleza kile alichokuwa amepanga na hivyo ilimbidi afanye upelelezi wake kwa makini ili kuweza kufaulu. Na jinsi anavyotekeleza mauaji hayo inadhihirisha kuwa Mkamandume alikuwa amechunguza kila hatua ya mahasimu wake.

### 4.7.11 Wazee ni walevi na wapyoro

Katika kila jamii hapakosi wazee wanaojiingiza katika ulevi na baada ya kulewa au wanapotoka ulevini, jambo lilanalofanyika mara nyingi usiku wa manane au mapema alfajiri, wanatembea wakipaza sauti na kuimba, kuwasalimu na kuwasifia marafiki zao na vilevile kuwakejeli mahasimu na maadui. Wanapowakejeli maadui, si ajabu kuwasikia wakitumia luhga yenye matusi au isiyo na heshima wala tasfida. Katika riwaya hii, Mzee Mponda amechorwa kwa njia inayoafiki maelezo haya. Tunaambiwa kuwa;

Mount Kenya University

> Time hakupata usingizi kamwe usiku ule. Na lini amepata usingizi? Jogoo la kwanza lilipowika alijua alfajiri inaanza kuingia. Mzee Mponda alipopita upenuni pao na ulevi kichwa tele, na nyimbo na matusi kama kawaida. Time alihakikisha kwamba alfajiri inaelekea mapambazukoni.
>
> Uk 85.

Ni hali ambayo Mzee huyu amezoea na ndio maana Time ashajua wakati wa mzee huyu kupita hapo kwao. Matusi na kejeli zake mara nyingi huelekeza kwa Mkamandume ambaye ni adui yake tangu zama.

> Alisita hapo, akafyonza, "Zamani", aliendelea sasa makusudi anapasa sauti yake juu, "zamani, tuligaragra vumbini na sasa twagaragara topeni – tofauti iko wapi? Si yaleyale tu. Tofauti ya ukame na umajimaji. Na…na sasa si wapo wanaolalia vitanda vya dhahabu kama walivyolalia wale tuliowatimua? Tofauti nini? Zamani si tulikuwa punda na Mikia yetu. Siku hizi sisi ni punda kasoro mkoa. Na ikifika siku ya kujikomboa tunaota tena na kuifyata! Ha-ha-ha…ha-ha-ha…ha- ha- haaa," alicheka kicheko cha stihizai kilichopasua makiwa ya usiku mpevu.
>
> Uk 86.

**4.7.12 Wazee ni wacheshi**

Wazee katika riwaya hii wamepewa uwezo wa kuchekesha kwa mizaha ya aina mbalimbali. Wazee wanapokuwa na vijana huwa wanapenda kutaniana hali ambayo huleta vicheko. Mzee Mkasi anadhihirisha sifa hii hasa wanapokuwa na Time. Time anapomtembelea Mzee Mkasi, mazungumzo yao yanaanza kwa kutaniana kama ifuatavyo;

> "Oooo bibiye," alianza kutania, "yoyoyo bibe amefika yoyoyo … karibu."
>
> Nimeshakaribia bwana," Time alirejesha mzaha. Tabia ya Waswahili, babu kumtania mjukuu wake kwa mzaha wa mume na mke – ingwa mzee huyu si babu yake Time mzaa baba au mama.
>
> "Karibu uketi… chukua kibao hicho hapo upenuni."
>
> "La, sitakaa nikakutazama wewe ukifanya kazi – leo zamu yako kukupikia… nimekuja makusudi, maana sitaki ulie wivu".
>
> Wivu n'talia tu, maana hapa hupiti mpaka upotee njia".
>
> Kimya. Wakawa wanatazamana na kuchekeana.
>
> "Mchi uko wapi?"
>
> "Mchi wa nini?"
>
> "Nikusaidie naona kutwanga mhogo…"
>
> "Wacha tu. Hulioni joto na jua hilo? Nitakutoa jasho b're Bi. Mrembo"
>
> Mohammed 2013 uk 161-162.

Mazungumzo yanabainisha ucheshi uliopo katika maneno ya Mzee Mkasi. Mzee huyu anadhihirisha tena tabia yake hii wakati Time anapotaka kumuuliza swali;

> "Samahani Mzee Mkasi…" Time alionekana ana nia ya kumwuliza Mzee Mkasi suala gumu …suala la muhali, "nikuulize kidogo."
>
> "Niulize sana".
>
> Mohammed 2013; uk 177

Licha ya kuwa mzee huyu ameng'amua Time ana jambo zito la kuuliza, anamjibu kwa mzaha. Hii inadhihirisha ukuruba walio nao wawili hao.

### 4.7.13 Wazee wametamauka

Kutamauka ni hali ya mtu kukata tamaa maishani au kukosa imani ya kufanikiwa katika jambo fulani. Baadhi ya wazee wanapoona umri wao umesonga sana, huhisi kuwa hawana uwezo wa kutekeleza jambo lolote na kufaulu maishani. Halli hii huletwa na ile hali kuwa mzee anaona nguvu zake zinaelekea kuisha na pia wakati wake wa kuwa hai umepungua na hivyo kuona kuwa hakuna tumaini tena. Mhusika aliyejipata katika hali ya kukata tamaa ni Mkamandume. Baada ya bidii yake ya muda mrefu na kushiriki katika vita vya kukomboa taifa lao kutoka kwa wakoloni pamoja na vita vya baada ya uhuru, Mkamandume hakupata afueni yoyote licha ya kuwa alikuwa mtu wa karibu na Bosi. Mkamandume anajipata kiwa hoi, hana nguvu tena za kufanya ukulima, pesa alizotarajia upata hakuzipata hali inayomletea msongo wa mawazo. Ananpoenda kwa Mzee Mkasi, tunampata Mkamandume akiwa na Mawazo haya yanayoashiria kuwa kakata tamaa;

> "Kumbuka kila kitu kilicho na kinachoathiri maisha yako ni muhimu kwa sababu ni njia pekee ya kujitambua na kuanza upya kama alivyoanza Mzee Mkasi".
>
> Kuanza upya katika hali hii niliyonayo? A-a, mimi nimekwisha. Nimechelewa kutambua. Nimechelewa kujua. Na anayechelewa kachelewa! Hasa aki'sha kama nilivyokwisha mimi. Kisu kimeingia mpaka mifupani. Mimi sikutambua mapema lakini Mzee Mkasi si kama alitambua mapema tu, alitambua zamani pia. Hii ndiyo tofauti yetu. Maisha ni kutambua …maisha ni kujua mapema. Ni kuelewa tokea zamani …
>
> Uk 377.

Maelezo haya yanadhihirsha wazi mtu ambaye amekata tamaa. Zaidi ya haya, Mkamandume anapofika kondeni mwake na kuona jinsi mazao yake yameathiriwa na ugonjwa fulani ambao haueleweki, anachukua 'mndu' wake na kufyeka kila kitu mle shambani. Hii ni ishara tosha kuwa mzee huyu alikwisha kutamauka na haoni tumaini lolote katika mazao hayo wala maisha yake.

Mount Kenya University

### 4.8 Maudhui yanayoibuliwa na kuendelezwa kupitia kwa wahusika wazee

Maudhui hurejelea jumla ya mawazo au mada zinazowasilishwa katika kazi ya fasihi. Mada hizi huibuliwa kupitia kwa mazungumzo, tabia pamoja na matendo ya wahusika. Nadharia ya uhalisia inashikilia kwamba, matukio ya kazi ya kifasihi ni sharti yawiane na matukio katika ulimwengu halisi. Hivyo maudhui yanayaoibuliwa katika kazi ya fasihi ya kihalisia hushabihiana na hali halisi iliyomo katika jamii husika. Waandishi huchagua wahusika kwa njia ya kibunifu na makusudi ili kuhakikisha kuwa ujumbe wao umefika kama alivyokusudia. Na ili kuhakikisha kuwa ujumbe umewafikia hadhira mahsusi, huwatumia wahusika wanaolandana na walengwa wake. Katika sehemu hii, maudhui yaliyowasilishwa kupitia kwa wahusika wazee katika riwaya zote mbili zitaangaziwa kwa kina.

### 4.8.0 Maudhui katika Riwaya ya *Tumaini (2006)*

Katika riwaya ya *Tumaini (2006)*, mwandishi alilenga kumtetea mtoto wa kike kutokana na madhila anayofanyiwa na jamii kama vile kunyimwa elimu, kuozwa mapema, kupashwa tohara miongoni mwa mengine anayopitia. Katika kupitisha ujumbe wake huu, mwandishi aliweza kuibua maudhui mbalimbali kupitia kwa wahusika wazee. Utafiti huu ulibaini maudhui kama vile, ukeketaji, ndoa za mapema, elimu, ukatili, ndoa, ulezi, uongozi mbaya, bidii, urafiki na tamaduni.

### 4.8.1 Maudhui ya ukeketaji

Ukeketaji hurejelea hali ambapo mtoto wa kike hupitishwa kwenye jando au tohara kama hatua mojawapo ya kuweza kuvukishwa kutoka utoto au utu uzima. Baada ya kufanyiwa unyago, tendo na tamaduni iliyoshikiliwa na jamii nyingi za kiafrika na ambayo ilifanywa punde tu mtoto msichana anapofikia umri wa kubaleghe. Utamaduni huu umeshikiliwa na kuendelezwa na wazee katika riwaya ya Tumaini wakiongozwa na Babake Tumaini, Mzee Masumbuko. Mzee huyu anapanga njama ya Tumaini kupashwa tohara, ila Tumaini anabaini mpango huu ambao haupendelei na hivyo anaishia kutoroka kwao na kwenda kuishi kwa mjombake.

> Tumaini alikuwa amekamilisha darasa la saba katika shule ya msingi ya Kivulini, kijijini Mabuyuni. Hata hivyo hakuwa na matumaini ya kuyabadilisha Mawazo ya babake kuhusu kuendelea na masomo ya darasa la nane. Matumaini yake yalizidi kufifia babake alipoanza kufanya mipango ya kumpasha tohara.
>
> Momanyi 2006, uk 14

Licha ya kutoroka kwa Tumaini, mzee huyu hakufa moyo, aliendelea na mpango wake huo ila hakufua dafu.

Mzee Masumbuko anafaulu kuwashawishi wadogo wake Tumaini ambao ni pacha; Rehema na Mashaka kupashwa tohara. Hao wawili waliridhia haja ya baba yao ya kupashwa, tunampata kujua haya kutoka kwa Idi anapotumwa kuwaalika wajomba zake;

> "Mama, una ujumbe hapa,", Riziki alimwita mamake aliyekuwa akishughullika mle nyumbani. Bi. Halima alitoka nhe ana alipomwona Idi, alimsalimia kwa furaha na kumwuliza, "Haya bwana mdogo, leo una yapi kutoka nyumbani?"
>
> "Nimetumwa niwaambie wewe na Ba Mdogo mfike nyumbani Jumamosi – mimi na akina Mashaka tunapashwa tohara", Idi alisema huku haya zimemchachia.
>
> "Salaala! Alitamka Bi. Halima, "Mzee Masumbuko hajapata funzo baada ya tafrano za Tumaini? Ataka kuwatahiri pacha wale awaoze! Naona Masumbuko mambo yatatumbukia nyongo mwaka huu."
>
> "Lakini Ma Mdogo, akina Rehema wanayataka wenyewe. Hata mama alipinga lakini wao wamesema lazima watahiriwe," Idi alidakia.
>
> Momanyi 2006, uk 78

Mzee Masumbuko anashikilia mila hii licha ya kuwepo kwa wimbi la mabadiliko ambalo linavuma na ambalo limewababeb wazee wenzake ambao tayari wamebadilika na kujaribu kumshawishi Mzee Msumbuko ila hawajafanikiwa;

> "Kweli kabisa. Wahenga walinena, hakuna mchele usiokuwa na ndume. Mzee Masumbuko anajaribu kupigana na upepo wa mabadiliko. Haelewi kwamba kufanya hivyo ni sawa na kupiga ngumi ukuta? Vyombo vya habari vinatangaza usiku na mchana kwamba ukeketaji wa wasichana ni marufuku kufanywa siku hizi. Nikijaribu kumweleza mzee huyu ananitilia huku akinitolea kule. Wazee wenzake wamekwisha kumketisha na kumsihi afuate uamuzi wa wazazi wenzake kupiga marufuku mila hii, lakini nasaha zao hazijafua dafu. Hata hivyo, upepo wa wakati utampeperusha kama jani kavu, akajuta laity iangalibadilisha msimamo wake."
>
> Momanyi 2006, uk 24

Ni dhahiri kuwa Mzee masumbuko anashikilia imani hii ya wasichana kukeketwa licha ya kuwa na athari nyingi kwa mtoto wa kike na pingamizi zilizopo kuhusu mila hii. Rehema na Mashaka wanapashwa tohara na hatimaye kuozwa baada ya masomo ya shule ya msingi licha ya kuwa na umri mdogo.

Utafiti huu ulibaini kuwa, mwandishi wa riwaya hii alikuwa amepania kudhihirisha baadhi ya madhara ya ukeketaji kwa mtoto msichana ambazo ni pamoja; kunyimwa elimu au kukatishiwa masomo, kuozwa mapema na kwa lazima, matatizo ya uzazi, tofauti za kiakili kutokana na tofauti ya umri, kugombezwa na matatizo ya uke wenza. Haya yanadhihirika kupitia wahusika kama vile Mashaka na Rehema wana wa Mzee Masumbuko ambao wanalazimika kukatisha

masomo na kuozwa. Mashaka anaozwa kwa Mzee Lusimbo, mzee aliye na umri mkubwa kama wa babake;

> Aghalabu, Tumaini aliwaza juu ya dada zake, jinsi walivyokosa elimu kwa sababu ya tamaa ya baba yake. Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka, na akamwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo, kama mke wa tatu. Ndoa hiyo ilimsababishia Mashaka madhara makubwa ya kimwili na kiakili pia. Mzee huyo alikuwa na umri mkubwa sawa na wa babake Mashaka. Kwa hivyo wakawa hasikilizani kabisa. Yale yaliyomfurahisha Mashaka, mumewe aliyaona ni ya kitoto tu. Hakuacha kumsononesha kimawazo hasa pale alipomsuta kwa kosa lolote dogo alilofanya. Hakuwa kufu yake. Waaidha, Mashaka alipata taabu ya uzazi kutokana umri wake mdogo. Alizaa watoto watatu, wote kwa njia ya upasuaji kwa sababu ya matatizo ya uzazi.
>
> Momanyi 2006, uk 122- 123.

Rehema naye aliozwa kwa Shauri. Huyu alipata matatizo wakati wa kujifungua mwanawe wa kwanza aliyejulikana kama Sinangoa.

> …haukupita muda mrefu kabla ya daktari mkuu kumjia Tumaini pale alipokuwa akimsubiri dadake, na kumwarifu kuwa ingawa Rehema alikumbwa na matatizo hatari ya uzazi, alijifungua mtoto wa kike salama.
>
> Momanyi 2006, uk 126.

Hivyo basi kupitia kwa wahusika wazee mwandishi huyu ameweza kudhihirisha madhara ya ukeketaji kwa mtoto wa kike kama yalivyotajawa hapo juu. Vilevile ni dhihirisho kuwa kuna mila hii potovu ipo na inaendelezwa na wazee wachache ambao hawako tayari kubadilika.

### 4.8.2 Ndoa za mapema

Utafiti huu ulibaini kuwa ndoa za mapema ni mojawapo ya maswala yaliyozungumziwa na mwandishi na ujumbe huu kupitishwa kwa wahusika wazee. Wazee ndio wanaendeleza mila hii ya kuwaoza wasichana wakiwa wachanga na vilevile wengi wa wasichana hawa wanaolewa na wazee katika jamii. Katika riwaya hii, baadhi ya wahusika walioendeleza maudhui haya ni pamoja na Mzee Masumbuko, Mzee Lusimbo pamoja na Mzee Chumo. Mzee Msumbuko alichorwa kama Mzee ambaye hajali masomo ya mtoto wa kike na anamwona kama kitega uchumi kutokana na mahari ambayo atamletea. Hivyo anaona kumsomesha mtoto wa kike ni kupoteza pesa na wakati bure. Haya yanadhihirka kutokana na mazungumzo ya Idi ambaye anaiga maneno na tabia ya babake;

> …Tumaini alimwangalia kakake kwa muda huku akitikisa kichwa kwa masikitiko. Alielewa kuwa tabia ya Idi ni kielelezo halisi cha malezi ya babake. Kijana huyo mdoogo tayari alijua kuwa wanawake ni vifaa tu vya utumishi nyumbani mwao. Haya ndiyo aliyokuwa akifunzwa na babake. Anapomwambia yeye ataolewa tu, anajua hilo ndilo jukumu lake muhimu, maana ndivyo alivyofunzwa kuamini.

Momanyi 2006, uk 29

Kando na maelezo haya, maneno ya mkewe yanaelekea kuashiria hali ubidhaishaji wasichana wadodo. Anasema;

> Bi. Amina aliendendelea,
>
> "Nionavyo mimi ni kwamba Masumbuko amekwisha kuamua kumtafutia Tumaini mchumba, na hili linanikera sana. Kwa nini mwanangu huyu mdogo mwnye umri wa miaka kumi na minne tu aolewe? Kwa nini akatiziwe masomo ilhali ana ari ya kusoma? Kwa nini amsukume kwenye ndoa ya mapema ati kwa sababu anachelea aibu isiyoeleweka? Kwa nini mwanangu mwanagu anadiwe kama bidhaa inayomwozea muuzaji?"
>
> Momanyi 2006, uk 32

Maelezo yanabainisha waziwazi kuwa lengo kuu la Mzee Masumbuko kuwaoza mabinti zake ni ile kujipatia mali kupitia kwa mahari bila kujali hali ya wanawe kuwa ni wadogo kiumri.

Mzee Masumbuko pia anawaoza mabinti zake mapema, Mashaka na Rehema waliolewa punde tu walipofika darasa la saba na nane. Mashaka anaolewa na Mzee Lusimbo, ambaye pia ni mzee, na anayemptishia mashaka mashaka chungu nzima.

> Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka, na akamwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo, kama mke wa tatu.
>
> Momanyi 2006, uk 122.

Rehema naye alihiari kuolewa na kijana mwenzake aitwaye Shauri. Licha ya kuwa kaolewa na kijana mwenzake, Rehema alikuwa na umri mdogo jambo ambalo pia lilimwathiri katika ndoa yake.

> Rehema naye alihiari kuolewa na Shauri, akatupilia mbali ushauri wake. Tumaini alikumbuka jinsi Rehema alivyoteseka kujifungua mwanawe wa kwanza, Sinangoa.
>
> Momanyi 2006, uk 123

Mzee Chumo kwa upande wake anamuoa Zena kwa lazima licha ya umri wake mdogo na kumkatizia masomo. Zena alitekwa nyara na kupelekwa hadi kwa Mzee Chumo ambako alitawishwa na kuingizwa unyagoni na kufunzwa kunga za utu uzima;

> Tumaini alikumbuka vyema jinsi vijana hao makatili walivyombeba Zena juu na kumpelekea Mzee Chumo ili akawe mke wa nne. Juhudi za Zena kujiopoa ziliambulia patupu kwani vijana hao mabarubaru walimshinda nguvu.
>
> Momanyi 2006, uk 49.

Mount Kenya University

**4.8.3 Maudhui ya Elimu**

Wazee katika riwaya hii wamedhihirishwa kama kizingiti kikubwa kwa elimu ya mtoto wa kike katika jamii. Wahusika wazee hawathamini elimu ya msichana wa kike na hivyo masomo yao yanakatikia katika darasa la saba au nane wanapobaleghe tu na kupashwa tohara. Wale wachache wanaokwepa mtego huu hubahatika na kuendelea na masomo hadi chuo kikuu au vyuo anuai jinsi ilivyo kwa Tumaini licha ya kupitia changamoto chungu nzima hatimaye anafuzu kujiunga na chuo kikuu. Mhusika mwingine ni Riziki. Wazee amabo wamekuwa kizngiti kikubwa kwa elimu ya mtoto wa kike ni pamoja na Mzee Masumbuko, Mzee Chumo na Mzee Lusimbo.

Mzee Masumbuko anashikilia mila ya ukeketaji wa wanawake na punde tu baada ya kukeketwa wasichana hao huoleka na kukatisha masomo yao katika darasa la saba au nane. Hii ilijitokeza wazi pale anapowaoza mabinti zake wawili Rehema na Mashaka;

> Aghalabu Tumaini aliwaza juu ya dada zake, jinsi walivyokosa elimu kwa sababu ya tamaa ya baba yake. Mzee Masumbuko alipokea mahari ya mashaka, akamwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo.
>
> Momanyi 2006, uk 122.

Mzee Lusimbo na Mzee Chumo nao wanashiriki katika kumgandamiza mtoto wa kike kwa kumnyima elimu kwa wao kukubali kulipa mahari kwa watoto wadogo wanaostahili kuendeleza masomo. Mzee Chumo anamuoa Zena ilhali Mzee Lusimbo anamuoa Mashaka. Mzee Masumbuko alikuwa amepania kukatisha masomo ya Tumaini kwa hali na mali. Hii ndio ilimpelekea kufanya njama na Chifu Andrea ili Tumaini anyimwe ufadhili licha ya kufuzu vyema katika darasa la nane na kujihakikishia nafasi ya kupata ufadhili huo. Tumaini anapogundua kuwa babake alienda kumpata chifu, anaenda kwa mkewe kuulizia kile babake alitaka, naye anaambiwa;

> ….Bi Selina alitulia kwa muda kisha akatamka, “Babako alikuja kumshawishi chifu ahakikishe wewe huko kwenye orodha ya hao watakaofadhiliwa.”
>
> Momanyi 2006, uk 97

Ukeketaji na ndoa za mapema zimeonyeshwa kama kizingiti kikubwa kwa maendeleo ya mtoto wa kike. Inabainika wazi kuwa wale ambao hawakukeketwa wanapata fursa ya kuendelea na masomo kama ilivyo kwa Tumaini ambaye ilibidi atoroke kwao ili kukwepa mtego huo na Riziki ambaye alikuwa na bahati kwa kuwa wazazi wake walikuwa miongoni mwa wale wanaopinga mila hii potovu.

### 4.8.4 Maudhui ya ukatili

Ukatili hurejelea hali ya mtu kutokuwa na utu au huruma kwa binadamu wenzake, wanyama na hata ndege au wadudu, kwa muhtasari, chochote kilicho na uhai. Utafiti huu ulibaini kuwa maudhui ya ukatili katika riwaya hii yameendelezwa kupitia baadhi ya wahusika wazee kama Mzee Masumbuko. Mzee huyu hana huruma kwa mkewe na wanawe wanapofanya kosa au pia anapolewa. Anawaadhibu vikali jambo ambalo limewafanya kuishi kwa woga. Mkewe Bi. Amina anamwogopa mumewe kwa sababu ya udhalimu wake na ndio maana anapoamua kumpasha tohara Tumaini, Bi. Amina hafurahii jambo hilo ila anamwogopa mumewe. Bi. Halima anasema haya;

> … maneno ya Bi. Amina yalimshangaza sana dadake mdogo, kwani hakujua siku zote zile dadake alipinga tohara ya bintiye. Alielewa kuwa hofu ya kuzozana na mumewe na utengano ndiyo iliyomzuia kujiunga waziwazi na makundi ya wanawake yaliyopinga desturi hii.
>
> Momanyi 2006, uk 34

Mzee Masumbuko vilevile anadhihirisha udhalimu wake kwa mkewe pale Tumaini alipotoroka nyumbani. Mzee Masumbuko anazua rabsha na tafrani iliyomfanya Bi. Amina kuzunguka mitaa kumtafuta bintiye. Hatimaye anaporudi baada ya kumpata bintiye, anamkuta mumewe akimngojea akiwa tayari na hasira si haba, anamlenga na fimbo aliyokuwa nayo ambayo pengine ingempata ingemwangamiza au kumjeruhi vibaya. Isitoshe, Bi. Amina anapoukwepa, anachukua upapnga na kumfukuza, hadi anapokimbia kwa nyumba ya Mzee Okwemba.

> Masumbuko alisimama ghafla na kumnyooshea ule ufito huku akitamkwa kwa hamaki, "Yuko wapi? Yu wapi huyo mwanao Mchuro uliyeenda kumtafuta enh? Nijibu haraka ama…" kabla mkewe hajajibu, Masumbuko alimrushia ule ufito kwa nguvu zake zote. Ufito ulifyatuka kama mshale, ukayoyomea kwa Bi. Amina ambaye alichutama ghafla na kuupisha. Ufito uliupiga Dhoruba kali mpapai uliokuwa umepndwa hapi uani ukakatika vipande viwili.
>
> Bi. Amina aligeuka kuutazama mpapai wake uliokatika na kudondosha mapaipai mabichi ambayo yalitapaa uani pale. Alipogeza uso kumtazama Masumbuko, alimwona akikimbilia upanga wake uliokuwa umesimikwa karibu na mlango. Papo hapo aliinuka akapiga mbio hadi kwa mzee Okwemba. Aliupiga mlando kwa nguvu na kujitoma ndani bila hodi. Mara moja aliukomea mlango kwa ndani bila kujali alikokuwa Mzee Okwemba.
>
> Momanyi 2006, Uk 36

Hapa ukatili unaojitokeza ni ule wa kutaka kumwangamiza mkewe, bila shaka angempata mkewe wakati ule huenda angemkata kwa ule upanga aliokuwa ameuchukua, ufito ule vilevile ulikuwa unahatarisha maisha ya mkewe na hatimaye ukatili kwa mimea ambapo ule mpapai unakatika na kuangusha mapaipai mabichi.

Mzee Masumbuko pia anawagandamiza wanawe hasa wanapokosea. Tumaini anapopatikana kwa kina Riziki na Idi, anaelezwa kuwa babake ameendea upupu, mmea ambao unawasha mtu agusapo. Tunaelezwa yafuatayo;

> … "Naam, baba ana mazoea ya kutuadibu kwa kututia ndani ya gunia pamoja na majani ya upupu. Natumaini mnajua jinsi yanavyowasha. Baada ya kulifunga gunia ndi kwa Kamba, ndipo anapomchapa anayeadhibiwa hadi fimbo ivunjike vipande vipande. Isipovunjika, nawaambia ataendelea kuchapwa hadi mpita njia atokee kumkemea. Wakati huo wote, mama husimama mbali na hathubutu kutamka lolote. Kwa hivyo, nadhani sasa nadhani yumo mbioni kunisaka anitie mikononi nikapambane na upupu," alieleza Tumaini huku akijishika tama.
>
> Momanyi 2006, Uk 28.

Hii ni ithibati tosha ya ukatili wa Mzee Masumbuko kwa wanawe. Vilevile ukeketaji wa watoto wa kike ni aina nyingine ya ukatili unaoendelezwa na mzee huyu. Anahakikisha kuwa wasichana wake wanatahirishwa na Tumaini anapokataa anamkana kuwa si mwanake. Rehema na Mashaka nao walikubali na hatimaye walipata utata wakati wa kujifungua.

### 4.8.5 Uongozi mbaya

Mtafiti aligundua kuwa pia kuwa maudhui ya uongozi mbaya yamepitishwa kwa kuwatumia wahusika wazee katika riwaya hii. Wazee kama vile Mzee Masumbuko anatumia nafasi inayotokezwa na kuwepo kwa uongozi mbaya na usiojali haki kuendeleza ukandamizaji wake. Mzee huyu anashirikiana na Chifu Andrea ili kuhakikisha kuwa masomo ya Tumaini yanafika ukingoni kwa kukosa kupewa ufadhili. Anampa chifu huyo mlungula naye chifu anamhakikishia kuwa jina lake Tumaini halitakuwa kwenye orodha itakayopeanwa.

> ….hapo alimsikia chifu akisema ana orodha ya watoto wanne ambao wanastahili kusaidiwa. Kisha akaendelea kuwataja majina yao. Lahaula! Jina la Tumaini halipo kabisa. Wote waliotajwa ni wale wavulana wanne waliofaulu mtihani pamoja naye.
>
> Momanyi 2006, uk 101

Kukosekana kwa jina la Tumaini kwenye orodha hiyo inadhihirisha uongozi wa chifu kuwa nim baya. Uongozi huo unajali rushwa ili kubatili haki na vilevile haujali elimu ya mtoto wa kike. Chifu huyu vilevile anapokea mlungula ili kufumbia macho maovu yanayoendelezwa na Mzee Masumbuko. Mzee Masumbuko anapowaalika wageni wa kumposa Tumaini, anaenda kwa chifu na mbuzi ili kumshawishi kufumbia macho yale yatakayojiri licha ya kuwa ni kinyume cha sheria.

> Siku moja jioni, kabla ya wageni wa Mzee Masumbuko kuwasili, Bi Halima alimwona mzee huyu akimkokota mbuzi kuelekea uani mwa Chifu Andrea. Haya yalimshtua Bi. Halima kwani hakuelewa kwa nini Mzee Masumbuko ampelekee

Chifu Mbuzi. Alisimama ghafla huku ameduwaa kama mtu aliyepokonywa ulimi. Bi halima mara kicheko kilimpasuka, “Haheee, he, he, heee! Halafu akajisikia akisema, “Mngalegeza demani; chombo ki juu ya mwamba. Maajabu ya Firauni haya!” Aliwaza iwapo Mzee Masumbuko alikuwa akienda kumhonga chifu ili kuufunika uovu aliotenda au aliotarajia kutenda.

Momanyi 2006, uk 55.

Ukimya wa chifu wakati wasichana wanaolewa na umri mdogo na kwa lazima na pia ukeketaji kuendelezwa katika eneo lake ni dhihirisho tosha kuwa Chifu huyu ni mfisadi na uongozi wake bila shaka ni mbaya.

### 4.8.6 Maudhui ya Bidii

Wahusika wazee katika riwaya hii wametumika kukuza na kuendeleza maudhui ya bidii. Wahusika wazee katika riwaya wamechorwa kuwa watu wnaojihusisha na chughuli mbalimbali ili kujiendeleza kiuchumi na kukimu familia zao. Wahusika hawa ni pamoja na Mzee Masumbuko, Mzee Okwemba na Mzee Sulemani. Mzee Masumbuko ni mkulima shupavu anayepanda mimea ya aina mbalimbali.

Kutokana na ukakamavu wake katika kilimo, shamba lake liliguna kwa wingi wa mavuno. Aidha aliatika aina mbalimbali za migomba kama vile mkono wa tembo, mkojozi, kigurue, mzungu mwekundu hata kisukati.

Upande mwingine wa shamba mzee huyu aliatika miboga. Mamumunye, na matiki yalinawiri kutokana na huduma zake pevu. Baada ya kukamilisha kazi kondeni mwake, Mzee Masumbuko aliindea konde nyingine mlimokuwa na mihindi na mimea ya pamba.

Uk 12 – 13.

Mzee Sulemani ni mzee mwingine ambaye ametumika kuendeleza maudhui haya, tunaarifiwa kuwa;

Sulemani alikuwa **mchuuzi** huko Maunguja na harakati zake biashara Mombasa zilimkutanisha na Mzee Masumbuko, ambaye aghalabu alimtembelea.

Uk 51

Mzee Okwemba, licha ya umri wake kwenda sana hali inayodhihirika kutokana na ulegevu mwilini anapopinda na uchache wa meno anapocheka, anajibidiisha kufanya biashara ya kuchuuza Samaki ambao huwatoa mbali;

Mzee okwemba aliyasitiri maisha yake kwa kuchuuza Samaki. Shaibu huyu alikuwa akitembea mwendo mrefu kwenye mabwawa ya maji ambako shughuli za uvuvi ziliendelea. Huko alijinunuloa Samaki na kuwachuuza mtaani humo. Uk 3

Wazee hawa wanatia bidii ili kuendeleza jamii zao na kujikimu kimaisha licha ya umri wao ambao umesonga na hata baadhi yao kuwa wanyonge.

### 4.8.7 Maudhui ya urafiki

Urafiki kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (1990), ni uhusiano mwema baina ya mtu na mtu, nchi nan chi au jamii na jamii; usuhuba. Maudhui ya urafiki yameibuliwa kupitia kwa wahusika wazee katika riwaya hii. Wahusika wazee wanaonyeshwa kuwa na uhusiano mwema baina yao kwa mfano Mzee Masumbuko na Mzee Sulemani. Hao wazee wawili walijuana kutokana na safari za kibiashara ambazo Mzee Masumbuko alifanya kule Mombasa. Tunaambiwa kuwa urafiki kati yao ulikuwa hadi kiwango cha kuwekeana siri;

> Chanzo cha kujuana kwao kilitokana na safari za kibiashara alizofunga mara kwa mara Mzee Masumbuko, akipeleka mikungu ya ndizi na vipeto vya matunda kuuza Mombasa.
>
> Sulemani alikuwa mchuuzi huko Maunguja na harakati zake za kibiashara Mombasa zilimkutanisha na Mzee Masumbuko ambaye aghalabu alimtembelea. Urafiki shadidi uliimarika kati ya wazee hao, wakawa hawana siri kati yao.
>
> Momanyi 2006, uk 51.

Urafiki mwingine unaojitokeza katika riwaya hii ni ule unaotokea baina ya wahusika wazee na vijana. Wahusika wazee wakati mwingine huwa na uhusiano wa karibu sana na vijana ambao huwasaidia kutekeleza baadhi ya majukumu na pia kupiga gumzo nao. Mzee anayetumika kuendeleza maudhui haya ni Mzee Okwemba. Mzee Okwemba ana usuhuba na Tumaini ambaye mara nyingi anapopita pale humsaidia kufanya usafi kama tulivyoelezewa hapa;

> … "Au we nakwenda olewa uko? Aliongeza mzee huyo huku akicheka zaidi na kutazama kifurushi cha nguo mikononi mwa Tumaini.
>
> "La hasha. Nipe ufagio nikusaidie kufagia kabla sijaenda." Tumaini alimwambia huku akiweka kifurushi chake juuu ya kigoda kilichokuwa karibu na mlango, na kuchukua ufagio. Alinyunyiza maji sakafuni ili kutoa vumbi kisha akaanza kufagia kila pepmbe ya kile kibanda.
>
> "We ndito musuri kwelikweli. We nasaidia mii sana," mzee alisema huku akikiendea kigoda kingine na kuketi. Mara nyingi Tumaini ilimsaidia mzee huyu kusafisha kijumba kile mbali na kumtekea maji na kumchanjia kuni.
>
> Momanyi 2006; 80-81

Mazungumzo baina ya Tumaini na Mzee Okwemba yamejaa ucheshi kuashiria mlahaka mwema ulio baina yao. Vilevile, ni dhahiri kuwa Tumaini anampenda Mzee Okwemba kwa kuwa tunaelezewa kuwa mara nyingi humsaidia na vilevile Mzee Okwemba humpa Samaki waliosalia baada kuchuuza mchana kutwa.

### 4.8.8 Maudhui ya mila, desturi na tamaduni

Mila kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (1990), ni mambo yanayofanywa na jamii fulani yanayolingana na asili, mazingira na nyendo za jamii hiyo. Utamaduni nao ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Mila na tamaduni hubadilikabadilika kutoka jamii moja hadi kingine na pia hubadilika kadri muda unvyosonga. Utafiti huu ulibaini kuwa maudhui haya yameangaziwa katika riwaya hii hasa mila zilizopitwa na wakati kama vile ndoa za mapema na ukeketaji, kutafutiwa mchumba, nafasi ya mwanamke na ubabedume.

Ndoa za mapema zinashadidiwa katika jamii hii na wahusika wazee licha kuwa ni mila iliyopitwa na wakati. Wahusika wazee ndio wanaohusika katika kuwaoa na kuwaoza wasichana wenye umri mdogo. Mzee Chumo, Mzee Lusimbo na Mzee Masumbuko ndio wanashirikiana katika tendo hili. Mzee Lusimbo alimwoa bintiye Masumbuko aitwaye Mashaka naye Mzee Chumo akamwoa Zena msichana wa shule. Mzee Masumbuko pia anamwoza bintiye Rehema kwa kijana aitwaye Shauri. Katika jamii hii pia, ndoa za lazima zinaenziwa na kushikiliwa na wazee. Zena alibebwa na vijana kwenda kuingizwa kwenye unyago na kuozwa kwa lazima. Katika sherehe hiyo, vipengele kadha vya utamaduni wao hujitokeza kama ilivyo katika maelezo yafuatayo;

> Alimhurumia Zena ambaye alitawishwa, akaingizwa unyagoni na kufunzwa kunga za utu uzima. Haya yalimfanya akose kwenda shule ili asubiri kuolewa na Mzee Chumo. Hapo ndipo wangealikwa wazazi, jamaa na marafiki kushuhudia ndoa hiyo isiyo na misingi ya mapenzi kwa wawili wapendanao. Ng'ombe, mbuzi na kuku wangechinjwa na waalikwa wangesherehekea kwa wingi wa vyakula na vinywaji. Ngoma ya kiasili ingechezwa, watu wangeingia katika mwtibwiriko na minenguo ya tangu jadi. Hapo Zena angejitokeza mbele ya kaumu akiwa na mume wake Mzee Chumo. Hata kama hakuyafurahia yote yale kutokana na lazima za wazazi kuolewa, angelazimika kutia tabasamu la bandia ili mradi afurahishe umati. Hapo vigelegele na riboribo za arusi vingepamba na kushamiri katika maskani yake mapya. Ndipo wanawake wangejitayarisha kupakua majungu ya vyakula aina aina na kutitika ili kuwashibisha waalikwa hao. Baadaye, tembo la kiasili lililoivishwa likaiva lingewaburudisha hadhara kwa wingi wa vicheko na nderemo.
>
> Momanyi 2006, uk 50

Katika sehemu hii, mambo yanayoibuka ni pamoja na ndoa za lazima, unyago kwa wanawake kama njia ya kutolewa utotoni kuingizwa utu uzima, vyakula na vinywaji hasa tembo kuwepo kwenye sherehe, pamoja na ngoma ya kiasili. Vipengele hivi vinaibuliwa kutokana kwa kuwepo kwa ndoa ya Mzee Chumo na Zena ambaye ni msichana mdogo.

Ukeketaji ni tamaduni nyingine iliyoshika kasi katika jamii hii na inayoshikilia na wazee kama Mzee Masumbuko ambaye anahakikisha kuwa mabinti zake wanatahirishwa kisha kuolewa.

Mount Kenya University

Wanawe Rehema na Mashaka waliridhia kupashwa tohara naye Tumaini alikataa na kutoroka kwao. Anapotoroka babake anajaribu njia za kumuoza na hatimaye anaamua kumuoza mbali ili kujiondolea aibu. Anapoibua dhana hii inaashiria kuwa wazee katika jamii hii hasa ukoo wa kina Masumbuko bado wanashikilia imani hii.

> Tumaini alikuwa hajakoshwa unyago au hata kufunzwa unyumba. Ndiyo maana aliamua angemwoza bintiye mbali sana na kwao. Sababu nyingine ni kuwa alitaka kuficha aibu ya kuchekwa na wazee wa ukoo wake kwamba amemweka msungo nyumbani.
>
> Momanyi 2006, uk 51-52

Wazee katika jamii hii bado wanamwangalia mwanamke kama kiumbe dhaifu ambaye anafaa kubakia tu jikoni na nyumbani ili kutekeleza majukumu ya ulezi na upishi. Mtoto wa kiume ndiye anayethaminiwa zaidi katika jamii hii. Hii inadhihirika na mafunzo ambayo Idi amepewa na babake ya kuwaona wanawake kama watu wa kuolewa tu na baada kuolewa wataishia kubakia jikoni.

> Pacha hao walifuatiwa na mtoto wa kiume aliyeitwa Idi. Huyu alimanda sana babake, sio kwa sura tu bali hata kwa tabia. Alikuwa mwingi wa hamaki na ukaidi. Kutokana na vitimbi vya babake, kijana huyu mdogo aliwaona dada zake kama watumishi tu pale nyumbani. Alithibitisha haya kutokana na kauli kalikali alizoelekeza kwa dada zake, kama vile kuwaambia wao ni kama bidhaa za uwekezaji tu pale nyumbani. Walisubiri tu kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomesha.
>
> Momanyi 2006, uk 14.

Kutokana na maelezo haya tunabaini kuwa Mzee Masumbuko alikuwa anashikilia utamaduni wa kuwaona watoto wa kike kama vitega uchumi tu na kuwa elimu haikuwafaa, nafasi yao ni kuolewa na kulea na kupikia mwanaume. Vilevile mwanamke katika jamii ihii anaweza kudhulumiwa na kufanyiwa madhila chungu nzima na mwanamume bila kusema lolote au kupinga kauli za mwanamume kwa ajili ya kutunza ndoa yake. Bi. Amina ni mhusika anayepitia madhila chungu nzima mikononi mwa Mzee Masumbuko ambaye humdhulumu kwa kumpiga mara nyingi hadi kiwango ambacho Bi. Amina hawezi akamkomesha mumewe anapowaadhibu wanawe kupita kiasi. Vilevile huwa anamwadhibu kwa kisingizio kuwa alimlipia mahari;

> … Vilio vya mshangao vilisikika miongoni mwa wale wanawake, huku wazee wakijaribu kumpokonya Yusufu ile bakora. Alitaka kuivunjia kichwa cha shemejiye, huku akisema bakora hiyo ndiyo anayoitumia Mzee Masumbuko 'kumwadhibu' mkewe ambaye ni dadake, kwa kisingizio kuw alimlipia mahari.
>
> Momanyi 2006, uk 63.

Kauli hii inadhihirisha wazi baadhi ya imani potovu inayoshikiliwa na wazee kuwa mwanamke anastahili kuadhibiwa na mumewe kwa sababu ya kulipa mahari.

Jambo jingine ambayo mtafiti alibaini inayowakilisha utamaduni wa Kiafrika ni kuwepo kwa tembo katika sherehe au tukio lolote la kijamii. Katika riwaya hii, wakati wa kupanga tohara ya Tumaini, mamake Tumaini Bi. Amina anandaa vyakula pamoja na tembo, Tumaini anapotoroka, analalamika kuwa amewaletea hasara kubwa;

> "Sasa wewe unaogopa kutahiriwa tu? Tazama hasara uliyotuleta. Majungu ya pombe yameivishwa tayari, makapu ya vyakula hadi sasa yanarundikana mwangu nyumbani, watu wanazidi kuniletea tu."
>
> Momanyi 2006, Uk 31

Vilevile, posa za Tumaini zinapoletwa na Mzee Sulemani, tembo inaadaliwa na kunywea na wazee;

> …. Hata hivyo, aliamua kuyatupilia mbali Mawazo hayo na kuwaingiza wazee wale katika gumzo la unywaji pombe.
>
> Momanyi 2006, uk 57.

Ni dhahiri kuwa katika jamii hii, tembo huthaminiwa na hutumiwa na wazee hasa wakati wa sherehe kujiburudisha na kupitisha wakati.

### 4.8.9 Maudhui ya migogoro

Migogoro inarejelea migongano, mikwaruzano au kukosekana kwa maelewano baina ya watu au makundi ya watu kuhusu jambo fulani. Wahusika wazee wametumika kuendeleza maudhui haya ya migogoro katika riwaya ya *Tumaini (2006)*. Wazee kadha wanajipata ndani ya migogoro ambayo baadhi hutatuliwa na nyingine zinaishia kwa vurugu na hata mapigano.

Kuna mgogoro unaotokea baina ya Mzee Masumbuko na mkewe Bi. Amina pale Tumaini anapotoroka nyumbani kwao. Mzee Masumbuko anamlazimisha mkewe aende amtafute bintiye na anaporudi bila bintiye, nusura amwangamize kwa ufito aliokuwa nao mkononi na kisha kumfukuza kwa upanga hadi pale Bi. Amina anakimbilia chumba cha Mzee Okwemba ndipo anasalimika.

Mgogoro mwingine unaibuliwa baina ya Mzee Masumbuko na Shemejiye ppamoja na wazee wengine wakati Mzee Sulemani anakuja kumposa Tumaini. Mgogoro huo unasababishwa na shemejiye kupinga mpango huo wa Tumaini kuozwa kwa mwanawe Sulemani. Mgogoro huu unatibua kikao kizima kilichokuwa kimepangwa kwa nia ya kujadili posa za Tumaini.

> “Sasa shemegi ni ya nini haya na mambo huyajui? Kwanza sikukualika hapa uje kuzusha zogo mbele ya wageni wangu,” tafrani zilimzidi Mzee Masumbuko, akawa anatayataya mle sebuleni. Kisha alipasuka, “Wewe wajua peupe Tumaini aliasi mila za kwetu na kukimbilia kwa mamake mdogo. Kilichobaki ni kumwoza ili nisafishe jina la ukoo wangu-” Lakini Mzee Majungu alimkata kalima kwa kusema, “Masumbuko mbona wamwaga mtama penye kuku wengi? Unataka kutwambia kuwa unataka kumwoza bintiyo kwa kuchelea aibu?”
>
> “Ndiyo maana umesafiri ughaibuni kumtafutia mchumba?” Mzee Seyai aliuliza, huku akionyesha kuchukizwa na vitendo vya Mzee Masumbuko…
>
> Uk 63

Hali hii nzima inaonyesha mgogoro mkubwa ulio baina ya wazee waliojumuika kujadili posa za Tumaini. Hali hii ilichangiwa na wazee waliolikwa kutojua kilichokuwa kikiendelea na mpango mzima wa Mzee Masubuko. Mzee Sulemani na wenzake wanajipata katika mgogoro huu bila kutarajia. Ilibidi wote waliokuwa mle ndani waondoke baada ya mtafaruku kuzuka.

Ni dhahiri kuwa wahusika wazee ndio wametumika kuzua na kukuza baadhi ya maudhui katika riwaya ya *Tumaini (2006)* kama ilivyobainisha na utafiti huu. Nadharia ya uhalisia hushikilia dhana kuwa matukio ya kifasihi yanafaa kushabibiana na hali halisi katika jamii. Matukio katika riwaya hii yanaakisi uhalisia uliopo katika jamii nyingi za kiafrika kama vile kuwepo kwa migogoro, ndoa za mapema, ubabe dume, mtoto wa kike kukandamizwa miongoni mwa mengine na ambayo wahusika wazee ndio huchangia pakubwa.

### 4.9 Maudhui katika *Mkamandume (2013)*)

Katika *Mkamandume (2013)*), utafiti huu ulibaini kuwa wahusika wazee wametumiwa kuendeleza na kukuza maudhui mbalimbali kama vile; utamaushi, ukatili, mabadiliko, uongozi, bidii, tamaa, majuto, ukombozi, afya, ulezi, urafiki, mapenzi, uozo, ukeketaji, utamaduni, ushauri, ulevi, ukulima na changamoto zake, tamaa, ubaguzi, utu, usaliti, migogoro, dini na msamaha na maridhiano.

Mwandishi wa riwaya hii alitumiwa wahusika wazee kimakusudi ili kuweza kuafikia lengo lake na kuhakikisha kuwa ujumbe wake unwafikia wale aliowakusudia. Wahusika wazee wametumika moja kwa moja kujenga maudhui hay ana kwingine wametumika kuwajenga wahusika wengine wanaoendeleza maudhui haya. Utafiti huu ulibaini maendelezo ya maudhui ifuatayo;

#### 4.9.1 Maudhui ya utamaushi

Utamaushi hurejelea hali ya mtu kukata tamaa ama kukosa matumaini juu ya jambo fulani. Hali hii huweza kutokea pale ambapo mtu ametia bidii katika jambo fulani mara kadhaa na

akakosa kufanikiwa au mwenyewe akaona kuwa hana uwezo wa kufanikiwa kutokana na kukosa nguvu, fedha, elimu na mambo mengine yanayohitajika. Katika *Mkamandume (2013)*) mtafiti alibaini kuwa baadhi ya wahusika wazee walidhihirisha hali ya kukata tamaa.

Mhusika aliyetumika kuendeleza maudhui ni Mzee Mkamandume. Mkamandume ni mhusika aliyekuwa na bidii maishani itokea akiwa kijana akipigania ukombozi wa Malelejimema, alikuwa mkulima shupavu ambaye aliatika mimea mbalimbali kama mihogo na migomba (uk 23). Hata hivyo, mambo yanapomwendea kinyume na mazao yake kuonyesha dalili ya ugonjwa ambao hawaujui, mzee huyu anakata tamaa na kuhiari kufyeka kila kitu shambani mwake. Vilevile maneno yake mwenyewe yanadhihirisha mtu aliyekata tamaa, anasema;

> "…. kuanza upya katika hali hii niliyonayo? A-a, mimi nimekwisha. Nimechelewa kutambua. Nimechelewa kujua. Na anayechelewa kachelewa! Hasa aki'sha kama nilivyokwisha mimi. Kisu kimeingia mpaka mifupani."
>
> Uk 377

Maneno haya yanadhihirisha wazi kuwa Mzee Mkamandume katamauka, hana imani tena ya kuanza kazi ya ukulima. Vilevile alipoelezwa yale ambayo yalifanywa na Shombo, Mkamandume anasema kuwa ameshajimaliza;

> "Wewe, hata wewe Shombo yakhe…" Alijisikia anasema, ingawa hakuwa na hakika, "huwezi kuulinda unyumba wako utaweza kunimaliza mimi? Mimi huwezi kunimaliza wewe Shombo maana nimeshajimaliza mwenyewe. Tazama hapa nilipo sina hisia, sina hofu, sina wasiwasi. Ni mtu mwingine Shombo mimi, unapiga ngumi ukuta b're utauumiza mkono wako!".
>
> Uk 451.

Mkamandume anaposema kuwa keshajimaliza, inadhihirisha kuwa ashatamauka na hivyo hana chochote cha kupoteza na anazidi kusema hana hisia wala hofu ni dhahiri hana cha kupoteza tena.

### 4.9.2 Maudhui ya ukatili

Utafiti huu ulibaini kuwa maudhui ya ukatili yamekuzwa na kuendelezwa kwa kupitia wahusika wazee. Ukatili huu unajitokeza kwa viwango mbalimbali kama vile baina ya mtu na mwenzake au baina ya makundi ya watu. Katika hii, maudhui haya yameendelezwa na Mzee Mkamandume anayedhihirisha ukatili wake kwa kuwaangamiza mahasimu wake kwa upanga. Mkamandume anamuua Shombo kwa kumvizia anapotoka msikitini (uk 483), anamuangamiza Bosi wake tena kwa njia hiyihiyo ya kuvizia na kumkata shingo (uk 486), ndiye mwenye kuwaua wazazi wake Soud Aziz Kindy na Mahfudha kama anavyosema Bwan Sleyyum;

> “Inanistaajabisha sana mimi Soud.” Sauti ya Bwan Sleyyum ilirudi chini na kufyonza huzuni nyingi mno. “Inanishangaza kuwa wewe unajua kuwa Mkamandume ndiye alimwua babako na mamako na bado ukawa unataka kumwolea binti yake…”
>
> Uk 301

Ukatili wa Mkamandume vilevile unajitokeza wakati anapata habari kuwa Viwe ni mja mzito. Mkamandume anamshika shingo na kutaka kumwangamiza, mkewe na Time wanapojariu kumwokoa pia nao wanahasiriwa na mzee huyu bila huruma, hadi wanakijiji wanapofika kuitikia vilio vya Tufaa na Time walipoona mambo yanakwenda mrama. Uk 112. Ukatili vilevile ulikuwa ukiendelezwa na polisi kama alivyofanyiwa Bwan Sleyyum alipokamatwa kwa madai ya Mkamandume kuwa kasema Bwan Aziz kauawa na kudhulumiwa bure;

> …. ingawa alipozungumza na mtu yeyote yule, hata mkewe Bi. Mwana, alitaja mauti ya Bwan Aziz tu, si mauaji yake! alijifunza kutotoa mawazo yake waziwazi baada ya kutoka kwa Bamkwe. Kule alikokwita yeye jahanamu ya dunia! Huko ndiko alikofunzwa adabu na hatimaye kushonwa mdomo. Ile fikra tu ya kulala chini kwenye saruji mbichi bila ya hata kirago kulikomtumbua pumu za maisha; kulala katika kijichumba kidogo kilichosheni mikoromo na mashuzi ya mahabusi ba wasio na hatia, na kile kinyesi kikukwa na kidogo katika debe kinachokesha usiku kucha na kutupwa asubuhi, ilitosha! Seuze vile walivyomfanya, yaani kumvuta chini mwake! Lo! Hataki kukumbuka.
>
> Uk 254

Haya maelezo yamesheheni ukatili usio mfano unaoendelezwa na polisi na pia viongozi. Mle ndani mlikuweomo na watu walio na hatia na pia wasio na hatia. Uwepo wa watu wasio na hatia ni dhihirisho la unyanyasaji.

### 4.9.3 Maudhui ya Uongozi mbaya

Uongozi unarejelea hali ambapo viongozi wa taifa fulani hawafuati sheria inavyopaswa. Wao huendeleza maovu kama vile ufisadi, unyanyasaji, matumizi mabaya ya vyombo vya dola, unyakuzi wa ardhi na ukosefu wa huduma muhimu. Utafiti ulibaini kuwa, wahusika wazee katika *Mkamandume (2013)*Mkamandume (2013) wametumika kukuza maudhui haya kama vile Mkamandume, Bwan Sleyyum na Mzee Mkasi.

Bwan Sleyyum ni mmoja wa waathiriwa wa unyanyasaji uliokuwa ukiendelezwa na viongozi kwa kupitia matumizi mabaya ya vyombo vya dola. Bwan Sleyyum alishikwa kwa sababu ya maneno ya Mkamandume ambaye alimripoti kuwa kazungumzia mauaji ya Bwan Aziz na bila uchunguzi wowote kufanywa, Bwan Sleyyum alitiwa ndani (uk 254). Madhila yaya haya yalimpata Mzee Mkasi aliporipotiwa na Mzee Mkamandume kwa sababu ya chuki tu. alimwekelea kosa, naye Mzee Mkasi akashikwa na kutiwa ndani na vilevile ardhi aliyopewa

na Bw Aziz lilinyakuliwa na utawala mpya (uk 184). Wakati wa mazungumzo baina yake na Time wanasema haya;

> "Sijasahau," alijibu Time kwa huzuni, "Siwezi kusahau mambo yaliyokukuta kwa uchochezi wa babnu. Ulitiwa ndani zaidi ya mara sita bila kosa lolote. Mimi najua hukuwa na kosa. Huwezakje mtu kama wewe kuwa n akosa? Makosa yenyewe hukukimbia wewe."
>
> "Kosa nilikuwa nalo," alithibitisha Mzee Mkasi huku akijaribu kupasua kicheko cha kejeli, "Kosa langu kubwa bila shaka lilikuwa kwa nini sikuunga zamani wala suingi mkono mpaka sasa dhambi zao?"
>
> Mohammed 2013 uk 186.

Mkamandume naye hakusalimika hatimaye, anajipata akinyanyaswa na uongozi uliopo kwa kunyimwa haki anayostahilli. Mkamandume ni mchapa kazi afisini na tuzo za mfanyakazi bora zinapotolewa, kila mmoja anatarajiwa kuwa ndiye atapata ile tuzo hiyo inaenda kwa mtu mwingine kila mara kwa sababu ya kuwa karibu na bosi wake (uk 26). Tuzo hizi zinatolewa licha ya wizara kulalama kuwa hakuna fedha za kutosha (uk 26), jambo linalodhihirisha ubadhirifu baina ya viongozi. Mkamandume anapoomba kupewa mapumziko, anatarajia kuwa atalipwa, ila anaambiwa kuwa wizara haina pesa licha ya kuwa alikuwa amepewa kazi ya kushukisha sofa mpya iliyonunuliwa (uk 330) jambo liliompa matumaini ya kupata malipo ila alikosa na hatimaye ananyimwa haki yake kwa kisngizio cha kukosa kurudi kazini. Bosi anaonyeshwa kama mtu mfisadi na ambaye amejilimbikizia mali nyingi kwa muda mfupi jambo lilaloashiria kuwa ameiba mali ya umma. Haya yanajitokeza Mkamandume anapoenda jiji kula na kula kwenye hoteli hiyo ambako kisadfa anasikia mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea kando yake;

> … Mara alimsikia mmoja kati ya wale wawili waliobaki juu ya meza akiuliza swali.
>
> "Huu mkahawa wa nani?"
>
> "Hujui wa nani?"
>
> "Nitajuaje mambo yote?"
>
> "Aaa, lakini mwenye mkahawa huu ni maarufu, ana makampuni mengi sasa, ana viwanda, ana majumba ya kukodisha, ana mahoteli, ana mikahawa ana… bepari letu kubwa…"
>
> "Nani lakini?"
>
> "Waziri wetu wa biashara. Juzijuzi tu alikuwa mchochole kamili. Jana alikuwa mkurugenzi katika ofisi moja. Utajiri wote huu kaupata wapi?"
>
> "Ennh," alishituka kidogo aliyeamshwa.

"Ndiyo kazi yao, wanaiba serikalini kujenga hifadhi yao nyumbani."

"La, wanaiba mali yetu wananchi."

Uk 440

Mazungumzo haya yanadhihirisha hali ya uozo uliopo serikalini ambako viongozi huiba mali ya wananchi. Vilevile wanapanga njama ya kunyakua ardhi iliyo Malelejimema karibu na ufukwe ili kujenga hoteli ya kifahari ila wananchi wanakataa wakongozwa na wazee ambao wanamwendea Soud kwa ushauri kuhusu hatua watakayochukua ili kuokoa ardhi yao (uk 479). Uongozi uliopo katika Malelejimema ni mbaya na usiojali haki za wazee wala raia zao, ikizingatiwa kuwa wakati wa Maandamano askari wanawamwagia risasi licha kuwa waliokuwa mstari wa mbele walikuwa ni wazee (uk 486-487). Hivi inamaanisha uongozi wa Malelejimema hauwajali wazee. Vilevile, kazi wanazofanyishwa afisini wazee ni nyingi mno na nzito. Kwa mfano Mkamandume anafanya kazi ya kuosha vyoo ambavyo ni chafu mno na hapewi vifaa vya kutumia kuosha (uk 323), juu ya hayo, analazimishwa kushukisha sofa mpya iliyonunuliwa licha ya kuwa wafanyikazi wenzake hawapo. Inamlazimu kutafuta msaada kwa mzee mwingine ambaye ni tarishi, Mzee Mwamedi (uk 331). Kufanyishwa kazi ngumu kwa wazee hawa ni dhihirisho la ukatili unaoendelezwa na viongozi katika viwango mbalimbali.

Licha ya madhila wanayofanyiwa moja kwa moja, uongozi unaendeleza unayanya kwa kuwakosesha wananchi hasa wazee mahitaji muhimu kama vile huduma za afya ambapo hawana bima wala serikali haishughuliki kuwapa fidia wanapoumia kwa mfano Kombo anapopigwa risasi anaachwa hospitalini bila kupata fidia wala malipo yoyote ya bima na mshahara unaocheleweshwa (uk 366). Ukosefu wa maji ni jambo jingine pamoja na vifaa muhimu za kufanyia kazi. Mzee Mkamandume analazimika kuweka maji kando ili atumie kufanya usafi maana maji hayapatikani. Vilevile vifaa vya kuoshea vyoo havipatikani na hivyo kumlazimu kuingia chooni bila hata kufunga mapua licha ya harufu kali (uk 323).

Mwandishi wa riwaya hii ameshughulikia maudhui ya uongozi kwa upana hasa uongozi mbaya kwa kupitia wahusika wazee ambao wanaathirika kwa njia ya mojamoja kutokana na uongozi uliopo. Matatizo wanayopitia wazee katika riwaya hii yanawakilisha au kufanana na yale ambayo baadhi ya wazee wanapitia katika jamiii kama ilivyo katika mihimili ya nadharia ya uhalisia.

### 4.9.4 Maudhui ya majuto

Majuto yanarejelea hali ambapo mtu huwa huzuni inayosababishwa na kosa lililotokea au alilofanya hapo mbeleni na akakosa kupata fursa ya kubadilisha mambo hasa baadaye

anapogundua kosa hilo. Baadhi ya wahusika wazee katika jamii, hubainisha hali ya kuwa na majuto baadaye maishani. Mihimili ya ndaharia ya uhalisia inadai kuwa yanayaotokea katika jamii ni sharti yawe na uhusiano wa moja kwa moja na matukio halisi katika jamii. Katika *Mkamandume (2013)*) (Mohammed 2013), mtafiti alitambua Mzee Mkamandume kama aliye na majuto mengi kutokana na maovu mengi aliyoyafanya hapo mbeleni. Mkamandume aliwaangamiza watu wengi katika vita vya kikabila, aliwaangamiza pia wazaziwe Soud kando na kuwasingizia wengine na kuwafanya watiwe mbaroni kama vile Mzee Mkasi, Bwan. Sleyyum kando na kuwagandamiza wanawe kama vile Viwe na Time. Mkamandume anapogundua uovu aliotenda hapo baadaye anapatwa na majuto. Huenda ikawa hili ni jambo mojawapo lililomfanya Mzee Mkamandume kuwa kama mwehu na kuishia kukosa kuzungumza na watu ila nafsi yake mwenyewe. Haya yanajitokeza ifuatavyo;

> Ufyekaji wa vichwa ulimjia tena. Na matarajio ya baada ya kufyeka yakafuata. Kwa muda wote huo baada ya ushindi wao, Mkamandume aliamini kwamba vita vile vilikuwa vya halali na manufaa kwa wote…
>
> Mkamandume alitaka kujuta lakini hakujua ajutie nini au vipi. Alijikuta anapiga kelele ndani ya moyo wake… tumedanganywa … wapumbavu sisi … wajinga … tumedanganywa … Alisikia vyema ile sauti yake ya ndani sasa.
>
> Mohammed 2013 uk 20

Ugunduzi alioufanya Mzee Mkamandume kuwa kule kufyeka haukuwa wa manufaa kwao hata kidogo linamfanya kujutia matendo yake ya hapo awali na kuwa na msongo wa mawazo. Anapoenda kwa Mzee Mkasi kuomba msaada Mzee Mkamandume anajikuta akiwa na mawazo tele yanayodhihirisha majuto. Tunaelezwa kuwa;

> Katika kususuika hivi, Mkamandume zilimjia kumbukizi za aina kadha. Kwanza pale zamani walipokuwa wakipigania uhuru wao, ujumbe mkubwa ulikuwa uhuru na kazi. Leo umekuwa uhuru na maneno na wachache kujilimbikiza mali inayozalishwa na wengi kwa jasho. Tena zilimjia kumbukizi za chuki zake kwa Mzee Mkasi. Aliwaza jinsi alivyowapikia majungu akamnyang'anyisha shamba alilopewa na Bwana Aziz Kindy tokea uhai wake. Kisha akamtilisha ndani. Na sasa katika fikra hizo alimwona Mzee Mkasi katika macho yake, siku ile alipoendewa kuambiwa shamba lile si lake tena lazima ahame akatafute pepngine pa kuishi kuendesha maisha yake. kisha alimwona hivihivi siku ile aliyokwendaa kuchukuliwa korokorono. Na sasa pale katika maficho allipotuama Mkamandume alijikuwa akisema na Mkasi kwa mbali.
>
> Mohammed 2013, 378-379.

Mkamandume anajutia matendo haya yake ya hapo awali alipomtendea Mzee Mkasi maovu tele na anapoenda kwake anajawa na hofu na kumbidi kujificha pia anapozungumza ingawa ni nafsini mwake anadhihirisha woga wa aina fulani.



Mount Kenya University

Mzee Mkamandume anajutia vilevile kumfukuzaViwe wakati ule alipompata akiwa na mimba na kumhasiri kasoro afe mikononi mwake.

> … Mkasa wa Viwe si mkasa, ni kashfa. Katika kashfa hii, Mkamandume ilimjia siku ile aliyopambana na wanawe na mkewe alipokuwa kimbinginya Viwe. Angelimuua kama sikuja kwa watu wengi kumpapatua. Matokeo ni kumfukuza Viwe. Na Mkamandume akaona hangejali lolote katika makiwa yake. sasa miaka mitatu tena, jicho la Mkamandume halijakutana na lake Mkamandume. Kila mtu yumo katika dunia yake. Viwe katika mwitu unaoitwa jiji, amekwenda kujivurumiza katika giza kama mnyama aliyeasi. Anatamba katika jiji lililozungukwa na kila aina ya hatari. Mkamandume alijua hivyo na hakujali. Lakini sasa taathira ya kujua iko wazo zaod kuliko ilivyokuwa jana au juzi. Kwa hivyo anajihisi kujali. Ndiyo kwanza sasa amaizi ujinga wake. Mtoto kachezea kinyesi, kisha kawatapakaza watu wake…
>
> Uk 318.

Mkamandume anajutia tendo lake la kutaka kumwangamiza bintiye wakati ule na pia kumfukuza kwake. Amegundua kuwa tendo hilo lilikuwa la kijinga na hivyo kumfanya kujutia hatua aliyochukua. Anapojaribu kujishawishi kuwa ilikuwa haki kutenda vile fikra zake zinakataa.

Majuto ya mkamandume yanamfanya kuishia kuomba msamaha kwa mahasidi wake ambao aliwakosea hapo awali japo wakati huo hakuweza kusema nao moja kwa moja bali alidhihirisha haya kwa vitendo vyake. Mzee Mkamandume anajutia maovu aliyowatendea Bw. Sleyyum pamoja na Nadia. Anaenda kwa Bwan Sleyyum na kuwakuta wakiwa sebuleni na Nadia. Anapokaribishwa kukaa anasita na badala yake anaamua kupiga magoti na kulia dhihirisho la kuomba msamaha jinsi ambavyo wenye nyumba hiyo walitafsiri;

> "Karibu uketi sofani." Alitafadhalisha Bwan Sleyyum.
>
> "Hasemi siku hizi." Alijibu Nadia.
>
> "Hata na sisi tumeshasikia kwamba hasemi, lakini keti Bwana Mkamandume, tukutilie kikombe cha chai?
>
> Hapo ikatokeza miujiza. Mkamandume alikwenda chini taratibu, huku machozi yakimtiririka. Magoti yake yalipofika pale chini, aliinamisha kichwa na kwenda chini zaidi mpaka akakaa mkao wa kusujudu. Kilio kikubwa na cha nguvu kikamtoka. Akalia hapo kwa muda mbele ya mshangao wa kila mtu. Alipokwisha kulia kwa shake na kwikwi shibe yake, alisimama, akataka kusema neno lakini lisitoke. Alipoona hivyo aligeuka ghafla na haraka akatoweka kama alivyoingia.
>
> Uk 409-410.

Matukio kama haya yanajirudia pale Mzee Mkamandume anapoenda kumuaga Nadia kwenye uwanjwa wa ndege anaporudi ulaya kwa matibabu. Mkamandume hasemi lolote ila anaishia kugumka na kulia pasi na kutoa sauti yoyote ila machozi yanamtoka, Soud na Nadia wanamuelewa na hivyo Nadia anamwambia kuwa amemsamehe (uk 459).

### 4.9.5 Maudhui ya mila na utamaduni

Mila na utamaduni ni sehemu muhimu ya kila jamii. Mila na tamaduni za jamii hutofautiana ingawa kuna baadhi zinazokaribiana hasa miongoni mwa jamii zinazopakana. Mila na tamaduni mara nyingi hushikiliwa na kuendeleza na wazee katika jamii. Katika *Mkamandume (2013)*), mwandishi wake alifuata mkondo huu katika kukuza maudhui haya. Mwandishi alishughulikia maswala kama vile ukeketaji, upishi, ndoa, uendeshaji wa familia.

Ukuketaji ni swala ambalo limejitokeza katika mazungumzo ya Bi. Reja na Bi. Tufaa wanapopanga njama ya kumtoa mimba Viwe. Kisingizio chao eti itakuwa ni kumpeleka Viwe kumchezea unyago. Ni dhahiri kuwa kisingizio hiki hakingepingika kwa sababu ni sehemu ya tamaduni ya jamii hii.

> "Basi Viwe tutamchukua kwa kisingizio cha kumchezea unyago, lakini lengo letu ni kumtoa mimba kwa madawa ya kienyeji …"
>
> Uk 103.

Utamaduni wa watu huhusisha imani hasa kuhusu chimbuko lao. Katika *Mkamandume (2013)*), imani hii ipo na inaendelezwa na Mzee Mkamandume. Mzee Mkamandume anaithamini kisima cha Msera kwa kuwa anaiamini kuwa ndicho kitovu chake kama alivoelezwa na mababu zake. Mkamandume anaendeleza mila hii kwa kuwaelimisha wanawe na wajukuu wake kuihusu. Kwa mfano Mkamandume anakumbuka walivyokuwa na babake;

> Mkamandume akajikuta anamkumbukia babake, Mjaka Mkamandume, alipokuwa akija naye hapo kisimani Msera siku zile alipokuwa yeye mdogo. Na baba mtu akamwambia, "Baba, hapa ndipo penye *panga* yetu. Hiki ndicho kitovu chetu. Hapa ndipo palipochimbuka asili yeti. Ndipo yalipoanza makazi na makuzi yetu adhimu- tangu na tangu. Hapa ndipo walipo wazee wetu na ndipo tulipo sisi na vizazi vyetu. Ndipo tunastahiki kuwepo sisi sote. Leo na kesho na kesho kutwa. Pabovu. Pabaya ndiyo. Pananuka. Pameoza. Uk 32.

Vilevile ni jukumu la wazee kuelimisha wajukuu wao kuhusu tamaduni za jamii yao kwa mfano anamchukua mjukuu wake Mkamandume na mwanawe Katija kwenda mle kisimani anapokwenda kukiaga kisima kile, kisha anawaeleza kuwa ndicho kitovu chao (uk 480). Mzee Mkasi pia anajikuta akitekeleza jukumu hili la kuwaelimisha wajukuu hasa Soud na Time kuhusu baadhi ya mila na pia historia ya jamii yao. Time anapomtembelea wanazungumzia

mengi kuhusu utamaduni kama vile wazee kuamini kwamba watoto wao wanabaki kuwa watoto tu hata wakiwa watu wazima (uk 177) na matukio ya hapo awali kama vile uchinjaji, kule kushtumiwa na babake Time (uk 179 – 187).

Kipengele kingine cha utamaduni kinachojitokeza katika riwaya hii kupitia wahusika wazee ni swala la ugawaji wa majukumu ubaina ya wanaume na wanawake. Katika jamii hii, mwanamume hatarajiwi kuingia jikoni kupika. Bwan Sleyyum anafunga leso na kuingia jikoni kusaidia na upishi, Bi. Mwana hutoka nje mbio kwa kuwa ni jambo ambalo hatarajii kufanywa na mwanamume (uk 288).

Jukumu jingine katika jamii hii ni uchinjaji wa kuku. Hili ni jukumu linalotarajiwa kutekelezwa na wanaume na si wanawake kama inavyojitokeza pale Mzee Mkasi anapotembelewa na Time. Hata hivyo, Mzee huyu anaonekana kusaili hekima ya tamaduni hii;

> "Mchinje wewe," alishauri Mzee Mkasi ambaye kila siku tokea ujana wake hakuwa na moyo wa kuchinja kuku na baadaye ukubwani kuchinja kukuu kukawa kunamkumbusha kuchinja watu alikokuona wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe.
>
> "Kwa nini?" Time alijifanya hajui miko ya mzee huyo.
>
> Mchinje tu…" Alikazania.
>
> "Mila za Waswahili lakini zinashikilia kuku achinjwe na mwanamme."
>
> Uk 166.

Jukumu la kuendesha familia kwa maana ya kuwapa mahitaji ya kila siku kama vile chakula na mahitaji mengine ni jukumu la mwanamume kama inavyodokezwa kupitia kwa Mzee Mkamandume hasa pale alipokosa malipo na kushindwa kuikimu familia na jambo la mkewe kuendesha familia linampa maumivu;

> Sasa ukweli huu unaonata aliuona waziwazi Mkamandume. Aliuhisi kwa maumivu makali! Fikra ya kukopa, kuomba ilimshitua! Fikra hiyo ilimsumbua kwa maana nyingi.
>
> Kwanza aliitikadi kwamba yeye ndiye mwendesha nyumba. Si dhamana ya Tufaa kwamwe kuiendesha nyumba! Hizi ni fikra alizorithishwa mkono kwa mkono kutoka kwa wazee wake. Ndizo fikra pekee alizozijua kuhusiana na mkewe. Mwanamume asiyeweza kuiendesha nyumba yake ameshakatwa uume wake.
>
> Uk 366.

Ni wazi kuwa imani hii ya mwanamume kuendesha familia ni imani inayorothishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kushikiliwa na jamii hasa wazee, ndio maana inamwia vigumu mzee Mkamandume kuikabili fikra hii ya mkewe kuendesha nyumba yake.

Vilevile mafiti alibaini kuwa wahusika wazee wametumiwa kuibua mila ya utoaji wa kafara katika jamii hii. Mzee Mkamandume alikuwa na ng'ombe mmoja ambaye alikuwa akimfuga kwa minajili ya utoaji wa kafara mwakani ili kuweza kuepuka balaa;

> Pesa hana, hata kitu chochote hana? La; anacho! Ana ng'ombe mtamba wa pepo wao. Ng'ombe kilishizo cha kafara ya siku ya mwakakoga. Kilishizo cha bwanamkubwa. Yule pepo aliyeanza kufugwa na huyo oMkamandume wa mwanzo mhenga wa wahenga. Amefugwa pepo huyo awe kinga ya ukoo wao. Mila inasema, ikiwa ukoo utashindwa kutekeleza kitiba cha kuchinja ng'ombe siku yam waka koga (mwaka hata mwaka), basi ukoo huo utafikwa na laana au balaa.
>
> Uk 383-384.

Itikadi ya kuoa na kuozwa kwa wasichana wadogo inajitokeza katika riwaya hii kwa kupitia wahusika wazee. Mzee Mkamandume anakumbana Tukaije ambaye ni Jirani yake mle kisimani. Tukaije kutokana na maelezo bila shaka ni msichana mdogo na Mzee Mkamandume anabaki akijiuliza maswali kuhusu kuolewa kwake mapema;

> …. Mwanamke mwenyewe Tukaije Jirani yake. Mdogo sana kwake, na mdogo sana kwa mumewe pia. Kwa nini wanaume huoa watoto wadogo kama hawa? Labda hali hii ya kulazimishwa kuolewa na watu wazima au wazee ndiyo iliyomfanya Tukaije awe mtundu kidogo ingawa mke wa watu.
>
> Uk 369.

Vipengele hivi vya utamaduni vimeshughulikiwa kwa kina na ukamilifu kwa kutumia wahusika wazee. Kwa kutumia wahusika wazee mwandishi amefaulu kuafikia lengo lake la kufikisha ujumbe ambao unadhihirisha hali mbalimbali na mila mbalimbali baadhi ambazo zimepitwa na wakati na zingine ambazo zinastahili kubadilishwa.

### 4.9.6 Changamoto za uzee

Mwandishi pia alidhamiria kuibua changamoto ambazo wahusika wazee wanapitia katika jamii. Kwa kuwa fasihi ni kioo cha jamii inayoagazia maswala na changamoto ambazoo wanajamii hupitia. Mtafiti alibaini kuwa mwandishi huyu alishughulikia changamoto ambazo wahusika wanapitia kama vile magonjwa, ukosefu wa mahitaji ya kimsingi, msongo wa mawazo miongoni mwa mengine. Kwa kupita Bwan Sleyyum, mwandishi alidhihirisha matatizo yanayowaandama wazee kama ifuatavyo;

> …kisha alijitazama tena yooni na sasa akagundua kwamba mwili wake umempuuka kidogo, lakini alama za uzima zinamfufurika kila pahala mwilini mwake, ukitoa ile miguu inyomvimba na kumwuma bila sababu-labda ndio ishara ya uzee tena.
>
> Uk 257.



Mount Kenya University

Changamoto zinazojitokeza katika sehemu hii ni kama vile hali ngozi kubadilika, miguu kuvimba na kuuma. Kutokana na umri uliosonga, wazee katika jamii hukabiliwa na changamoto kama hizi katika jamii.

Bi. Naima vilevile anapitia changamoto za kusikia vyema kutoka na hali ya uzee. Bi. Mwana anamweleza Soud kuwa ziku hizi anapitia changamoto za kulazimika kupiga kelele anapozungumza naye;

> "Nakuuliza vijana, vijana, vijana," Soud alikazania na kupaza sauti kwenye neno kijana, "nakuuliza vijana hawajambo?"
>
> "Eee?"
>
> "Vijana hawajambo?" Soud alirudia suala huku akipaza sauti zaidi.
>
> "Hawajambo." Hatimaye Bi. Naima alilipata suala na kutoa jibu sahihi, na baadaye akaungama, "Eee mume wangu we, masikio yangu yamekuwa mazito ziku hizi, sisikii vizuri, sharti ukase sauti sana."
>
> "Basi n'do kazi niliyonayo hapa," alirukia Bi. Mwana, kutwa hivyohivyo nipige naye kelele. Jasho litakutoka! Ukimwambia hivi anakwambia vile. Maji anasema moto. Moto anasema maji…"
>
> Uk 283.

Changamoto nyingine ni kuwa wazee hukumbwa na magonjwa ya mara kwa mara kutokana umri wao ambao umesonga sana kama vile Bi. Naima ambaye tunaarifiwa kuwa siku hizi ni mgonjwamgonjwa;

> "Bibiye hajambo?" Soud aliuliza kwa wasiwasi kidogo.
>
> "Mzima, yuko jikoni anamalimaliza … njaa zinauma tena…"
>
> "Na Bi. Naima?"
>
> "Yupo tu, ende wapi? Lakini siku hizi ni mgonjwamgonjwa …"
>
> Uk 280

Kifo ni changamoto nyingine inayowakumba wahusika wazee kutokana na hali mbalimbali ambazo wanapitia. Baadhi ya wahusika wazee waliaga dunia kama vile Mzee Mwemedi pamoja na Silima. Kifo cha Mzee Mwemedi kilitokea bila Mkamandume kupata habari na hivyo alikosa fursa ya kuhudhuria mazishi yake (uk 365). Silima yasemekana alikuwa akiugua kwa muda kabla ya kifo chake;

> "Mbona umezubaa? Hukunyoohsa hata mikono kumpokea maiti na kutabaruku kwa sunna? Sasa unangoja nini, twende tukamsindikize mwenzetu?" Alitoa rai Mahmudu.
>
> "Mwenzetu?" Aliwaza Mkamandume.

"Huna habari?"

"Sina! Nani kwani?" Alijibu Mkamandume kwa macho.

"Silima… alikuwa akiumwa siku nyingi tu …"

Uk 401.

Kifo cha Silima kinadhihirisha kuwa mauti mengine yanayowakumba wahusika wazee ni kwa sababu ya magonjwa yanayowaathiri. Mhusika huyu alikuwa ameugua kwa muda mrefu kabla ya kifo chake. Ugonjwa aliougua haukutambulika na ugonjwa huo ulimfanya akakonda na kupuuka na pia akili zilimtoka. Wahusika wengine ambao kutokana na usuhuba wao na Mkamandume huweza kuchukuliwa kama wazee na kutokana na hali yao wametumika kuonyesha changamoto ambazo wahusika wanapitia. Mkamandume anapowaona wakibeba maiti anashangaa;

> Yule pale Bakari aliyekwenda naye shule pamoja. Uso umemchujuka na meno ya mbele kumtoka. Na yule Vuai aliyesoma naye Kor'an chuoni, kabakia mifupa. Na tena Mussa aliyesuhubiana naye zamani uvuvini, mweupe kwa safura. Huyu na yule, yule na huyu. Wengi aliowajua na waliomjua. Lakini Hapana aliyemwona Mkamandume sasa. Hapana aliyekuwa mzima au aliyekuwa akitazamika. Wote walikuwa *maitikwenenda*. Hata wale wadogo wake mara mia Mkamandume aliwaona wabovu zaidi kuliko yeye. Wamegeuka wakongwe wa miaka tisini na saba. Hivi ndivyo walivyobaki kwa matesa ya makusudi.
>
> Uk 400.

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa wahusika hawa walipitia changamoto tele maishani yaliyofanya miili yao kuchujuka na kuonekana kuzeeka zaidi ya walivyo. Mhusika mwingine anayedhihirisha changamoto wanasopitia wahusika wakongwe ni Bi. Mkubwa ambaye aliaga baada ya kubanwa mbavu aking'an'gania vitunguu;

> Kisa kimoja hataisahau kamwe Mkamandume. Katika msongamano wa kuwania vitunguu vibovu, bimkubwa mmoja wa miaka sabini ihivi alibanwa mbavu katika kibiru akapinduka chini na kupoteza fahamu. Alipochukuliwa hospitali hakuchukua siku nyingi aliiaga dunia.
>
> Uk 392.

Kisa hiki kinaonyesha changamoto ambazo mhusika huyu alipitia ambayo ni pamoja na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kama vile vitunguu, kukosa heshima na msaada kutoka kwa wanajamii wengine ambao hawakugundua kuwa hangeweza kusukumana nao kutokana na umri wake ambao ulikuwa umesonga na mwili wake kuanza kukosa uwezo wa kuhimili mbanano na hivyo kupelekea kuvunjwa kwa mbavu zake zilizosababisha kifo chake. Kwa kuwatumia wahusika wazee hivyo basi, mwandishi ameweza kuibua baadhi ya changamoto ambazo wazee wanapitia katika jamii.



Mount Kenya University

### 4.9.7 Maudhui ya ukulima na changamoto zake

Ukulima umejitokeza kama maudhui muhimu iliyoendelezwa kupitia kwa wahusika wazee katika riwaya hii. Mtafiti alibaini kuwa mwandishi alikusudia kubainisha baadhi ya changamoto zinazowakumba wakulima katika jamii pamoja na tija inayoweza kupatikana katika ukulima kando na kuonyesha kuwa ukulima umewachiwa wazee katika jamii. Wahusika vijana hawajihusishi na ukulima licha ya kuwa wao ndio wenye uwezo wa kuingia shambani na kufanya kazi. Mwandishi amewatumia wahusika wazee kama vile Mzee Mkasi na Mzee Mkamandume.

Mzee Mkasi ni mkulima hodari anayeatika mimea ya aina mbalimbali katika shamba lake. Mzee huyu alikuwa amepanda migomba ya ndizi, mihogo, mayungwa, viazi vitamu, michungwa, michenza kangaja, michenza ajemi, milimau, mbirimbi ya kushitukia, midimu, mibalungi, mistaafeli, mitufaa na minazi ya kitamli licha ya kuwa na kitalu kidogo (uk 161), kando na upanzi wa mimea mbalimbali, mzee huyu alifuga kuku. Hii ni dhirisho tosha la mkulima mwenye bidii.

Mzee Mkamandume vilevile alikuwa mkulima hodari aliyekuwa akiatika mimea mbalimbali kama mihogo na ndizi. Hata hivyo anakumbana na changamoto zinazomfanya kuamua kufyeka mazao yake shambani. Changamoto hizo ni pamoja na magonjwa yanayoathiri mazao yao na ambayo hayashughuliwi na walio mamlakani kwani hao hawajali;

> Hatimaye Mkamandume alizindukana na kujikuta mazingira yamemfumaniza na kumweka mkabala na ukweli mbichi unaonanta. Alitupa jicho kutoka pale alipokuwa kasimama na mbele yake, mbali na ule mwembe boribo. Huko alikagua kwa jicho la hasira konde yake ya mhogo na migomba. Konde jina tu. Haikuwa na cha kustahiki kuitwa konde. Majani ya mhogo yalikuwa ngozi ya kikongwe iliyosinyaa – alama ya ushindi wa maradhi sugu ya mimea yaliyoshinda dawa. Na migomba imesimama kama iliyopigwa radi. Kumeingia nini katika tegemeo la mkulima? Kinatokezea nini?
>
> Uk 21-22

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa kuna maradhi yanayoathiri mime ana dawa ambazo wanatumia hazijawasaidia. Uongozi uliopo pia unaonekana kutojali;

> Hayo na yawe masuala yasiyo na majibu, alilolijua Mkamandume ni kuwa hakuna aliyejali tena. Wanaohusika hawahusiki itena ila kufukuzana na vivuli vyao katika dunia *usoni twende…*
>
> Uk 22.

Kando na athari ya magonjwa, kuna unyakuzi wa ardhi na mabadiliko ya hali ya anga ambazo zinawaathiri wakulima;

> …uonevu ni upi zaidi ya hii unaomkuta kila mtu siku hizi? Eti wameua ili kuchukua ardhi. Haya wameshachukua hiyo ardhi nd'o imekuwa nini? Mashamba yote yameota magugu. Minazi imeparama. Mikarafuu imesibiwa na maradhi tusiyopata kuyasikia. Mihogo inadhiika. Migomba inakauka! Nchi imesibika, imedamirika! Haina Samaki, haina kaa, haina Kamba, haina ndege, haina baadhi ya matunda. Kila kitu kimekimbia na wenyewe.
>
> Uk 255

Changamoto hizi zimewaathiri sana wahusika wazee maana hao ndio wamejiingiza katika ukulima hasa baada ya wengi wao kustaafu au wengine kukosa chaguo lingine. Mwandishi ameibua changamoto hizi kwa nia ya kuonyesha ukosefu wa juhudi miongoni mwa viongozi za kutatua matatizo yanayowakumba wakulima na badala yake kujilimbikizia tu mali nyingi.

Mwandishi wa riwaya hii amefaulu kuwasilisha maudhui yake kwa kutumia wahusika wazee. Katika uwasilisha wake, amezingatia mtindo wa kihalisia unaoafikiana na nadharia ya uhalisia ambapo maudhui yaliyowasilishwa yanafanana na matukio katika jamii na vilevile wahusika waliotumika ndio mara nyingi huathirika na huhusishwa na masuala yaliyoshughulikiwa kwa kupitia wazee hawa.

### 4.10 Fani katika Riwaya ya *Tumaini (2006)*

Senkoro (2011) anafafanua fani kuwa ni ule ujuzi wa kisanaa unaoutumiwa na mtunzi katika utunzi wake. Wamitila (2008) anafafanua fani kuwa ni jumla ya mbinu, mitindo na vifaa anavyotumia mtunzi kuiwasilisha maudhui na lengo yake. Fani huweza kuhusisha vipengele kama vile, wahusika, lugha, mtindo, muundo na mandhari. Mtafiti alijikita katika kutafiti jinsi waandishi walitumia wahusika wazee kufanikisha matumizi ya lugha.

Mwandishi wa riwaya hii aliteua mbinu za lugha kiubunifu na kwa kuzingatia wahusika mahususi wana. Wahusika wazee wametumia lugha teule ianyoashiria upevu wao kiumri na pia uwezo wao wa kufinyanga lugha kulingana na miktadha mbalimbali. Baadhi ya mbinu zilizotumika na wahusika wazee pamoja na zile ambazo mwandishi ametumia kwa wahusika wazee ni kama; methali, tashbihi, misemo na nahau, lafudhi, dayalojia, maswali ya balagha, taswira, kinaya, majazi na chuku.

#### 4.10.1 Matumizi ya methali

Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupifia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa (Kamusi ya Kiswahili Sanifu 1990). Utafiti ulibaini baadhi ya methali zilizotumika na wahusika wazee au wahusika wengine pamoja na mwandishi kuzungumzia

Mount Kenya University

baadhi ya mambo yanayowazungukia wahusika wazee. Baadhi ya methali hizi ni kama zifuatazo;

Msiba wa kujitakia hauna kilio (uk 40); methali inatumika na Mzee Yusufu wanapoongea na Mzee Masumbuko kurejelea kule kutoroka kwa Tumaini jambo ambalo lilisababishwa na yeye Mzee Masumbuko kutaka kumkeketa. Methali nyingine ilitumika na Mzee Majungu kwa Mzee Masumbuko. Anamuuliza;

> Lakini Mzee Majungu alimkata kalima kwa kusema, "Masumbuko, mbona wamwaga mtama penye kuku wengi?"
>
> Uk63

Mzee Majungu alihiari kutumia methali hii badala ya kutumia maneno ya wazi kumkemea mzee mwenzake ishara tosha ya hekima na ujuzi walionao wazee. Methali nyingine inatumika na Bi. Amina mkewe Masumbuko kujaribu kumshawishi kuhudhuria sherehe ya bintiye kufuzu ila Masumbuko anadhihirisha hasira tele, anamwambia;

> "Punguza hasira mwenzangu. Mwungwana hanuni mashavu, hununa moyoni."
>
> Uk 152

Methali nyingine inatumika na mwandishi mwenyewe kuelezea athari ya matusi aliyotoa Mzee Masumbuko kwa shemejiye Shabani. Anasema;

> Shabani aliufungua mlango ili mzee huyo aweze kutoka, lakini ikinyume na hayo, alimiminiwa matusi mfululizo. Matusi hayo yalimkera mno Shabani na kumhakikishia kuwa hakika ulimi unauma kuliko meno.
>
> Uk 64

Kupitia kwa wahusika wazee mwandishia aliweza kupata fursa ya kutumia mbinu katika uandishi wake ili kuhakikisha kuwa ujumbe wake umepokelewa inavyofaa na hadhira lengwa.

### 4.10.2 Matumizi ya misemo

Hizi ni kauli fupi zinanzotumiwa na jamii mahususi na zilizo na maana napia hupitisha maadili au hukoleza utamu lugha. Msemo inafasiriwa kama fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalum ili kutoa maadili ilhali nahau ni fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana ya kawaida ya maneno hayo. Nahau aghalabu hutumia kitenzi katika kuiunda. Utafiti huu ulibainisha kuwa mtafiti aliweza kutumia mbinu hii katika kazi hii kupitia kwa wahusika wazee. Baadhi ya nahau na misemo zilizotumika na wahusika wazee au kwa wahusika wazee ni kama;

Chuki humchoma anyehifadhi uk 151, kauli iliyotolewa na Bi. Amina akijaribu kumsihi mumewe waweze kwenda sherehe ya Tumaini baada Mzee Masumbuko kumkana Tumaini, hivyo msemo huu unatumiwa ili kumkumbusha Mzee huyu athari ya chuki.

Nahau zilizotumika katika riwaya hii na wazee ni kama vile;

Ana mkono wa barafu (uk 66)

Kupasua mbarika (uk 61)

Mtu na hamsini zangu (uk 40)

Nyumba hii aione paa (uk 39)

Kujitia za mtonga (uk 40)

Akili zako kwenda likizoni (uk 40)

Hizi ni baadhi ya nahau zilizotumika na wahusika wazee katika riwaya hii ili kuhakikisha kuwa ujumbe umefika ipasavyo na kuwa lugha ya mwandishi imenata na kupendeza.

**4.10.3 Matumizi ya Tashbihi**

Tashbihi ni mbinu ya kufananisha vitu viwili kwa kutumia viunganishi ili kutoa maelezo faafu, kujenga taswira au kuhakikisha kuwa ujumbe unaopitishwa umeeleweka vyema. Baadhi ya tashbihi zilizotumika ni kama zifuatazo;

Mzee huyu alilima mithili ya trekta (uk 12), kurejelea jinsi Mzee Masumbuko alikuwa akilima.

Mnachuuza watoto kama vipeto vya matunda (uk 41), maelezo haya yalitolewa na Mzee Yusufu akirejelea ile hali ambapo wasichana wanapashwa na tohara na kuozwa ili wazee wapate mahari.

Kufyatuka kama risasi kuelekea chumbani mwake (uk 41), kurejelea jinsi Mzee Masumbuko alipoondoka mle sebuleni.

Vibega vikainuka juu kama vya ndege (uk 123), kutoa taswira ya hali ya mashaka baada ya kuolewa na Mzee Lusimbo na kupitia madhila mengi.

> Aliendelea kusimama pale nje kama sanamu, akikodolea macho kiwiliwili kile cha mpapai. Alimeza mate na kuyahisi machungu kama shubiri
>
> Uk 37

Mount Kenya University

Maelezo yanayorejelea Bi. Amina anaporudi na kuona madhara ya ufito kwenye mpapai. Jambo hilo lilimshtua sana akabaki kusimama pale na kuwaza. Mbinu ya tashbihi imetumika katika ujenzi wa taswira na kufanikisha ufafanuzi wa mwandishi kuhusu matukio mbalimbali yanawazungukia wahusika wazee.

### 4.10.4 Matumizi ya Lafudhi

Lafudhi hurejelea matamshi ya mzungumzaji yanayotokana na lugha yake ya mwanzo au lugha zinazomzunguka. Mtafiti alitambua kuwa mbinu hii imetumika kwa mhusika ambaye ni Mzee Okwemba. Kutokana na matamshi yake, mzee huyu anaweza kutambulika anakotoka na athariya lugha yake ya kwanza katika matamshi yake. Kwa mfano, badala ya kusema mwizi yeye anasema 'mizi' pale Bi. Amina anapoingia kwake kujiokoa alipokuwa akifukuzwa na Mzee Masumbuko;

> …. Alibatuka kwa kelele "Mizi…mizi.. iko mizi!" aliwaita majirani.
>
> Uk 36 – 37.

Baada ya Mzee Masumbuko kuondoka na Bi. Amina kufungua mlango, mazungumzo yao yanadhihirisha matumizi ya lafudhi ya mzee huyu;

> Mama Toma… ni wewe! Toka mama, yeye kwisa kwenda. Misee ile mbaya. Ye nachapa we tena," Mzee Okwemba alitamka huku akitetemeka mwili mzima kwa hofu.
>
> Uk 37.

Maneno ya mzee huyu yanadhihirisha matumizi ya lafudhi au atahri ya lugha ya kwanza ya mzee huyu. Mwandishi alinuia kubainisha chimbuko la mzee huyu na kuonyesha kuwa katika jamii, kuna watu wnaotokea maeneo mengine na kujiunga na jamii tofauti na licha ya kuishi nao, inawawia vigumu kudondosha athari ya lugha ya kwanza katika mazungumzo yao.

### 4.10.5 Mbinu ya dayalojia

Dayalojia hurejelea mazungumzo yanayotokea baina ya wahusika katika riwaya au kazi za fasihi. Mwandishi huamua kubadilisha mtindo wa maandishi badala ya kutumia usimulizi wa moja kwa moja, anatumia dayalojia baina ya wahusika mbalimbali. Katika riwaya ya *Tumaini (2006)*, utafiti huu ulibaini kuwa mbinu hii imetumika miongoni mwa wahusika wazee kama ifuatavyo;

Kuna mazungumzo baina ya Mzee Masumbuko, Mzee Yusufu, Bi. Halima, Bi. Amina na Shabani;

> "Je, Amina, umempata Tuma?" Yusufu alimuuliza, akionyesha dhahiri wasiwasi aliokuwa nao.
>
> "Naam, kaka, yuko kwa shimeji Shabani," Bi. Amina alimjibu.
>
> Nashukuru kusikia hayo. tulikuwa na wasiwasi mwingi juu yake. je sasa kwa nini hamkuja naye?" Yusufu aliuliza huku akiwatazama na kujaribu kuyasoma Mawazo yao.
>
> Mzee Masumbuko alijitoma ndani sebuleni na kumuuliza Yusufu, "Aje kwa nini? Mtoto kisirani yule. Badala ya wewe kuniuliza jinsi nitakavyowaambia wazee kuhusu jambo hili, wewe unakazana kuyajua ya Tuma."
>
> Uk 39-40

Mbinu hii vilevile imetumika kwa wahusika kama vile Mzee Okwemba na Amina uk 36-37, Mzee Okwemba na Tumaini uk 80-81, Mzee Masumbuko na wazee waliokuja kumposa Tumaini pamoja na marafiki zake kama vile Mzee Seyai na Majungu uk 60 – 62 n.k.

Nadharia ya umuundo unashikilia kuwa ni vigumu kutenga vijenzi vya fasihi kwa kuwa vinashirikiana kwa pamoja ili kuhakikisha ufanisi wa kazi maalum. Mwandishi alitumia mbinu hii ili kuweza kuibua baadhi ya maudhui, sifa pamoja na mbinu nyingine za lugha kama lafudhi iliyojitokeza katika mazungumzo ya Mzee Okwemba kwa mfano;

> "Mzee shikamoo?" Tumaini alimsabahi.
>
> "Ooh, musuri Toma, we naenda wapi? We narudi uko tena?" Mzee Okwemba alisimama huku akitabasamu na kufunua kinywa kilichokuwa na uchache wa meno.
>
> Uk 80.

### 4.10.6 Matumizi ya balagha

Maswali ya balagha ni yale ambayo hayahitaji kujibiwa na anayeulizwa bali huulizwa kwa nia ya kukejeli, kusisitiza jambo au kuteka makini ya msikilizaji na msomaji wa kazi ya fasihi. Utafiti huu umebaini kuwambinu hii imetumiwa kwa wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini (2006)*. Baadhi ya mifano ya matumizi ya mbinu hii ni kama ifuatavyo;

> "Hata kama ni Beijing, hayo kwangu siyo muhimu. La muhimu ni kwamba wanawake kama hawa ndio wanozimbia mila zetu kaburi. Hawa ndio waliokuja na malalamiko baada ya huo mkutano wa Be…Beichini kitu gani sijui – na kuanza kupayuka kuwa tohara ya kike ni mbaya. Wao hawakutahiriwa? Mama zao hawakufanywa hivyo? Je, walishindwa Kuwazaa? Tangu zamani nyanya zetu walitimiza ada hii. Mbona hawakuona kasoro yoyote ambayo hii leo mnadai ipo? Si ujinga huu? Nyie mnadanganywa na wazungu ili mdharau mila zenu, nanyi mnakubali bila kudadisi kwa nini," alisema Mzee Masumbuko kwa hasira.
>
> Momanyi 2006, uk 41.

Katika aya hii, Mzee Masumbuko anauliza maswali kadha ambayo hayajibiwi au hapeani fursa ya maswali hayo kujibiwa ili kuhakikisha kuwa hoja anayotaka kupitisha na kusisitiza imefika jinsi alivyodhamiria. Mzee Masumbuko alikuwa anajaribu kutetea azma yake ya kumpasha tohara Tumaini.

Mfano mwingine unajitokeza wakati wa mazungumzo baina ya wazee waliokuja kumposa Tumaini pale ambapo wanawaarifu waliohudhuria kikao kile kuwa walikuja kwa ajili ya posa. Mzee Yusufu anashangaa kisha kuuliza maswali yafuatayo;

> "Nani! Yusufu aliruka na kusimama wima, mikono kiunoni. Alimgeukia Mzee Masumbuko kwa hamaki na kumuuliza, "Yaani Masumbuko umewaleta wageni hawa kutoka huko - sijui wapi – Mmbrui – kumposa mtoto wetu mchanga anayesoma shule? Hii ni aibu gani hii?"
>
> Uk 61 – 62.

Maswali yanayoulizwa na Mzee Yusufu kwa njia moja ni kejeli kwa Mzee Masumbuko ambaye anafanya kitendo ambacho hakifai. Vilevile, hayo maswali lengo ni kuwakejeli wale wageni waliokuja kwa kukubali kumposa mtoto mdogo.

**4.10.7 Mbinu ya majazi**

Majazi ni mbinu ambayo mwandishi anawapa wahusika majina yanayofanana na tabia au hali zao za kimaisha. Katika riwaya hii, wahusika wazee wamepewa majina yanayolingana na tabia pamoja na hali zao kwa mfano Mzee Masumbuko.

Masumbuko ni ile hali ambapo mtu hapati utulivu, kila wakati kuna jambo linalomsumbua. Mhusika huyu anadhihirisha hali inayofanana na jina lake kwa kuwa ana mambo mengi yanayomsumbua na kumzungusha maishani kila ujao. Vilevile watu walio karibu naye wanapitia changamoto kwa kutangamana naye. Mzee Masumbuko anasumbuka kutokana na kutoroka kwa Tumaini alipokuwa akipanga kumpasha tohara. Jioni ile shimeji zake wanakuja kwake na kumuonya dhidi ya kujaribu kumpasha tohara Tumaini jambo linalomsumbua sana mzee huyu. Mzee huyu anahiari kumtafutia mchumba Tumaini kutoka Mombasa; kule kutafuta ni kujisumbua, na baada ya kufaulu kupata, mpango wake unatibuliwa na shimeji zake na kumletea masumbuko tele. Hatimaye Tumaini anapofuzu, anakataa kwenda katika ile sherehe ya kufuzu kwa sababu jambo hilo linamsumbua.

Kando na Mzee Masumbuko kusumbuka pekee, anawasumbua watu anaotagusana nao. Tumaini anapotoroka kwao, Bi. Amina anakosa amani kutokana na usumbufu wa mzee huyu, ilhali usumbufu huo huo wa kutaka kumpasha tohara na kumuoza Tumaini ndio ulisababisha Tumaini kutoroka. Mzee Sulemani anapata masumbuko mengi baada ya posa zake kukosa

kujadiliwa na badala yake kukawa na mtafuruku. Hali hii inadhihirisha kuwa jina Masumbuko linaafikiana vyema na tabia pamooja na hali ya mzee huyu.

Mzee mwingine mwenye jina la majazi ni Mzee Majungu. Neno majungu kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (1990) linamaanisha tabia ya kutoa habari za uongo dhi ya mtu mwingine. Mzee Majungu anamtahadhari Mzee Masumbuko na kutoboa siri mbele ya wageni wake na marafiki zake waliojumuika kwenye kikao cha kupokea posa za Tumaini. Mzee Majungu anasema;

> Lakini Mzee Majungu alimkata kalima kwa kusema, "Masumbuko, mbona wamwaga mtama penye kuku wengi?"
>
> Uk63.

Hivyo basi ni dhahiri Mzee Majungu hakutaka ukweli ujulikane na alilolotaka yeye ni habari za uongo kutolewa ili kuhifadhi ile siri ya Mzee Masumbuko.

Mhusika Mashaka licha ya kuwa yeye si mhusika mzee, jina lake ni la kimajazi. Jina hili liliangaziwa kwa kuwa, mashaka yaliyompata mhusika huyu yanatokana na wahusika wazee. Mashaka yake yanaanza pale anapoolewa na Mzee Lusimbo na kuishia kupata mateso na matatizo chungu nzima kama vile kutoelewana na mumewe, wake wenza kumchukia, matatizo ya uzazi na pia changamoto za kimawazo na kimwili yaliyomfanya Mashaka kukonda na vibega vyake kuinuka kama vya ndege. Mzee Masumbuko ndiye aliyemsababishia Mashaka haya matatizo yote kwa kumuoza mapema.

Mhusika mwingine ambaye jina lake ni la Majazi na udhihirisho wa jina lake linatokana na wahusika wazee ni Tumaini. Tumaini ni jina linaloashiria kutokufa moyo licha ya changamoto au hali ya kuwa na imani kuwa jambo fulani litafaulu hatimaye. Mhusika huyu anapitia changamoto tele kama vile kupangiwa tohara na babake na kisha mpango wa kuozwa kwake. Ni kuwepo kwa tumaini kuwa angefaulu kukwepa kupashwa tohara ndio ilimfanya atoroke kwao nyumbani na kwenda kwa shangaziye. Babake anapopanga njama ya kumkatisha elimu kwa kumnyima ufadhili kupitia Chifu Andrea, tumaini linamsukuma Tumain ikujipeleka kwenye ofisi ambako mkutano ulikuwa ukifanywa ili kujitetea na hatimaye anafaulu. Tumaini anaendelea na masomo yake kwa sababu ana imani kuwa atafaulu na hatimaye anazishinda changamoto na vikwazo vilivyowekwa na Mzee Masumbuko na kusoma hadi kufuzu chuo kikuu.

Bi. Amina vilevile ni mhusika ambaye amepewa jina la majazi. Neno amina ni kiitikio cha maombi kusema na iwe hivyo. Mhusika huyu anadhihirisha hali ya kukubali chochote

kinachosemwa na mumewe bila kupinga. Anaridhia kupigwa na kufanyishwa kazi nyingi na mumewe, wanawe wanapoadhibiwa na mumewe hawezi akathubutu kumsimamisha au kusema neno lolote na wakati wa Tumaini kupashwa tohara hakatai amri ya mumewe licha ya kuwa hakuwa akikubaliana na tohara hiyo ya mwanawe. Hivyo inadhihirika kuwa kila jambo kwake ni kama anasema amina kama lilivyo jina lake.

### 4.10.8 Matumizi ya Kinaya

Kinaya ni mbinu ambayo jambo au maelezo fulani yanayotumika yanatokeza kwa njia ambayo haikutarajiwa au kwa njia kukejeli au stihizai. Mbinu hii imetumika miongoni mwa wahusika wazee katika riwaya hii kama vile Mzee Sudi kupewa jina ambalo haliambatani na matukio yanayomzunguka.

Sudi humaanisha kuwa na bahati nzuri, hata hivyo mhusika Mzee Sudi katika riwaya hii anaonekana kutokuwa na bahati kwani mambo yanamwendea kombo. Anashindwa kumshawishi Mzee Sulemani kuoa tena baada ya mke wake kuaga dunia (uk 60) na vilevile wakati wa kupeleka posa, anakatishwa kauli kwa kuulizwa maswali na hatimaye kikao kilivurugika na hivyo kumuonyesha mzee huyu kama mtu asiye na bahati kwa kile ananuia kutenda.

Kinaya kingine kinajitokeza katika kile kikao cha kupokea posa za Tumaini. Haihalisi kuwa watu hasa wazee wamealikwa kwenye kikao kile bila kupewa taarifa kuhusu yale waliyoyaendea. Mwenyeji wao Mzee Masumbuko hakuwaeleza sababu ya wageni wale kuja. Mzee Masumbuko alikuwa na sababu zake za kuwaficha ila wazee wenyewe hawakuuliza, hadi pale Mzee Sudi anapowatajia na wote wanashangaa (uk 60). Kikao kile ambacho kilitarajiwa kuwa itaishia kwa sherehe, shnagwe na vigelegele, inageuka na kuishia kwa vilio na vimako jambo ambalo halikutarajiwa pia (uk 60).

Kinaya kingine kinajitokeza katika maneno ya Mzee Yusufu wakati wa mtafaruku uliotokea wakati wa kujadili posa za Tumaini. Mzee Yusufu anatoa kauli;

> “Leo utaonja utamu wa bakora hii unayompigia dadangu,” alifoka Yusufu.
> Uk63.

Katika kauli hii, anasema kuwa ataonja utamu wa bakora. Bakora ile bila shaka sit amu bali ni chungu mtu anapopigwa nayo hasa ikizingatiwa kuwa Mzee Yusufu alikuwa na hasira na alikuwa akitaka kumvunjia bakora ile kichwa cha shemejiye.

Ni kinaya kwa Mzee Masumbuko kummiminia matusi Shabani baada ya kumfanyia hisani ya kumfungulia mlango alipokuwa amefungiwa ndani;

> Shabani alifungua mlango ili mzee huyo aweze kutoka, lakini kinyume na hayo, alimiminiwa matusi mfululizo. Matusi hayo yalimkera mno Shabani na kumhakikisha kuwa hakika ulimi unauma kuliko.
>
> Uk64

Ilitarajiwa kuwa Mzee Masumbuko angemshukuru Shabani kwa kumfungulia mlango, ila anaishia kummiminia matusi tele. Kinaya kingine katika maelezo haya ni ulimi kuuma licha ya kutokuwa nan jia ya kuuma kuliko meno yaliyo na uwezo wa kuuma.

**4.10.9 Mbinu ya taswira**

Taswira inarejelea matumizi ya maelezo yanayochora picha akilini mwa msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi. Kunazo aina kadha za taswira zinazopatikana katika kazi ya fasihi kwa mfano; Taswira ya kuona/muono: Hii ni taswira inayolenga hisia za kuona. Waandishi hutumia maneno ambayo yanamruhusu msomaji au mtazamaji kuona picha ya kile kinachozungumziwa. (Kisilu, 2006), Taswira ya kusikia/Sikivu: Hii inalenga hisia za kusikia. Inaeleza sauti mbalimbali ili kumfanya msomaji au mtazamaji kusikia sauti hiyo akilini mwake (Kisilu, 2006), Taswira ya harufu/mnuso: Hii ni taswira inayolenga hisia za kunusa. Waandishi hutumia maneno yanayoelezea harufu ili kumwezesha msomaji kuhisi harufu hiyo (Mazrui & Shariff, 1994), Taswira ya mguso: lengo la taswira hii ni hisia za kugusa. Inaeleza jinsi kitu kinavyohisi unapokigusa (Mwanzi, 1993), Taswira ya Ladha/muonjo: hii ni taswira inayolenga hisia za ladha. Inaeleza jinsi kitu kinavyoonja, na kumfanya msomaji kuhisi ladha hiyo akilini mwake (Abrams & Harpham, 2014), Taswira ya kihisia: Taswira hii inahusu hali ya kihisia au ya kiakili ambayo inamwathiri mhusika au msomaji (Ngugi wa Thiong'o, 1972).

Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini (2006)* ametumia aina mbalimbali za taswira katika kazi yake. utafiti huu ulibaini baadhi ya taswira zilizotumiwa kwa wahusika wazee kama ifuatavyo;

Taswira oni imetumika katika kuchora picha ya mhusika Okwemba anapocheka. Tunapewa maelezo yafuatayo;

> Mzee Okwemba alisimama huku akitabasamu na kufunua kinywa kilichokuwa na uchache wa meno.
>
> Uk80.

Hapa msomaji anaweza kupata picha ya Mzee Okwemba jinsi alivyo na meno chache kinywani, anavyotabasamu na kusimama.

Taswira nyingine ni ile ya Zena akibebwa kuwa mke wan ne wa Mzee Chumo;

> Tumaini alikumbuka vyema jinsi vijana hao walivyombeba Zena juu juu na kumpelekea Mzee Chumo ili akawe mke wake wa nne. juhudi za Zena kujiopoa ziliambulia patupu kwani vijana hao mabarubaru walimshinda nguvu. Lililomshtua na kumshangaza Tumaini ni jinsi wapiti njia walivyokataa katakata kumsaidia Zena wakati alipowaita huku akilia waende kumsaidia. Wanaume waliambaa tukio hilo na wanawake walipita na hamsini zao.
>
> Uk 49

Katika maelezo hayo hapo juu, msomaji anaweza akapata kuona picha ya jinsi Zena alivyokuwa akibebwa, picha ya vijana wenye nguvu na pia picha ya wapiti njia wakiambaa tukio lile.

Maelezo kuhusu sebule ya Mzee Masumbuko jinsi ilivyopambwa inatoa taswira oni na pia Sikivu;

> Sebule ya Mzee Masumbuko ilikuwa imepambwa vizuri kwa minajili ya wageni hao. Makochi mawili marefu yenye rangi ya kahawia yaliegemezwa kwenye pande mbili za kuta, ilhali katika pande zingine za kuta kulipangwa viti viwili vya mbao za msonobari. Katikati ya sebule kulikwa na meza ndogo ya duara iliyofunikwa kwa kitambaa cha rangi ya sharubati chenye naksi za maua ya kijani kibichi pembeni. Juu ya meza hii kulikuwa na chupa pana yenye maua mekundu yaliyochopekwa ndani. Ukuta mmoja ulitundikwa saa yenye umbo la mstatili, ambayo ilikuwa ikitoa mlio wenye mahadhi ya kupendeza kila baada ya saa moja.
>
> Uk 57 -58.

Katika maelezo haya, taswira mbili zinajitokeza, taswira sikivu inajitokeza katika mlio wa saa ukutani, Taswira hii inajitokeza pale wageni wa Mzee Masumbuko wanapoingia na kelele za kuwakaribisha kusikika (uk 57). Pia msomaji anaweza kupata picha ya jinsi sebule hiyo ilivyopangwa na kupambwa. Mwandishi ametumia pia mbinu kuwachora baadhi ya wahusika wazee kama vile; Mzee Sudi na Sulemani (uk 59) na pia jinsi Mzee Masumbuko anavyolima (uk 12).

Taswira hisi na oni zinajitokeza katika amelezo ya Tumaini anapoeleza shangaziye jinsi wao huadhibiwa na Mzee Masumbuko. Msomaji huweza kuona jinsi mtu hutiwa kwenye gunia lenye upupu na vilevile kuhisi uchungu au mwasho unaotokana na kutiwa kwenye gunia lenye upupu. Kando na hayo, msomaji huweza kuhisi machungu ya yule anayeadhibiwa;

> "Naam, baba ana mazoea ya kutuadibu kwa kututia ndani ya gunia pamoja na majani ya upupu. Natumaini mnajua jinsi yanavyowasha. Baada ya kulifunga gunia ndi kwa Kamba, ndipo anapomchapa anayeadhibiwa hadi fimbo ivunjike vipandevipande."



Mount Kenya University

Uk 28

Mwandishi huyu alitumia mbinu hii ili kuweza kuipa uhai kazi yake na pia kuibua na kukuza baadhi ya maudhui pamoja na sifa za wahusika.

### 4.10.10 Matumizi ya Wimbo

Utafiti huu ulibaini kuwa kuna matumizi ya wimbo ambao mhusika anayelengwa na wimbo ni Mzee Masumbuko na mwimbaji wa wimbo huu ni mkewe Bi Amina. Wimbo huu ni kama ifuatavyo;

"*Yataka eee yataka moyo*
*Hasidi kuishi naye*
*Yataka ee yataka moyo*
*Hasidi kuishi naye-"*
Uk 57

Wimbo huu bila shaka uliimbiwa Mzee Masumbuko na mwenyewe anapousikia anakuwa na wasiwasi kidogo ila anajaribu kuyatupilia mbali Mawazo hayo. Wimbo huu unatumiwa kwa lengo la kupitisha ujumbe maalum na kudokeza sifa mojawapo ya Mzee Masumbuko ambaye ni hasidi wa Tumaini na mkewe Bi. Amina ambaye amepitia mengi machungu na kule kuvumilia kwake ili kutunza ndoa yake inaingiliana vyema na wimbo huu.

### 4.11 Fani katika *Mkamandume (2013)*)

Mtafiti alichunguza pia jinsi wahusika wazee wametumika kufanikisha jinsi lugha ilivyotumika katika *Mkamandume (2013)*) (2013). Mtafiti aliongoza na mihimili ya nadharia ya umuundo katika kutambua fani hasa iliyotumika na wahusika wazee katika riwaya hii ili kufanikisha dhamira ya mwandishi. Mtafiti aliweza kutambua kuwa katika riwaya hii, mwandishi ametumia mbinu mbalimbali za lugha na sanaa kwa kupitia kwa wahusika wazee kama vile; jazanda, tashbihi, taswira, majazi, takriri, maswali ya balagha, kisengere nyuma, uzungumzi nafsi, nyimbo, dayalojia, kinaya, misemo na nahau miongoni mwa mbinu nyinginezo. Katika kazi hii mtafiti aliangazia kwa kina mbinu za; jazanda, taswira, kisengere nyuma, takriri, uzungumzi nafsi, dayalojia, majazi na nyimbo.

### 4.11.1 Matumizi ya jazanda

Jazanda hurejelea matumizi ya maelezo yenye maana fiche au matumizi ya kitu kimoja kuwakilisha kingine chenye mfanano wa aina fulani usio wa moja kwa moja. Kamusi Sanifu ya Kiswahili (1990) inafasiri jazanda kama picha inayomwingia mtu kichwani au taswira.

Hivyo maelezo yanayotumiwa na mwandishi huwa si ya moja kwa moja ila yanamwezesha mtu kupata picha ya kina kutokana na ulinganishaji huo.

Mtafiti aligundua kuwa mbinu hii imetumika kwa wahusika wazee kama vile Mzee Mkamandume;

> 'Mbegu mbovu iliatikwa zamani Mkamandume na waatikaji wamekuwa hatimaye wakikaa chonjo na mara kwa mara husogea kuitilia maji na mbolea konde yao. Zamani kulikuja waatikaji waliokuwa na mikono mirefu ambao waliatika mbegu hii kila walipotua na kulowea. Kwa muda fulani mmea huu mbaya ulionekana kusitawi hapo zamani, lakini baadaye kwa juhudu za watu waliumwagia sumu na kuanza kudumaa. Ala! Katokea kidudumtu mwingine mwatikaji mweusi mwenye mkono mfupi lakini mwenye hamu ya kuhodhi na kumiliki na kumeza, kauutilia maji na mbolea tena na sasa mmea wa chuki unanawiri upya. Na kama kawaida yeye kaketi chonjo akitazama matunda ya sumu yanayozaliwa na mti huo jinsi yanavyoliwa na Wamalelejimema.'
>
> Uk 398.

Maelezo haya yanarejelea chuki iiliyoanzishwa na wakoloni ambao wamerejelewa kama waatikaji wenye mikono mirefu. Wanarejelewa hivi kwa sababu nia yao kuu ilikuwa kupora rasilimali za Waafrika na walitumia mbinu ya kuatika chuki miongoni mwa Waafrika ili kuweza kuwatawala kwa urahisi. Mmea huu kumwagiwa sumu inarejelea umoja ambao Waafrika walianza kushikana na kupigania uhuru wao. Hata hivyo baadaye viongozi wa Kiafrika walipochukua hatamu za uongozi waliendeleza tabia hii ya kupanda chuki; hao ndio wanarejelewa kama waatikaji wenye mikono fupi. Viongozi hawa wana tamaa ya kunyakua mali ya umma na kuwadanganya raia kwa kukuza na kutilia mbolea chuki miongoni mwa wanajamii inayojitokeza kama ukabila.

Mahmudu vilevile ametumia jazanda katika mazungumzo yake na Mkamandume kama ifuatavyo;

> Mahmudu alisita hapo kama kwamba kumpa nafasi Mkamandume arambe utamu wa sifa yake. kisha akaendelea.
>
> "Tatizo lake ni kutoona mapema kwamba hii ni dunia ya kutomezwa kama mbwa usasini … mbwa tu ndiye anayekabiliana na dhoruba za ngiri usasini, akitolewa jicho, akikatwa mguu, akitobolewa tumbo … bure tu! Ushindi wa mbwa kil ani wa bwana wake …"
>
> Uk 403.

Mbwa katika usimulizi huu unarejelea waliopigania uongozi uliopo kama kina Mkamandume na Silima miongoni mwa wengine walioshiriki katika vita vya kukomboa taifa lao na vilevile kushiriki katika vita vya kikabila. Kule kujeruhiwa kunarejelea madhara ambayo wale

waliosaidia kupigania taifa lao wanapata. Wao ndio huenda vtani lakini ushindi unapopatikana wao hawakumbukwi bali viongozi huchukua sifa zote na wao kupewa makombo kama vile Mkamandume kupewa kazi ya kufanya usafi licha kuwa miongoni mwa wapiganaji. Mbinu hii imetumika na mwandishi kwa nia ya kuibua maudhui mbalimbali na vilevile kuongeza ladha na kubadili mkondo wa uandishi. Wahusika wazee ndio wametumika kuhakikisha kuwa mbinu hii imefaulu.

### 4.11.2 Matumizi ya taswira

Taswira inarejelea matumizi ya maelezo yanayochora picha machoni pa msomaji ama msikilizaji wa kazi ya fasihi. Kunazo aina mbalimbali za taswira kama vile; taswira mguso, taswira oni, taswira sikivu, taswira muonjo na taswira hisi. Taswira hizi zimetumika katika *Mkamandume (2013)*), miongoni mwa wahusika wazee kama ifuatavyo;

> Hivi vilikuwa vihitimisho. Soud alibaki kakodoa macho akiajabia vipi angeweza kuingiza chochote kingine tumboni mwake lau punje ya mchanga! Juu ya meza alihesabu: tende ya kusonga samli iliyorashiwa ufuta na kudondoshewa harufu nyembamba ya tangawizi. Vileja ambavyo ukivishika vidole vinaingia ndani. Kashata za njugu. Visheti. Donasi. 'Pudin'. Chai ya maziwa nzito. Chai ya mkandaa nyepesi iliyodondoshewa majani ya mperemende na kutojozewa pilipili manga, hiliki na harufu tulivu ya tangawizi. Kahawa kavu iliyopikiwa hiliki na tangawizi.
>
> Uk 296.

Taswira zinazojitokeza katika dondoo hili ni pamoja na taswira mnuso; *...harufu nyembamba ya tangawizi,* taswira mguso; *Vileja ambavyo ukivishika vidole vinaingia ndani.* Na taswira oni; mtu anaweza kupata picha ya vyakula hivyo vilivyoandikwa mezani, wingi wake pamoja na aina zilizo mezani.

> Kwanza aliingia behewa tupu lenye madirisha katika kuta zake zote tatu. Kila ukuta ukiwa na madirisha matatu yenye vioo vya rangi. Mchana madirisha hayo hufungwa ili miale ya mwangaza ipate kupenya na kumwaga sago la rangi behewani na kuwiana vyema na rangi ya maziwa ya kuta na kukogana na rangi na harufu ya maua ya miwaridi, miafu na miasumini isiyoacha kuchanua hapo ili mianzi ya pua ya Bwan Sleyyum inase kipepo cha harufu ya mchanganyiko wa maua hayo.
>
> Uk 257

Ufafanuzi huu unaibua picha mbalimbali akilini mwa msomaji. Msomaji huweza kuona jinsi choo cha Bwan Sleyyum kinavyokaa na vilevile kunusia ile harufu inayoingia mle ndani.

Taswira mnuso na sikivu pia imedokezwa pale Mkamandume alipokuwa ameenda kisimani Msera;

> Kitambo kikapita na baadaye ndege, aghalabu chozi jabiri, pembawapi, manja, mnana, tongo, makweche, miramba na wengi wengineo walishuka hapo kwa shangwe, hoihoi, vigelevigele na sherehe fulani – sanasana juu ya vivumbasi, mitule, midizimwitu na mibambakofi. Walipokwisha kushereheea hapo kwa muda, ndege wote hao waliruka na kutumbukia kwenye machaka yaleyale na misitu ya mikarafuu. Na mwisho ule mnaso wa udi na uvumba ulinasuka katika mianzi ya pua ya Mkamandume na kupotea na walivyopotea wale popo na ndege.
>
> Uk 31.

Taswira oni anayopata msomaji hapa ni ile ya ndege wa aina mbalimbali wakitua pamoja na miti nayo taswira Sikivu inajitokeza pale ambapo ndege hao wanashuka kwa sherehe na hoihoi. Vilevile taswirra mnuso inajitokeza katika sehemu hii ambapo mnaso wa udi na uvumba unafikia mapua ya Mkamandume.

### 4.11.3 Matumizi ya kisengere nyuma

Kisengere nyuma ni mbinu ambapo mwandishi wa kazi ya fasihi anarejelea matukio yaliyotokea hapo mbelenii kabla ya kile ambacho anakizungumzia kwa wakati huo. Katika riwaya hii, wahusika wazee wametumika kuendeleza mbinu hasa wakati mwandishi anaporejelea mambo yaliyotokea wakati wa ujana wao au hapo mbeleni. Wahusika kama vile Bwan Sleyyum, mzee Mkamandume na Mzee Mkasi miongoni mwa wengine wametumika kuendeleza mbinu hii kama ifuatavyo;

> Katika kujisusuika hivi, Mkamandume zilimjia kumbukizi za aina kadha. Kwanza pale zamani walipokuwa wakipigania uhuru wao, ujumbe mkubwa ulikuwa uhhuru na kazi. Leo umekuwa uhuru na maneno na wachache kujilimbikizia mali iinayozalishwa na wengi kwa jasho. Tena zilimjia kumbukizi za chuki zake kwa Mzee Mkasi. Aliwaza jinsi alivyompikia majungu akamnyang'anyisha shamba alilopewa na Bwana Aziz Kindy tokea uhai wake. Kisha akamtilisha ndani.
>
> Mohammed 2013; uk 378-379.

Katika sehemu hii mwandishi anafaulu kutufahamisha matukio ya hapo awali kwa kutumia mhusika huyu kuwazia au kurejelea matukio hayo kama vile vita vya uhuru, chuki yake kwa Mzee Mkasi na unyakuzii waliofanya kwa kisingizio.

Bwan Sleyyum anakumbuka maisha yao ya ujanani wakiwa na babake Soud Bwan Aziz Kindy na uchumba wake na mkewe pamoja na jinsialivyoshughulikia kitalu hicho mwenyewe;

> Bwan Sleyyum pia alikuwa kachukuliwa na mandhari ya kitalu chake. Ilikuwa kama akifanya hivyo makusudi kusafisha fikra chafu ndani ya nafsi yake, ili akizitoa nje, zitoke nadhifu ili kumteka kiumbe mkaidi kama Soud.
>
> Kwanza, aliwaza juu ya shauku yake ya maua na mimea aliyokolezwa nayo tokea udogo wake alipoambukizwa skuli katika somo la elimuuuu- viumbe. Na kisha, katika umrii wa baleghe, miti na maua yakawa ni vikolezo vyake vya mapenzi,

> hasa alipokutana na Bi. Mwana. Kuna uzani katika miti, majani, maua, Bi. Mwana na mapenzzi ya wao waili pale….
>
> Pili, Bwan Sleyyum alikumbushika kwamba katika kitalu hicho mlikuwa na michezo kadha ya ujana wake - yeye na rafiki zake ambao kwa bahati mbaya wote sasa hawapo. Hasa Bwan Aziz, Mungu ampe usingizi mwema huko aliko yeye na mkewe.
>
> Mohammed 2013; uk 294

Mwandishi kwa kupitia mbinu hii anafaulu kutujuza mengi yaliyotokea katika jamii hii kama ambavyo Bwan Sleyyum anaibua maswala ya elimu na chanzo cha kupenda maua, usuli wa uhusiano wao pamoja na urafiki uliokuwepo baina yake na Bwan Aziz. Mwandishi vilevile kwa kupitia Mzee Mkasi amefaulu kutuelezea kuhusu historia ya jamii hii hasa wakati wa vita, pamoja na chanzo cha chuki baina yake na Mkamandume na madhila aliyopitia kwa sababu ya visingizio vya Mkamandume (uk 178 – 182).

### 4.11.4 Uzungumzi nafsia

Katika kutalii data iliyokusnywa, mtafiti alibaini kuwa kuwa mwandishi alitumia wahusika wazee ili kufanikisha matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia. Hii ni mbinu ambayo mwandishi hutudokezea mawazo ya mhusika fulani au mazungumzo yanayojiri nafsini mwake. Wakati mwingine huwa ni mazungumzo ila mara nyingi huwa ni fikra za mhusika. Baadhi ya wahusika wazee waliotumia mbinu hii ni pamoja na Mzee Mkamandume, huyu ndiye mhusika ambaye ametumia mbinu hii pakubwa hasa pale baada yake kuelemewa na fikra na kuwacha kuongea. Ingawa hazungumzi ila mawazo yake yanaibuliwa waziwazi na mwandishi hivi kwamba tunafahamu yanayojiri akilini mwake. Kwa mfano wanapokuwa kwenye chombo wakisafiri kwenda uwanja wa ndege, mengi yanajiri akilini mwake kama;

> "Wewe, hata wewe Shombo yakhe…" Alijisikia anasema, ingawa hakuwa na hakika, "huwezi kuulinda unyumba wako utaweza kunimaliza mimi? Mimi huwezi kunimaliza wewe Shombo maana nimeshajimaliza mwenyewe. Tazama hapa nilipo sina hisia, sina hofu, sina wasiwasi. Ni mtu mwingine Shombo mimi, unapiga ngumi ukuta b're utauumiza mkono wako!".
>
> Uk 451.

Mawazo haya ya Mzee yametiwa sauti na mwandishi ili kuweza kufikisha ujumbe anaonuia kufikisha na kutudhihirishia mipango ya mhusika huyu. Mwandishi pia ametumia njia kuendeleza maudhui mbalimbali. Mzee Mkasi pia ametumiwa kuendeleza mbinu hii. Mzee huyu anapomdadisi Time, mawazo mengi yanampitikia, anadadisi mabadiliko yake na hatimaye tunaelezwa;

> Baada ya kitambo cha kufikiri Mzee Mkasi alikenua. Kwa nini anauliza maswala ambayo majinu yake anayo kwenye ncha ua ulimi wake? Labda majibu aliyajua, lakini kilichomleta Time leo hakukijua, ingawa alishuku kilikoelekea. Pamoja na hayo shaka si haki wala halali. Mzee Mkasi atangojea yafunguke yenyewe mambo.
>
> Uk 63.

Kupitia mawazo ya Mzee huyu mwandishi ameweza kutuchorea wasifu wake pamoja na ule wa mhusika mwingine, Time, ambaye anawaza kumhusu. Time ni mwanawe Mzee Mkamandume ila anapenda kwenda kukaa na Mzee Mkasi na wakati mwingine humsaidia shambani na pia jikoni kwa mapishi. Utumiaji wa mbinu hii umefanikishwa kwa kutumia wahusika wazee.

### 4.11.5 Matumizi ya takriri

Takriri ni urudiaji wa neno, fungu la maneno au sentensi katika kazi ya fasihi. Katika *Mkamandume (2013)*) mwandishi ametumia aina mbalimbali za urudiaji kwa wahusika wazee kama vile urudiaji wa neno, urudiaji wa kifungu na vilevile sentensi nzima kama ifuatavyo;

> Kunywa! Siku ngapi ameambiwa maneno hayo Mkamandume. Kunywa! Utapata pesa tu siku moka! Kunywa! Bila shaka hilo lilikuwa Simango! Mara ngapi atakunywa bila yeye kunywesha?
>
> Uk 324.

Neno kunywa limerudiwarudiwa katika dondoo hili ili kusisitiza kile kinarejelewa. Mwandishi alikusudia kuonyesha ugumu wa hali ya Mzee Mkamandume katika kukubali kumtegemea rafikiye kazini na kuibua changamoto wanazopitia kazini.

Maneno ya Mzee Mwemedi yanarudiwa jinsi yalivyo katika ukurasa wa 329 na 366, katika mawazo ya Mzee Mkamandume;

> "…Wacha kujifanya wewe peke yako ndiye unayeumia. Na wala sioni sababu ya wewe kung'ang'ania kuona Fahari ya yote yaliyotokea. Watu wanaonufaika na kuneemeka si waliopigania kitu chochote. Ndivyo ulimwengu unavyokwenda Mkamandume, wewe tazama husaidiki. Wewe nani katika nchi hii? Ni kijidudu kidogo, pamoja na mhanga wako ulioutoa kwa kudhani ulikuwa ukiokoa nchi. Sasa ndugu zetu wenyewe ndio wanaochukua mapanga yasiyoonekana kutukeketa. Watoto wetu wenyewe ndio wanaotudidimiza. Uk 329 na 365-366

Maelezo haya yamerudiwa jinsi yalivyo si kwa sadfa bali kimakusudi ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa kupitishwa kama vile kuibua kuonyesha changamoto ambazo wapiganiaji uhuru wanapitia hasa wazee katika jamii. Hii ni dhihirisho la jinsi wahusika wazee katika riwaya hii wametumika kufanikisha matumizi ya takriri ili kupitisha ujumbe.

### 4.11.6 Mbinu ya dayalojia

Wahusika wazee katika *Mkamandume (2013)*) kulingana data iliyokusanywa wametumika ili kufanikisha matumizi ya mbinu hii. Wahusika waliotumika ni pamoja na Bwan Sleyyum akizungumza na Soud, Mzee Mkasi na Time, Mzee Mkasi na Soud na Nadia kama ifuatavyo;

> "Haki, haki, haki, kuna haki gani hapa?" Bwan Sleyyum alionekana kaghadhibika kidogo, na ilipobainika kwamba sauti yake ilipanda kidogo, alijikataza na kumtaka Soud samahani.
>
> Soud alinyamaza kimya kwa muda, kisha taratibu akamjibu Bwan Sleyyum. "Naweza kukisia kiwango cha hisia zako. Na kwa kweli una haki na una sababu kabisa kukasirika, lakini … lakini …" Soud alijishauri moyoni nini aseme, au kama aseme alilotaka kusema. "Nadhani roho yangu moja …"
>
> "Ikitoka basi?" Alimaliza Bwan Sleyyum kauli ya Soud.
>
> "Usifanye ujinga huo. Una watu wanaokupenda na kukutathmini. Huko peke yako …"
>
> "Sikukusudia hayo … Nimekusudia kwamba mimi kijana, sina fungamano zozote za kunizuia kupigania haki zangu na za wengine …"
>
> Uk 300

Maungumzo haya yanadhihirisha tofauti iliyopo baina ya wahusika wa umri mbalimbali. Vilevile mwandishi aliitumia mbinu hii kuwajenga wahusika wengine kama vile Soud na kuibua sifa za wahusika wazee.

Mzee Mkasi anatumika kuendeleza mbinu hii pia kama ifuatavyo;

> "Oooo bibiye," alianza kutania, "yoyoyo bibe amefika yoyoyo … karibu."
>
> Nimeshakaribia bwana," Time alirejesha mzaha. Tabia ya Waswahili, babu kumtania mjukuu wake kwa mzaha wa mume na mke – ingwa mzee huyu si babu yake Time mzaa baba au mama.
>
> "Karibu uketi… chukua kibao hicho hapo upenuni."
>
> "La, sitakaa nikakutazama wewe ukifanya kazi – leo zamu yako kukupikia… nimekuja makusudi, maana sitaki ulie wivu".
>
> Wivu n'talia tu, maana hapa hupiti mpaka upotee njia".
>
> Kimya. Wakawa wanatazamana na kuchekeana.
>
> "Mchi uko wapi?"
>
> "Mchi wa nini?"
>
> "Nikusaidie naona kutwanga mhogo…"
>
> "Wacha tu. Hulioni joto na jua hilo? Nitakutoa jasho b're Bi. Mrembo"
>
> (Uk 161-162.

Mazungumzo haya baina ya mhusika na kijana yanabainisha wazi jinsi wahusika wazee walivyofaulisha matumizi ya dayalojia.

### 4.11.7 Mbinu ya majazi

Majazi ni matumizi ya majina yanayolingana na tabia ya mhusika fulani. Kutokana na data ya utafiti huu, ilibainika kuwa baadhi ya majina ambayo wahusika wazee walipewa yanalingana na hulka zao. Baadhi ya wahusika hawa ni pamoja na Mkamandume, Mponda na Mkasi.

Jina Mkamandume linatokana na maneno mawili ambayo ni "mkama" na "ndume"; mkama linarejelea mtu anayekama ambalo ni tendo la kufinya pande zote za kitu kilichomo vitu majimaji kama vile matiti. Kwa kawaida anayekamwa ni ng'ombe wa kike ila hapa anarejelewa kama mtu aliye na uwezo wa kukama ndume. Hii ina maana kuwa mhusika huyu ana bidii ya kufanya jambo ambalo linaonekana kama haiwezekani, na vilevile licha ya juhudi za kukama ndume, mkamaji hawezi akapata chochote ila kujiumiza bure. Mzee Mkamandume anaafiki sifa hizi za kufanya bidii katika juhudi za kukomboa nchi yake, ukulima na vilevile kabila lake. Licha ya bidii yake hii, hatimaye hanufaiki na lolote, wengine ndio hufaidikia bidii yake na hivyo mwenyewe kuwachwa akijuta. Kwa mfano, licha ya kumshtumu Mzee Mkasi na kufanya afungwe jela na pia ardhi yake kunyakuliwa, haya yote yalikuwa ni bidii ya kukama ndume maana hakufaidi chochote na hatimaye anapata Mzee Mkasi akiwa ameendelea na mimea yake kunawiri kuliko yake mwenyewe ambayo alilazimika kufyeka baada ya kuvamiwa na ugonjwa ambao hakujua ni upi (uk 21-24).

Mhusika mwingine aliyepewa jina la majazi ni Mzee Mkasi. Jina hili linatokana na neno kasi ambalo linamaanisha bidii, jitihada au juhudi. Mzee Mkasi anadhihirisha sifa hii ya kuwa na bidii. Licha ya umri wake na kuwa mkewe na wanawe waliaga kitambo, kitalu chake kimetutumaa na kinaendelea kunawiri kila uchao kutokana na bidii yake. mara nyingi mzee huyu alikuwa akipatikana kondeni mwake kama Soud anavyoashiria pale aliposhangaa kumkosa kondeni pake walipomtembelea. Mzee huyu amepanda mimea ya ainati kama vile migomba, mihogo, michungwa miongoni mwa mengine. Time anapofika anaandamana naye kwenda kukagua shamba lake na tunaelezewa yafuatayo kumhusu;

> …Kwani si inasemekana katika Kijiji kizima kwamba mzee huyu tu ndiye aliyeshonana na kazi na kuyayukiana na ardhi? Kwa kweli mzee Mkasi kila siku alikuwa na hamu na mapenzi makubwa ya konde zake. Kwake ardhi na konde ni vitu pekee vilivyobaki katika maisha yake mafupi yaliyosalia.
>
> Uk 169.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa Mzee Mkasi alikuwa mtu mwenye juhudi na bidii kazini mwake. Alipenda kufanya kazi yake kwa bidii na naguvu zake na ndio maana kwake kulinawiri kila kuchao.

Jina la mhusika mwingine mzee lililotumika ni Mponda. Ponda ni neno linalomaanisha kuvunjavunja kwa kutumia kitu kama jiwe, kinu na mchi miongoni mwa mengine. Hata hivyo mhusika mponda anatekeleza kitendo kilicho sawa na hiki kwa kutumia maneno hasa yanayokejeli na kufanya mtu kuhisi uchungu fulani au kuathirika kwa namna fulani. Mhusika huyu anapokuwa amelewa anarudi kwake akiwaponda maadui wake kwa maneno yanayobeba ukweli mchungu huku akiwa amejitia ulevi. Kwa mfano anamwingilia Mzee Mkamandume kwa kutetea uongozi uliopo na kuishia kukandamizwa pia naye. Mzee huyu anasema;

> …alisita akafyonza, "Zamani" aliendelea, sasa makusudi anapasa sauti yake juu, "zamani, tuligaragara vumbini na sasa twagaragara topeni – tofauti iko wapi? Si yaleyale tu. Tofauti ya ukame na umajimaji. Na … sasa si wapo wanaolalia vitanda vya dhahabu kama walivyolaloa wale tuliowatimua? Tofauti nini? Zamani si tulikuwa punda na mikia yetu, siku hizi sisi ni punda kasoro mkia. Na ikifika siku ya kujikomboa tunaota mikia ten ana kuifyata! Ha- ha – ha … ha – ha – ha … ha – ha- haaaa," alicheka kicheko cha stihizai kilichopasua makiwa ya usiku mpevu. Kisha alipiga hatua tena, huku akiimba wimbo wake maarufu…
>
> Uk 86

Mlengwa wa maneno haya ni Mzee Mkamandume ambaye hawaonani na Mzee Mponda toka ujanani kwa sababu ya kuchukua pande tofauti waki wa vita. Hata hivyo Mzee Mponda anaamua kumponda mwenzake kwa kumueleza ukweli. Vilevile jina lake linasadifiana na msemo wa ponda raha. Mzee huyu anaonekana kama mtu anayependa kuponda raha kwa kulewa. Ijapokuwa ni mhusika mdogo, tunapompata yu chakari na tunaelezwa kuwa ni hali ambayo ameizoea. Hivyo basi ulevi kwake ni njia moja ya kuponda raha.

### 4.11.8 Matumizi ya nyimbo

Data iliyokusanywa kutoka kwenye *Mkamandume (2013)*Mkamandume (2013) imedhihirisha matumizi ya nyimbo ni mbinu moja iliyofanikishwa kwa matumizi ya wahusika wazee. Nyimbo mbalimbali zilitumika katika riwaya hii kama vile wimbo maarufu wa Mzee Mponda anapokuwa amelewa;

> Mahodari wako wapi?
> Mahodari wako wapi?
> Wal'o kirusha fataki,
> Mahodari wako wapi?

Wal'o kifyeka machaka,

Mahodari wako wapi?

Wal'o kibeba jeuri,

Mahodari wako wapi?

Wako wapi?

Wako wapi?

Mahodari wako wapi?

Wote wameingia maji!

Mahodari wako wapi?

Wako wapi?

Wako wapi?

Uk 87

Wimbo mwingine ulitumika kwa kupitia mhusika Mzee ni ule uliokumbukwa na Bwan Sleyyum ambao walikuwa wakiimba nyakati za ujana wao wakati wa vikao vyao vya ulevi;

Kwenye masikani yangu ameingia tuyuri
Kamleta Bwana Mungu wa awali na akhiri
Kwa furaha chungu chungu nampokea vizuri

Karibu mpenzi wangu ewe ndege wa hariri
Karibu mgeni wangu ewe ndege wa hariri

Uk 260.

Nyimbo kadhaa zilitumiwa na mhusika Mzee Mkamandume kama vile nyimbo zilitumika wakati wa kupigania ukombozi wa taifa lao na pia kusherehekea ushindi wa kufukuzwa kwa wakoloni, mathalan;

Watoke wende kwao kwa salama na amani

Wachukue vil'o vyao vyetu wavitakiani?

Uk 382

Vilevile wimbo wa taarab uliokuwa ukienea redioni wakati ule baada ya ushindi na uongozi mpya kuchukua hatamu za uongozi;

Songa mbele songa mbele tumia yako maguvu
Si wakati wa kelele ondosha wako uvivu

Tumia yako maguvu        ondoa wako uvivu

Songa mbele, songa mbele

Uk 385

Wimbo mwingine uliofanikishwa kwa kutumia mhusika Mkamandume ni ule ulioimbwa na Kichalundu alipokuwa akizama (uk 427), na ule ambao Bwan Sleyyum alikuwa anakumbuka anapoenda kwenye kitalu au anakisikia kitalu kikimwimbia (uk 295).

Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo zilizotumika katika riwaya hii zilifanikishwa kwa kutumia wahusika wazee ili kuweza kuwasilisha ujumbe mahususi. Mbinu hii humsaidia mwandishi kubadili mtindo wake ili usiwe wa masimulizi mfululizo na kunasa makini ya hadhira.

**4.12 Hitimisho**

Sura hii iliangazia uchanganuzi wa data iliyokusanywa katika utafiti huu. Data kutoka riwaya mbili teule; *Mkamandume* (2013) na *Tumaini (2006)*, zilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya kinadharia. Mwandishi aliangazia wasifu wa waandishi wa riwaya zote mbili, kisha akaangazia sifa za wahusika, maudhui na hatimaye mbinu za lugha zilitumiwa na wahusika wazee.

Mount Kenya University

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia muhtsari wa utafiti huu, hitimisho la utafiti, mapendekezo yaliyotolewa na mtafiti.

## 5.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu ulichunguza nafasi ya wahusika wazee katika riwaya mbili zilizoteuliwa ambazo ni *Mkamandume* (2013), iliyoandikwa na Prof. Said A. Mohammed na *Tumaini (2006)*, iliyoandikwa na Dkt. Clara Momanyi. Utafiti huu ulikuwa na sura tano ambapo sura ya kwanza ilikusudiwa kujengea utafiti huu msingi thabiti kwa kuangazia maswala kama vile; usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na mipaka ya utafiti.

Sura ya pili nayo ilishughulikia kazi zilizofanywa na watafiti waliotangulia kuhusiana na masuala mbalimbali kama vile; wahusika na uhusika, wazee katika jamii ya Kiafrika, maudhui, fani pamoja na misingi ya kinadharia. Nadharia zilizotumika katika utafiti huu ni za mseto; nadharia ya uhalisia na umuundo. Misingi ya nadharia ya uhalisia iliyoongoza utafiti huu ni;

i) Maisha na matukio yote katika jamii hutambuliwa na kuelezwa kupitia uhalisi wake unavyodhihirika na wala sio unavyodhaniwa.

ii) Kazi ya mwandishi inafaa kudhihirisha ukweli jinsi ulivyo katika mazingira halisi. Mhimili huu ulimwezesha mtafiti kutathmini data aliyokusanya kama iliyodhihirisha ukweli wa mambo katika mazingira hasa kuhusu jinsi wahusika wazee wanavyoshughulikiwa na kufanya mambo yao katika jamii.

iii) Msanii huzingatia matatizo yanayokumba jamii wakati fulani kubaini vyanzo vyake. Mhimili huu ulimwezesha mtafiti kubaini maudhui yaliyowasilishwa kupitia wahusika wazee katika riwaya zote mbili.

iv) Msanii anatarajiwa kuwasawiri wahusika wake, matukio na mandhari yanayoakisi uhalisi wa mambo katika kipindi chake. Huu ulimwezesha mtafiti kutathmini hali ya wazee katika jamii husika katika vipindi mbalimbali walivyokuwa wakiishi.

Misingi ya umuundo iliyotumika katika utafiti huu ni;

Mount Kenya University

i. Muundo wa kazi ya kifasihi ndio humwezesha mtunzi kufikisha ujumbe anaokusudia. Mwandishi alitumia lugha kwa kuifinyanga ili kuwasilisha ujumbe wake. Alitumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa ujumbe umefika alivyotarajia.

ii. Lugha ndiyo humwezesha mtunzi kuelewa na kueleza ujuzi wake wa utendaji na mtazamo wa jamii kuhusu maisha. Kazi ya mwandishi huashiria ubingwa wake, ubingwa huu hujitokeza katika jinsi anavyofinyanga lugha yake ili kuwasilisha ujumbe wake ipasavyo, na hivyo hutumia mbinu mbalimbali. Sura ya nne ilishughulikiwa uwasilishaji na uchambuzi wa data iliyokusanywa. Data iliyokusanywa imewasilishwa kwa njia maelezo na mifano kutolewa.

**5.2 Hitimisho la utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ambayo ni; kutambua sifa za wahusika wazee, kutambua maudhui yaliyowasilishwa kupitia wahusika wazee na ni kuangazia jinsi wahusika wazee wametumiwa kufanikisha mbinu za lugha katika riwaya hizi mbili. Utafiti huu ulibaini yafuatayo;

Lengo la kwanza liliangazia sifa za wahusika wazee katika riwaya teule. Mtafiti alibaini kuwa wahusika wazee katika riwaya ya *Tumaini* (2006) wamepewa sifa mbalimbali kama vile; kuwa na hekima, kuwa wahafidhina, wacheshi, wenye bidii, katili, wafisadi, wapyoro, watambuzi, wenye hasira, waoga, wasiri, wapatanishi na wenye chuki. Wahusika hawa ni pamoja na Mzee Masumbuko, Mzee Sulemani, Mzee Sudi, Mzee Okwemba, Mzee Chumo, Mzee Lusimbo, Mzee Seyai na Mzee Majungu.

Katika *Mkamandume (2013)*), wazee waliotambuliwa na kuangaziwa ni; Mkamandume, Mzee Mkasi, Mzee Mponda, Bi. Reja, Bi. Mwana, Bw. Sleyyum, Babu Yakobo pamoja na wazee wa Kijiji. Wahusika hawa walipewa sifa mbalimbali kama vile: wenye hekima, wacheshi, wapelelezi, waliotamauka, katili, wahafidhina, wenye dharau, washauri, wenye mapenzi ya dhati, watetezi wa haki, wasamehevu na wenye bidii.

Wahusika hawa walifinyangwa na mwandishi kwa njia ambayo inawafanya kufanana sana na wahusika wazee katika jamii. Sifa walizopewa zinadhihirisha uhalisia uliopo katika jamii kuhusu tabia za wazee. Wahusika hawa walipewa sifa chanya na hasi kama vile ukatili, chuki, dharau ambazo mwandishi alikuwa na lengo la kukejeli miongoni mwa wahusika wazee. Alifanya haya kwa kuhakikisha kuwa wazee hao wamejutia sifa hizi hasi kama vile Mzee Mkamandume. Kando na kukejeli sifa hasi katika jamii, mwandishi alilenga kuhamasisha jamii kuhusu sifa na hali za wazee katika jamii.

Lengo la pili la utafiti huu ulikuwa ni kutambua maudhui ambayo yaliwasilishwa kupitia kwa wahusika wazee. Mtafiti alibaini kuwa wahusika wazee wametumiwa kuendeleza na kukuza maudhui mbalimbali katika riwaya zilizoteuliwa, hata hivyo utafiti huu uliangazia maudhui yafuatayo kwa kina; Katika riwaya ya *Tumaini (2006)*; maudhui ya ukeketaji, ndoa za mapema, elimu, ukatili, uongozi mbaya, bidii, urafiki, mila, desturi na tamaduni, na migogoro. Na katika *Mkamandume (2013)*); maudhui ya utamaushi, ukatili, uongozi mbaya, majuto, mila, tamaduni na desturi, changamoto za uzee na ukulima na changamoto zake. Ilibainika kuwa maswala yaliyoangaziwa kupitia wahusika wazee ni yale yanayoashikiliwa na wazee na kuathiri wazee katika jamii kama vile kushikilia mila zilizopitwa na wakati kama vile ndoa za mapema na ukeketaji jambo ambalo waandishi walilenga kupiga vita na kutetea elimu ya mtoto wa kike. Katika *Mkamandume (2013)*), mwandishi alilenga kuibusha mjadala kuhusu changamoto ambazo wahusika wanapitia katika jamii kama vile magonjwa, kupuuzwa, kufanyishwa kazi za sulubu, kukosa mishahara na kusongwa na mawazo kama ilivyodokezwa kupitia wahusika kama Bwan. Sleyyum na Mzee Mkamandume. Hii inadhihirisha kuwa wahusika wazee ni kiungo muhimu katika uandishi na utungaji wa kazi za fasihi ili kuwasilisha maudhui na kufanikisha dhamira ya mwandishi.

Lengo la tatu lilikuwa ni kuangazia jinsi wahusika wazee walivyofanikisha matumizi ya lugha katika riwaya teule. Utafiti ulibaini kuwa, kwa kutumia wahusika wazee kulimwezesha mwandishi kutumia mbinu mbalimbali za lugha kama vile, katika riwaya ya *Tumaini (2006)*; methali, nahau na misemo, tashbihi, lafudhi, dayalojia, maswali ya balagha, majazi, kinaya, taswira na wimbo. Na katika Mkamandume (Mohammed 2013), matumizi ya jazanda/sitiari, taswira, kisengere nyuma, uzungumzi nafsi, takriri, dayalojia, majazi na nyimbo. Mbinu hizi ziliweza kufanikishwa kwa kutumia wahusika wazee. Mbinu hizi zilijitokeza vizuri zaidi kupitia wahusika wazee na hivyo kumwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe aliolenga.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulipendekeza kuwa viongozi na mashirika mengine yanayoshughulikia maswala ya wazee yanafaa kuangazia na kuyatafutia suluhisho matatizo yanayowakumba wazee katika jamii ili kuwawezesha kuishi maisha yanayopendeza na kuweza kuhifadhi hazina hii muhimu. Baadhi ya changamoto zinazowakumba wazee katika jamii ni kama: umaskini, magonjwa, mapuuza, ukosefu wa usaidizi, unyonge, kufanyishwa kazi za sulubu, kuzongwa na mawazo na kushindwa kukimu jamii zao.

Mtafiti anapendekeza kuwa washika dau katika sekta za elimu pamoja na ukulima kutafuta mbinu za kuwahamasisha vijana kushiriki katika kilimo ili kuboresha mazao na kuongeza mavuno baada ya kubainika kuwa wahusika wazee ndio wanaojihusisha na ukulima zaidi na wahusika vijana hawaonekani kushiriki katika ukulima ila tu wanapowasaidia wazee. Hali hii inachangia kuzorota kwa hali ya ukulima katika jamii na taifa maana wazee hawana nguvu za kufanya zaidi na elimu ya kisasa ambayo inaweza kutumika kuboresha kilimo.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti zaidi

Maswala yanayowazingira wahusika wazee katika riwaya za Kiswahili ni mengi na hayajashughulikiwa kikamilifu kwa kuwa kazi moja haitoshi kushughulikia maswala haya yote. Mtafiti anapendekeza utafiti zaidi kufanywa kuhusu wahusika wazee katika fasihi ya Kiswahili hasa katika ushairi na tamthilia, vilevile kuhusu usawiri wa mwanamke mzee katika fasihi ya Kiswahili na uhusiano uliopo baina ya wahusika wa umri mbalimbali katika fasihi.

## 5.6 Hitimisho la sura

Sura hii iliangazia masuala kama vile muhtasari wa utafiti huu, hitimisho na vilevile mapendekezo ya utafiti.

Mount Kenya University

## MAREJELEO


Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*, Belmont, Wadsworth Publishing Company.

Chacha, W. (2013), Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Nguzo Mama na Mama ee. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chiangong, P. (2018). 'A Critical Analysis of the Role of Aberewa (Old Woman) in Bill Marshall's *Asana*'. In *Alter und Geschlecht: Soziale Verhältnisse und Kulturelle Repräsentationen*. Elisabeth Reitinger Ulrike Vedder, and Pepetual Mforbe Chiangong(eds). Wiesbaden: Springer Verlag, 143–162.Drabble, (1993)

Chilala, F. K. (2015). Standing in the circle: Images of old people in African literature. *Zambia Social Science Journal, 6*(1), 27–40.

Creswell, J. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches,* Thousand Oaks, CA SAGE Publications.

Danowski, J. L. (2011). *The portrayal of older characters in popular children's books: A content analysis from 2000 to 2010* (Master's thesis, Brigham Young University). *BYU ScholarsArchive*. https://scholarsarchive.byu.edu/etd/2469

Drabble, M. (ed), (1993). *The Oxford Companon to English Literature*. Oxford, Oxford University Press.

Flaubert, B. (1990). *Landmarks Of World Literature*, New York: Cambridge university Press.

Fowler J. (1975). *A Dictionary of Modern English Usage.* Oxford, Oxford University Press.

Gatere, J. (2019), Usawiri wa Familia ya Kisasa Katika Fasihi ya Watoto Nchini Kenya Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Hawthorn J. (ed), (2010). *The Routledge Companion to Postmodernism.* London, Routledge.

Hegel, G. (1971). *Introduction to Aesthetics,* Oxford: Clarendon.

Hill, J. (1977). *The Romantic Imagination*, London: Macmillan Press Ltd.

Hungwe, C., Mugari, Z. E., na Hungwe, E. (2022). Representations of Ageing in Contemporary Zimbabwe: A Gerontological Reading of NoViolet Bulawayo's (2013) *We Need New Names. Journal of Population Ageing (2024)*17:111-128 https://doi.org/10.1007/al2062-022-09380-3


Mount Kenya University

Kanwa, O. (2022), Usawiri wa Wahusika wa Kiume Katika Riwaya za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanawake. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Karimi, S. (2022), Nafasi ya Wahusika Wendawazimu katika Riwaya Teule: Kidagaa Kimemwozea na Mkamandume. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kombo, D.  na Trump, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction,* Nairobi: Paulines Publication.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology. Methods and Techniques*, New Delhi: New Age International.

Leech G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London, Longman publishers.

Leech G. (1981). *Language and Tact*. Oxford, Oxford University Press.

Lukacs, G. (1963). *The Historiccal Novel.* London, Pengui Books.

Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism*, London: The Marlin Press.

Macdowell, A. (1918). *Realism: A study in Art and Thought,* London; Constable and company.

Malaza A. na Addison C. (2013). The figure of Older Woman in African Fiction. *Current Writing: Text and Reception in Southern Africa, 20(1), 26-39*

Mathooko, J. na Wenzake (2007). *Academic Proposal Writing*, Nakuru: Amu Press.

Mbatia, H. (2001). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mlokozi, M., na Mrikaria, G. (Wah) (2009). *Mulika* na. 28. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mohamed. S. (2013). *Mkamandume*, Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Momanyi C. (2006). *Tumaini,* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki Wa Fasihi*, Nairobi: East African Educational Publishers.

Mount Kenya University

Musyoka, T. (2008). Usawiri wa Vijana Katika Tamthilia Teule za Kiswahili Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mutua, J. (2017). Mitazamo ya Waandishi wa Kike na Kiume Kuhusu Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili Tasnifu ya Uzamifu (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Pwani.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi. Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za Fasihi*. Augustane College; Rock Island.

Ruo, K. (1989). *Nguzo Za Ushairi Wa Kiswahili*, Nairobi: Macmillan.

Saussure F. (1974). *Course in General Linguistics.* London, Fontana-Collins.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi,* Dar es Salaam; Dar es Salaam Press and Publicity Centre.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi; Focus Books.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.

Wellek, R. (1961). *"The Concept of Realism in Literary Scholarship".* Neophilologus. London: J Cape.

https://www.unhcr.org/older-persons Ilipakuliwa 14/09/2023; 14:24

Mount Kenya University

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1: IDHINI YA CHUO

**Mount Kenya University**

REF: **MKU/ISERC/4078**
TO: **BETT KIPLIMO ANDREW**

Date: 07 August 2024

REG. **MAKI/2022/51273**

Dear Sir/Madam

**RE: NAFASI YA WAHUSIKA WAZEE KATIKA RIWAYA TEULE**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **2964**. The approval period is **07/08/2024 - 06/08/2025.**

This approval is subject to compliance with the following requirements:

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used

ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**

iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification

iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours

v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions

vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal

vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

Yours sincerely,

MOUNT KENYA UNIVERSITY
ETHICS REVIEW COMMITTEE
P. O. Box 342 - 01000,
THIKA

**Dr. Alfred Owino, PhD**
**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 | +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke  Web: www.mku.ac.ke

## KIAMBATISHO II: BARUA YA CHUO

# Mount Kenya University

MKU

## DIRECTORATE OF GRADUATE STUDIES

**MAKI/2022/51273**

**8th August, 2024**

***National Commission for Science Technology & Innovation (NACOSTI)***
***Off Waiyaki Way, Upper Kabete,***
***P.O Box 30623- 00100***
***NAIROBI, KENYA***

Dear Sir/Madam,

**RE: BETT KIPLIMO ANDREW – REGISTRATION NO. MAKI/2022/51273**

The purpose of this letter is to introduce the above named student who is pursuing **Master of Arts in Kiswahili** in the Department of **Psychology, Languages and Humanities** in the School of **Social Sciences.**

The title of the research is **"Nafasi ya Wahusika Wazee Katika Riwaya Teule."** It has been cleared by the University's Ethics Review Committee (Certificate attached) and now has to proceed to the field to collect data between **August, 2024 and October, 2024.**

Any assistance accorded to the student will be highly appreciated.

Thank you.

Mount Kenya University
P.O. Box 342-01000 Thika
Office of the Director
Graduate Studies

**Dr. Samuel M. Karenga, Ph.D**
**Director, Graduate Studies**
**Enc.**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.

## KIAMBATISHO III: IDHINI YA NACOSTI


REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 719607

Date of Issue: 13/September/2024

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. Andrew kiplimo Bett of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Uasin-Gishu on the topic: Nafasi ya Wahusika Wazee katika Riwaya Teule for the period ending : 13/September/2025.**

License No: NACOSTI/P/24/39987

719607

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions